

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Saba – Tarehe 14 Aprili, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatuh Asubuhi)*

**D U A**

Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo ni Siku ya Alhamisi, kama kawaida yetu, siku hii dakika thelathini za kwanza tunakuwa na maswali kwa Waziri Mkuu. Anayeanza ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE (KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI):** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la kwanza kwa Waziri Mkuu.

Kwa kuwa Katiba ni Roho ya Taifa; na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya mabadiliko au kuandikwa upya kwa Katiba ya Nchi, jambo ambalo Serikali imeridhia kupitia kwa Rais; na kwa sababu Serikali ililetia Muswada katika utaratibu wa haraka, Muswada wa *Constitution Review*:-

Je, baada ya Serikali kuona *reaction* ya wadau mbalimbali wakiwemo wanazuoni, Vyama vya Siasa, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wadau wengine mbalimbali, ambao wanafikiri kwamba, mchakato huu pengine unakwenda kwenye kasi ambayo badala ya kujenga inaweza ikatia nyufa katika mahusiano yetu; ni kwa nini Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu wasitoe tamko rasmi la Serikali la kukubaliana na utashi wa wadau ili kuusogezza Muswada huu mbele Wananchi wapate fursa ya kutosha ili kuweka mahusiano mema ambayo tunategemea katika Taifa letu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Mbewe, ambaye ndiye Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali imewasilisha Muswada hapa Bungeni na tuliwasilisha kwa Hati ya Dharura, kwa dhamira njema kabisa kwa kuwa tuliamini kabisa kwamba, watu wana hamu na shauku kubwa ya kutaka kufikia hatua ya

pili ya mchakato, kwa maana ya Katiba yenewe baada ya kuwa Tume ya Katiba imeundwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha Bungeni, kilichopo ni utaratibu ndani ya Bunge. Nimearifiwa kwamba, Kamati ya Katiba na masuala ya Bunge, ilikutana kuzungumzia yaliyojitokeza wakati wa *Public Hearing* walipokuwa wanakutana na Watanzania. Kiutaratibu, maoni yao hayo yanapaswa kwenda kwa Spika, Spika akishayapata na kuyachambua vizuri, yeye sasa akiona inafaa, akiona kuna uzito kutegemea na Kamati imeshauri nini, anaweza kushauriana na Serikali ili Serikali nayo iweze kuridhia maoni hayo au matakwa hayo kulingana na uzito wa jambo lenyewe lilivyo.

Hapa niliposimama, bado sijapata taarifa yoyote wamefikia wapi katika hatua hiyo. Kwa hiyo, sisi tumejipanga tukiamini kwamba, kama tulivyokuwa tumeleta jambo hili Bungeni na kama hakutakuwa na maoni tofauti, tutaendelea nalo. Endapo tutapata maoni mengine kwa uzito stahiki, sisi kama Serikali, tutaridhia tu kwa sababu hatuna tatizo; nia ni njema; ni kutaka tusonge mbele kwa namna ambayo Watanzania wote tutaridhika kwamba imekwenda vizuri.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE (KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI):** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri Mkuu; na kwa sababu jambo hili kwa kweli limezua hofu kubwa katika Taifa kutokana na uzito wake; pamoja na ukweli kwamba Ofisi ya Serikali ama kupitia Waziri Mkuu inapata taarifa za Bunge kutoka kwa Spika; ni kwa nini Waziri Mkuu asitumie fursa hii kuliambia Taifa kwamba; nia ya Serikali kwa sababu kama ni mawazo ya wadau yamesikika kupitia vyombo mbalimbali vya habari na siyo jambo la siri; yeye binafsi kama Waziri Mkuu na kama Mwakilishi wa Serikali hapa haoni ingekuwa jambo la busara zaidi kama angetangaza tu hapa kwamba tumeridhia kwamba tunauondoa Muswada huo ili mambo mengine yaweze kuendelea? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninajua Mheshimiwa Mbobe anataka niseme sawa tu; *you know*, hatuwezi kwenda hivyo, sisi tuzingatie taratibu tu, wala halina haraka hili. Pengine niwatoe hofu Wananchi, maana unaposema wana hofu kubwa na mimi ninajiuliza ni hofu ya nini?

Kwa sababu jambo hili ni suala la maoni yanayojitokeza katika kujaribu kuona ni namna gani tunaweza tukaja na mambo ambayo tunadhani yatatuwezesha kuwa na Katiba. Sasa fursa hii ya kuweza kutoa maoni na kupata maoni mazuri ya kutusaidia kujenga nchi yetu, hakuna sababu ya kujenga hofu yoyote kwa Wanzania na wala hii hatua tuliyofikia sidhani kama ina hofu yoyote, hofu ya lipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sioni kama kuna tatizo hata kidogo, suala kubwa kama nilivyosema, Kamati yenu ya Bunge, itakapokuwa imetoa maelezo yake kwa Spika, kiutaratibu Spika atapima uzito ataniambia maana mimi ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni. Mimi ni Mtanzania kama wewe, na kwa dhamira nzuri

tuliyonayo, nitaonekana mtu wa ajabu sana kama ushauri nitakaoupata kutoka kwa Spika, mimi niupuuze niseme naendelea hata kidogo siwezi kufanya hivyo!

Mheshimiwa Spika, ninatambua vilevile jambo hili ni kubwa siyo dogo; kwa hiyo, kwa uzito tutakaouona sisi tunaamini mambo yatakwenda vizuri. Ndugu yangu Mbowe mbona haraka, poa tu. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Suala hili lipo mikononi mwa Spika na mimi nina wataalam wangu. Tunaendelea, leo tunao Waheshimiwa Wabunge kumi na sita walioomba kuuliza maswali; anayefuata hapa ni Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mradi wa *Sourthen Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCT)*, umehusisha Mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma na kuitenga Mikoa ya Mtwara na Lindi:-

(a) Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu unaweza kutuambia sasa ni kwa nini Mikoa ya Mtwara na Lindi imetengwa katika Mradi huu wa *SAGCT*?

(b) Je, kuna hasara yoyote itakayopatikana kama Mikoa hii itaingizwa katika Mpango huu ili na wao waweze kushiriki pamoja na Mikoa mingine iliyopo ndani ya Mradi huu?

(c) Je, ni lini Serikali ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Faith, maswali ni mawili tu.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninataka nimtoe hofu tu, asidhani kwamba Mradi huu umetenga baadhi ya mikoa hapa; ni kama tulivyowahi kuja na kitu kinachoitwa *Southern Corridor*, ambayo *basically*, inachukua Mikoa ile ya Kusini kwa lengo mahususi la kujaribu kuona ni namna gani Mikoa ile inaweza ikaendelezwa kutegemeana na fursa zilizopo katika eneo lile. Tulipoanzisha ule Ukanda (*The Southern Corridor*), hakuna aliyeuliza kwamba, kwa nini mikoa mingine mnaitenga hapana! Kwa sababu Programu inapokuja, ina mambo fulani ambayo inajaribu kusaidia katika Ukanda unaohusika. Kwa hiyo, *SAGCT basically*, tunachojaribu kuona ni kwamba, Mikoa hii ndiyo yenye fursa kubwa ya kuweza kuzalisha zaidi kwa sababu ya mvua nzuri, udongo mzuri na uwezekano wa *irrigation* ni mkubwa sana.

Kwa hiyo, badala ya kuiacha tukawa tunaiona kama Mikoa mingine ambayo ina matatizo makubwa, tukaona labda tutafute namna ya kutumia fursa zilizopo pale ziweze kutusaidia kuzalisha zaidi, zilete chachu pana zaidi ili kuweza kulisha nchi kwa uhakika zaidi. Vilevile kusaidia watu waliomo katika Ukanda huo kwa kutumia fursa zilizopo

pale. Haina lengo zaidi ya hilo kwamba pengine ni kutenga hapana; ni kujaribu kutumia fursa zile vizuri zaidi kwa kadiri itakavyowezekana.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri, ninaomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mikoa ya Mtwara na Lindi ni Mikoa pekee ambayo inazalisha Zao la Korosho kwa wingi Tanzania nzima; je, Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni sasa kuna kila aina ya sababu kuiingiza Mikoa hii ya Lindi na Mtwara katika Mpango huu wa SAGCT?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama utakuwa umeangalia vizuri Mpango ulivyo, ni kweli kwamba, tuna eneo ambalo tumelilenga, lakini kuna vitu vilevile ambavyo tumevifikiria katika ule Mpango. Sasa zile *units* zingine ambazo tumezifikiria sisi ni zile ambazo zinaweza zikafikiriwa kutegemea na aina ya uzalishaji unaoendelea katika eneo hilo. Kwa hiyo, Mikoa ya Kusini kwa maana ya mpango wenyewe ulivyo na muunganiko wake hasa tutakapokuwa tunatazama masuala ya miundombinu, utaiona itaingia katika Mpango huu. Kwa kuwa ni eneo lingine muhimu, kama tulivyofikiria upande wa Kigoma na maeneo mengine ambayo tulifikiri yangeweza kuwa ni mazuri sana kwa ajili ya kuibua na kuanganishwa katika Mradi mzima, tutafifikiria pia na Mikoa hiyo.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, leo Redio Tanzania haitatutangaza kwa sababu matatizo ya jana bado hawajaweza kuyarekebisha.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, ikiwa ni mara yangu ya kwanza niweze kumwuliza maswali Waziri Mkuu katika Kipindi hiki cha Alhamisi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa maeneo mengi na kwa ujumla maeneo yote ya Mikoa ya Kusini yapo nyuma katika Sekta zote; za Elimu, Afya na Miundombinu; na kwa kuwa Mfuko wa Hazina ni mmoja ndani ya Taifa letu; na kwa kuwa Mikoa hiyo ni wazalishaji wakubwa na inaongezea pato kubwa la Serikali katika Taifa hili:-

Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa makusudi wa kuona hilo ili kuweza kuiendeleza Mikoa hii kutokana na umaskini ambao wanakabiliwa nao?

**SPIKA:** Ahsante. Siku nyingine usisome swali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye takwimu ambazo Kitaifa zinapatikana, utaona kwamba, ipo Mikoa ambayo ndiyo inadaiwa kwamba, iko chini sana kimaendeleo. Mikoa wa mwisho kabisa inasemekana ni Singida, unafuata Mikoa wa Dodoma, Mikoa wa Kagera na mingine miwili, mitatu, hivi. Mtwara na Lindi si mionganoni mwa ile Mikoa ya mwisho kitakwimu katika eneo hili la maendeleo, lakini ukweli utabaki pale pale kwamba, Mikoa yote kwa ujumla au Wananchi wote kwa ujumla ni lazima tutazame changamoto tuliyonayo; ni kubwa kwa maana ya hali ya umaskini ambayo bado ukiziweka katika uwiano bado Taifa letu linaonekana kwamba,

Watanzania wanaishi chini ya dola moja, ndiyo maana swalı lako linakuwa ni la muhimu sana bila kujali sana takwimu hizi mmepangwa wa ngapi, kwa sababu hata wale wanaoonekana juu ni kitakwimu kwa maana ya uhalisia wake, bado kuna changamoto kubwa.

Sasa tunachoweza kutazama kwa Mikoa hiyo ni fursa ambazo zinaanza kujitokeza pale. Bahati nzuri Mtwara mna fursa ambayo inajitokeza waziwazi ya upatikanaji wa gesi. Gesi ile itaweza kuwasaidia sana kuibua Miradi mbalimbali na hasa mtakapokuwa mmeifikia hatua kubwa zaidi ya kuzalisha umeme kwa wingi zaidi. Hata ukienda kwenye kina kirefu cha bahari, bado eneo hilo ndilo lenye uwezekano mwangi zaidi wa gesi ambao tunadhani mlango wake mkubwa bado utaendelea kuwa ni Mtwara. Kwa hiyo, kwa mipango ilivyokuwa, utakaloliona ni kwamba, bandari ile itakuwa kubwa, Lindi nayo itaingia pale na tunaamini kabisa italeta mbubujiko mkubwa zaidi katika kupatikana ajira lakini na maendeleo kwa ujumla.

Kwa hiyo na mimi ninadhani ni kujipanga vizuri, tuone namna tutakavyotumia fursa sasa ambazo zinajitokeza. Kwa upande wa Lindi, ninadhani vilevile tutaitumia vizuri sasa Mbunga ile kubwa ya *Selous Game Reserve* kuona kama tunaweza kuimarisha utalii, kwa sababu nao ni chachu kubwa ambayo inaweza kusaidia Watanzania katika eneo hilo. Kubwa kwa Wananchi wa Lindi na Mtwara ni kujipanga kufanya kazi kwa bidii zaidi ili fursa hizo ziweze kuwanufaisha zaidi, *otherwise*, utaona fursa zipo lakini hatua za maendeleo bado zitakuwa ziko chini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Baruani umeridhika; kama umeridhika siyo lazima uulize swalı?

**MHE. SALUM H. BARWANY:** Ahsante sana.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nimwulize swalı Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Serikali imeshatoa tamko kuhusiana na bei ya sukari nchini na alianza Mheshimiwa Rais na baadaye ukafuatia wewe ukiwa ziarani Kagera kwamba ni lazima bei ya sukari ishuke; na kwa kuwa maeneo mengi hapa nchini bado bei ya sukari haijashuka: Je, Waziri Mkuu anawaambia nini leo Watanzania kwamba ni mikakati mibaya iliyopangwa au ni utekelezaji mbaya ambao kule chini bado haujatekelezwa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba, sukari ni zao moja ambalo ni muhimu sana kwa maisha ya wanadamu, kwa sababu Watanzania wengi sasa tunatumia sukari kwa ajili ya chai, ndiyo maana uliona Serikali ilibidi iingilie kati na kutoa maelekezo ya kusaidia wanaohusika na biashara ya sukari kujaribu kusaidia Taifa kwa kuona kama sukari ile inaweza ikauzwa kwa bei ambayo watu watasema angalu kidogo inawapa uwezo wa kuweza kununua na ndiyo maana ukaona tukatoa tamko lile. Kwa taarifa ambazo ninazipata sasa kila wiki, yapo baadhi ya maeneo ambako

zimekuwepo jitihada nzuri, bei ile imeshuka kwa viwango tofauti tofauti kati ya eneo moja na jingine, lakini angalau ipo dalili ya kushuka kwa sukari.

Changamoto tunayoipata sisi ni kwa sababu baada ya kufuatilia utaratibu mzima baada ya kuona sukari inavyotoka viwandani kwenda kwa wauzaji wakubwa na hatimaye wauzaji wadogo, wauzaji wenyewe wadogo ambao wapo katika maeneo ya vijijini kwa sababu wao wanasema hali ya maisha imepanda, kwa hiyo, mahali pazuri anapoona anaweza akatengeneza fedha kidogo za kuweza kumsaidia ni kwenye sukari. Sasa tumelazimika kujaribu kuziomba Halmashauri zetu zijaribu kubanana na hawa ambao ni wauzaji wadogowadogo ili kusaidia kupunguza bei.

Kwa kuwa sehemu nyingi wametuambia, bei ile ya sukari kwa kuongeza faida ambayo wamejipangia wao wenyewe walisema kwamba, inawezekana kabisa sukari ile ikauzwa kwa bei tulioisema bila tatizo karibu maeneo yote na maeneo mengine kwa bei ndogo zaidi. Waswahili kila mmoja anataka fursa kwa kadiri anavyoona, maana hata Kagera pale nimekwenda ingawa ni pua na mdomo, lakini unakuta nako inanunuliwa kwa bei kubwa kuliko hata maeneo mengine ambayo yako mbali na kiwanda. Kwa hiyo, ni watu tu kutumia ile fursa kwa ajili ya kujaribu kujipatia visenti bila kujali hasa maslahi ya wenzao. Jitihada zinaendelea, ninajua ni changamoto kubwa na kazi kubwa. Ninaendelea kuwasahihi Watanzania, hasa wale wenyewe maduka madogomadogo, wajaribu kuliona hili ili kuwasaidia Watanzania wenzao waweze kupata sukari kwa bei ambayo ni nafuu.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini bado nina swali moja nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imeweka bei moja kwa nchi nzima lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza inategemea na baadhi ya maeneo; na kwa kuwa Serikali imetoa tamko hili lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo wanazalisha sukari bado wanataka bei iendane na bei ambayo Serikali imetamka lakini siyo sahihi; na kwa kuwa wao ni wazalishaji bei yao inapaswa kuwa chini kuliko sehemu nyingine yoyote ambayo wanatumia sukari; je, Waziri Mkuu anatoa tamko gani kuhusiana na maeneo ambayo wanazalisha sukari?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nilipojibu ile sehemu ya kwanza, maana nimekwenda Moshi TPC, nikawauliza wakanipa maelezo mazuri sana, lakini unapokwenda kwenye maduka ya wauzaji wadogowadogo na wao wanaona ndiyo wakati wenyewe wa kutengeneza fedha. Nikawashauri vizuri *TPC*, nilichokiona kizuri ni kwamba, wanaruhusu hata mtu yejote kwenda kununua pale sukari ilimradi iwe angalau ya kiwango cha tani moja. Kwa hiyo, nikawaambia Viongozi wa Mkoa waliokuwepo pale, hebu waambieni hata Vyama vya Ushirika, *SACCOSS* hizi mkiungana, mnawenza kuja kupata sukari hapa ya tani moja na ninyi kama ni Watanzania wema, mkaenda kuiuza kwa bei ambayo itasaidia kuwapa Watanzania unafuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kinachonisumbua mimi ni kwamba, watu wanakuwa wabinafsi kuliko kujali hii hali ambayo tunasema inawasaidia na watu wengine wote. Kwa hiyo, ninataka nimwambie dada yangu Mtema pale kwamba, acha tuendelee na hizi

jitihada za kubanana na kuendelea kuwasihii Wananchi watusaidie na wao vilevile kujaribu kuwabana hawa ambao *basically* unakuta hawana sababu hata kidogo, ukiachilia mbali hiyo kwamba na wao wangependa kunufaika kidogo katika kipindi hicho.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunionna.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, barabara ni kiungo muhimu sana katika kuleta maendeleo katika nchi yetu. Je, kwa nini Barabara ya Ndundu - Somanga ambayo ndiyo itafunga uchumi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara inasuasua?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sikumpata vizuri, anasema kwa nini Ndundu - Sumanga?

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara kutoka Ndundu hadi Somanga kilomita 60 ambazo pekee zimebaki kufungua barabara kutoka Dar es Salaam hadi Mtwara?

**SPIKA:** Swali hili moja kwa moja ni la Waziri wa Ujenzi sasa, siyo la kisera hilo; sijui Waziri Mkuu ninadhani unalifahamu?

**WAZIRI MKUU:** Ngoja tumtie moyo tu kwa sababu ni kweli anajua kwamba; ni la Mheshimiwa John Magufuli. Ninachowea kusema ni kwamba, asikate tamaa na wala asifikiri *ime-abandon* ule Mradi hata kidogo, ule Mradi bado tunao na ye ye mwenyewe anajua hali tuliyopambana nayo kati ya eneo lile katika kujaribu kuifungua kwa haraka zaidi. Eneo lile ni eneo ambalo lina chepechepe, kama mbuga ambazo zimechangia sana katika kuchelewesha Mradi ule kwa kiasi fulani. Kwa *speed* tunayokwenda nayo, tunaamini Mradi ule utakamilika, kwa sababu maeneo mengi tumeshafanya mambo mazuri, lililobakia ni eneo dogo sana la kilomita kama 60. (*Makofii*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Bajeti ya Mwaka 2009/2010, Serikali ililetia Bungeni mapendekezo ya kutenga zaidi ya shilingi trilioni 1.7 kwa ajili ya kuhuisha uchumi (*Stimulus Package*) na Serikali iliahidi hapa Bungeni ya kwamba, Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, atafanya Ukaguzi Maalum kwenye eneo hili. Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ametoa taarifa yake. Katika taarifa yake, pamoja na kuonesha kwamba, kuna zaidi ya shilingi bilioni 48 ambazo ameshindwa kuzithibitisha kama zilitoka kwa taratibu zinazotakiwa. Pia amesema kwamba, Serikali imemnyima taarifa muhimu ikiwemo orodha ya watu na makampuni ambayo yalifaidika na mpango huu. Mheshimiwa Waziri Mkuu; unatoa kauli gani kuhusu suala hili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sijui Mheshimiwa Kabwe maana mimi ndiyo Waziri Mkuu, ndiyo ninayeshughulika na masuala ya Serikali kwa upana wake. Kwa bahati mbaya sana, hiyo taarifa kwamba aliomba baadhi ya taarifa kutoka Serikalini tukamnyima, nilikuwa sijazipata. Kwa kuwa taarifa hizo nimezipata juzi, yaani kwa maana ya ma-book yale; na *so long* ndiyo ninazipitia, labda nipe nafasi nikishapata nafasi

ya kuipitia *then take up issue seriously*, kwa sababu hatuna sababu ya kumnyima ye ye ndiyo Mkaguzi wa Hesabu na kwa nini tuiseme hapana.

**SPIKA:** Amesema atakupa habari zaidi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninaomba nimsomee sehemu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, haitasaidia. Anasema ye ye anaipitia, sasa ukimsomea si unatupotezea muda wetu sisi?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba unipe fursa ya kuuliza.

**SPIKA:** Usimsomee, wewe uliza unachotaka kufanya nyongeza, amesema ye ye hajapata na atakwenda kujisomea huko.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ningependa nimwulize kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuzingatia kwamba nchi yetu ndiyo Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utoaji Taarifa na Uwajibikaji juu ya Afya ya Mama na Mtoto katika kutekeleza Malengo ya Milenia Namba 4 na 5. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuunda Kamati ya Kitaifa ambayo itahusika katika ufuatilaji wa suala zima katika ngazi zote kuanzia Vijiji hadi Taifa? Ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Wambura, kwa swali lake zuri. Tukiri kwamba, eneo moja ambalo bado tuna changamoto kubwa ni hili ambalo linahusu hali ya mama na mtoto. Ninaposema hivi, ninajaribu kuonesha tu matatizo ambayo yanajitokeza ambayo yanababisha vifo hasa kwa akina mama wajawazito wakati mwengine kutokana na sababu ambazo tukijipanga vizuri, tunaweza tukaokoa maisha ya akina mama wengi.

Tumepiga hatua kidogo, kwa maana ya vifo vya watoto wadogo, kutokana na juhudhi kubwa tumezitoa kwa kujaribu kuhakikisha kwamba, chanjo inapewa umuhimu mkubwa. Kwa hiyo, kuna *improvement* kidogo katika eneo hilo. Bado vifo vya akina mama ni vingi. Kwa hiyo, ninataka nikubaliane kabisa na wazo hilo na nilipokuwa Marekani pale *New York*, wakati wanazungumza utekelezaji wa suala la *MDGs*, eneo lililojitekeza kwa nguvu sana ni hilo na baada ya kurudi tumewataku wenzetu wa Wizara ya Afya, tulipe eneo hili mtazamo wa karibu zaidi ili tuweze kuona namna gani tunaweza tukafanya kazi ya kupunguza vifo vya akina mama kwa haraka kwa kadiri itakavyowezekana.

Bado tuna changamoto nyingi vijiji, ingawa kweli tuna zahanati na vituo vya afya, lakini tunahitaji waganga na wauguzi wengi. Hata pale tutakapowapata, bado utaona kumtoa mgonjwa kutoka Kijiji kwenye Kata ambako ndiyo kwenye Kituo cha Afya nako kunahitaji mikakati mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana juzi nilikubali kufanya kazi moja hapa ya kujaribu kunadi matumizi ya *ambulance* ya miguu mitatu. Mawazo yangu yalikuwa kwamba, pikipiki ya miguu mitatu katika maeneo ya vijiji, yaani unamtoa mgonjwa kumpeleka kwenye Kituo cha Afya, ingeweza ikawa ni njia mojawapo ya kusaidia sana kumkimbiza mama mjamzito aweze kupata huduma kwa haraka.

Nilitoa wito kwa wafanyabiashara wengine wajitokeze kwa wingi ili washindanishe bei na ubora ili tuone kama watu watakaojitekeza wana vifaa vizuri zaidi, tuweze kuisaidia jamii kwa kujaribu kutoa huduma hiyo kwenye vituo vyetu vya afya. Kwa hiyo, ninakubaliana kabisa tutajaribu kuliangalia tuone namna gani kutoka ngazi ya Kijiji mpaka kwenye Wizara yenyewe, kutakuwa na ufuatiliaji wa karibu katika eneo hili la vifo vya akina mama na watoto. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali hili.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye vilevile ni Mwenyekiti wa CCM, amenukuliwa akizungumzia kuhusu haja ya Chama kinachotawala kujivua gamba. Kati ya mambo aliyoyazungumza ni pamoa na kuondokana na watuhumiwa wa ujisadi.

Mheshimiwa Mkuu uliwhi kulieleza Bunge hili Tukufu kwamba; usingetaka kabisa kuzungumzia masuala ya MEREMETA kwa sababu ni siri za Jeshi. Baada ya kauli hii ya Rais na dhamira hii ya kujivua gamba kuhusiana na masuala ya ujisadi; je, uko tayari kutaja wahusika wa Kampuni ya MEREMETA na kuielekeza Serikali kuchukua hatua zinazostahili kuhusiana na tuhuma hizo? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mnyika, umepandia rafiki yangu hapa. Yaliyofanyika ndani ya Chama cha Mapinduzi ni ya Chama cha Mapinduzi na kilikuwa kinashughulikia na Wanachama wake. Jitihada za ndani katika kujaribu kujikosoa kwa sababu Chama kizuri lazima muwe na utaratibu wa kujikosoa. Kama ulimsikia vizuri Mwenyekiti wetu alisema, tutaendeleza hizo juhudhi kwa lengo la kujaribu kusaidia kujenga Chama ambacho ni imara, kinachokubalika na kinachopendwa ili tukifika mwaka 2015, tuweze kuwashinda kwa mara nyingine. Hii ndiyo ilikuwa hasa *message* yake. Sasa suala la MEREMETA ni jambo tofauti kabisa na pengine siko katika nafasi ya kuweza kulizungumzia kama unavyotaka nizungumzie, kwa sababu ni jambo lingine ambalo lina misingi tofauti sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza kabisa, ninapenda nikushukuru.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Unaanza.

**SPIKA:** Mimi ninazungumza, ninaomba ukae chini. Kwanza, ninaomba nimshukuru Waziri Mkoo, kwa namna alivyoweza kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Kama nilivyosema, maswali yetu yalikuwa ya watu 16 na muda wetu ni dakika 30, kwa hiyo, waliopata nafasi ya kuuliza maswali wamepata na wengine waendelee kuomba, ndiyo utaratibu tuliojipangia. Sasa tunaingia hatua inayofuata.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako kuhusu Nyongeza ya Sita ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu, inayohusu Mwongozo kuhusu Maswali kwa Waziri Mkoo.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo ninaouomba uko katika Nyongeza ya Sita (3)(3): “Mbunge ye yote atakayepata fursa ya kumwuliza Waziri Mkoo swali na kujibiwa, anaweza kumwuliza Waziri Mkoo swali lingine moja la ufanuzi.”

Mheshimiwa Kabwe Zitto, alipata nafasi ya kumwuliza Waziri Mkoo swali moja na likajibiwa na aliomba kuuliza swali la nyongeza umemzuia; ninaomba utueleze kama hicho kitendo cha kumzuia Mbunge kuuliza swali la nyongeza kwa Waziri Mkoo linakwenda sambamba na Kanuni za Bunge hili Tukufu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, ninapokaa ninaongoza kikao. Ninapoongoza kikao, ninasikiliza anayezungumza na wanaouliza. Amemjibu kwamba, hicho ulichosema sijakiona, nitakwenda kwa wataalam nikasome. Mheshimiwa Zitto akasema ninamsomea nikasema hapana, amesema kwamba atalijibu atakapokuwa amesoma. Ndiyo maana ya Kiti hiki, siyo kwamba unapelekwa kama vile na wewe umefungwa kitambaa hauelewi, hausikii; ndiyo hivyo inavyofanya kazi. Kwa hiyo, tunaendelea. (*Makofi*)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba kupata ufanuzi wa maswali kwa Waziri Mkoo, Siku ya Alhamisi kwa sababu mimi nilikuwa ni mtu wa nane kuiandikisha, Mheshimiwa Mnyika alikuwa karibu mtu wa 14; sasa nilikuwa ninataka kufahamu kama kuwahi kule kunakuwa hakuna maana tusiwe tunawahi au busara zako huwa zinaamua kuchagua mtu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ninafurahi umeuliza swali hilo. Nikikaa hapa, watu 16 lazima wengine wataachwa; kwa hiyo, ninapoangalia ninaangalia *gender*, ninaangalia vyama, ninaangalia maeneo, ninaangalia vijana na vitu vyote, ndiyo maana nimefanya hiyo kazi.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Leo yatajibiwa maswali matano tu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa ninaacha mwongozo, ninaongoza mimi. Tunaendelea.

Na. 90

**Kuongeza Madaktari na Wauguzi – Hospitali  
ya Wilaya Mpanda**

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLACK** aliuliza:-

Kutokana na kuundwa kwa Mikoa na Wilaya Mpya mwaka 2010, Hospitali ya Wilaya ya Mpanda kwa kipindi kifupi kijacho itakuwa ni Hospitali ya Mko na kwa sasa Hospitali hiyo inakabiliwa na upungufu mkubwa wa Madaktari na Wauguzi ikilinganishwa na wanaofika kwenye Hospitali hiyo kupata huduma za matibabu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza watumishi husika kwenye hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA  
SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Marystella Mallack, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, baada ya kuanzishwa kwa Mko mpya wa Katavi, Hospitali ya Wilaya ya Mpanda inaweza kupandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Mko. Aidha, kwa sababu hiyo, itahitaji kuwa na Madaktari Bingwa saba, Madaktari wa Kawaida saba, Madaktari Wasaidizi 14, jumla wanakuwa Madaktari 22 pamoja na Daktari wa Mko (*RMO*). Wauguzi wanategemeana na ukubwa wa hospitali; kwa mfano, hospitali inatakiwa kuwa na vitanda 300 hadi 450 na Afisa Muuguzi mmoja anahudumia vitanda kumi.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu zilizopo, Hospitali ya Wilaya ya Mpanda, inatakiwa kuwa na watumishi 184, watumishi waliopo kwa sasa hivi ni 126. Hivyo, watumishi wanaohitajika ni 58 katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Halmashauri ya Mpanda imeidhinisha katika bajeti yake nafasi za ajira mpya 58 kwa kada mbalimbali wakiwemo Madaktari watatu, wauguzi 27 na watumishi wa kada zingine 28.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha Vituo vya Afya vya Kinyonga, Kalema na Mamba, ambavyo vimepatiwa vifaa vya upasuaji wakati juhudzi za kupata Hospitali ya Mko wa Katavi zinaendelea. Juhudi zinafanyika kuvipatia umeme ili vianze kutoa huduma hiyo.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninapenda kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wahudumu wa afya vijijini wamekuwa wakikwepa kufanya kazi katika zahanati vijijini kutokana na mazingira magumu yanayowakuta kama vile ukosefu wa nyumba bora za kuishi, mshahara mdogo usiokidhi mahitaji, miundombinu mibovu kama vile barabara na mawasiliano. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma hizo kwa wahudumu hao ili waweze kukubali kuishi vijijini na kuipenda kazi yao pamoja na kutoa huduma bora kwa Wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anna Mallac, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama ukiwa na barabara nzuri, ukiwa na nyumba nzuri za watumishi, ukiwa na miundombinu mizuri, maana yake utakuwa unavuta watumishi zaidi kwenda katika maeneo hayo; hilo hata halina ubishi kabisa. Wale ambao wanakwenda katika Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Katavi, watakuwa wameona jitihada kubwa sana zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha kwamba, barabara nzuri zinapatikana na mambo mengine mengi ambayo ameyataja hapa. Si hivyo tu, Mkoa wa Rukwa sasa hivi tunavyoeleza, Daktari akienda katika Mkoa wa Rukwa au Katavi, anapewa shilingi milioni moja kama motisha. Watumishi wa kawaida wakienda pale, wanapewa kati ya shilingi laki tano mpaka laki saba, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, wanawavutia watumishi ili waende katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue takwimu hizi kama kielelezo cha wazi kabisa kinachoonesha dhamira ya Serikali na Wananchi na Jamii kwa ujumla ya kuona kwamba, wanawavutia watumishi ili waende katika Mikoa ya Rukwa. Nami ninachukua nafasi hii kwa niaba ya Serikali, kuwaomba watumishi wote ambao wanakuwepo katika Mikoa ya pembezoni, wawaonee huruma pia Wananchi walioko katika maeneo yale, kwa maana ya kuweza kuwapatia huduma hizo muhimu na tutazingatia haya maelekezo ninayoyatoa na sisi tutafanya jitihada kuhakikisha nyumba zinapatikana na miundombinu mingine inapatikana katika Mkoa huu wa Rukwa na Katavi.

Na. 91

### **Zahanati Katika Jimbo la Vunjo**

**MHE. AUGUSTINO L. MREMA** aliuliza:-

Serikali ina lengo la kuboresha afya za Wananchi wa Jimbo la Vunjo, kutokana na ukweli huo:-

- (a) Je, kuna zahanati ngapi kwa kila Kata za Vunjo zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa?

- (b) Je, mtandao huo wa ujenzi wa zahanati umeigharimu Serikali fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kupitia Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM), Serikali inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Afya kila Kata na Zahanati kila Kata nchini. Jimbo la Vunjo lina jumla ya Zahanati thelathini na mbili zikiwemo 16 za Serikali, mbili za binafsi na 14 za Mashirika ya Dini. Zahanati mbili za Matala na Kochakindo zinaendelea kujengwa. Mchanganuo wa zahanati hizo Kikata ni kama ifuatavyo:-

Zahanati kwa kila kata katika Jimbo la Vunjo: Kata ya Kilema Kaskazini ina Zahanati (1), Kata ya Kilema Kusini (2), Kata ya Kilema Kati (1), Kata ya Kirua Vunjo Mashariki (2), Kata ya Kirua Vunjo Magharibi (2), Kata ya Kirua Vunjo Kusini (6), Kata ya Kahe (2), Kata ya Kahe Kaskazini (2), Kata ya Mwika Kaskazini (2), Kata ya Mamba Kaskazini (2), Kata ya Mamba Kusini (2), Kata ya Marangu Mashariki (1), Kata ya Marangu Magharibi (3) na Kata ya Makuyuni ina Zahanati (4).

(b) Mheshimiwa Spika, mtandao wa ujenzi wa Zahanati katika Kata za Vunjo, ambalo ndilo Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, umeigharimu Serikali kiasi cha shilingi 508,166,289.88.

**MHE. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ninampongeza Naibu Waziri, kwa majibu mazuri na kwa kutoa karibu shilingi milioni 508 kwa ajili ya ujenzi wa hizi zahanati.

(a) Inavyoonekana kuna Zahanati 32; 14 za Mashirika ya Dini na mbili za Watu Binafsi. Ninakumbuka Januari katika jibu la swali langu la msingi alisema, lengo la Serikali ni kutoa huduma za afya bure kwa akina mama, watoto na wazee. Sasa naomba nimwulize katika Zahanati hizi 14 za Dini na hizi mbili za Watu Binafsi; kuna Mkataba gani kati ya Serikali na wale watu; Mashirika ya Dini na Watu Binafsi ili akina mama pamoja na wazee na watoto wanaotaka kutibiwa pale waweze kutibiwa bure kama ilivyo Sera ya Serikali?

(b) Kwa kuwa huduma ambayo inakosekana kule Kahe, Kata ya Kahe ni *ambulance* kwa ajili ya akina mama wajawazito. Je, anaweza kuniahidi kwamba zile *ambulance* za miguu mitatu ambazo anazigawa nchi nzima na mimi nitapata angalau mbili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, hili analolizungumza la hospitali ni Hospitali ya Kilema ambayo iko chini ya *RC* na Hospitali ya Kibosho na zipo nyingine za KKKT, ambazo ziko katika ngazi ya Zahanati; hizi ziko katika Halmashauri anayoizungumzia hapa. Vilevile ameuliza kwamba, tumeweka utaratibu gani ambao unawawezesha; hizi tunazitumia kama *Designated Hospitals*, yaani ni kama Hospitali Teule.

Hiyo huduma ya bure tunayoizungumza hapa ya kwanza kabisa ni akina mama wanapokwenda kujifungua pale hata kama wangekwsenda kwenye hospitali ninazosema hizi, tutamwangalia kama tunavyomwangalia katika hospitali ya kawaida kabisa. Akina mama wanapokwenda pale hawapaswi kutozwa nyembe, *gloves*, pamba na vitu vingine; wanatakiwa wapate huduma hizo *free of charge*. Wakienda na watoto wao wenye umri wa miaka mitano kurudi chini hawaguswi. Wakienda pale wakiwa wanaumbuliwa na Kifua Kikuu, UKIMWI na Saratani, hao wote hawatozwi kitu chochote. Wazee ambao wana miaka 60 na kuendelea nao hawatozwi kitu chochote.

Tatizo ambalo tumelipata kwa upande wa wazee ni kwamba, unamkuta mzee amechakaa labda kwa sababu ya maji tu na nini, lakini tumeepata tatizo la kupambanua. Hata hivyo, tunafikiria kutakuwa kuna haja ya kuwa na vitambulisho kwa ajili ya hao wazee ambao wameainishwa kwamba, wapate hizo huduma bure kama anavyosema Mheshimiwa Lyatonga Mrema. Kwa hiyo, anachosema hapa ni kwamba, zile hospitali ambazo tunazihudumia kuititia kwenye utaratibu huu wa kushirikiana kati ya Mashirika ya Dini na Serikali, mama huyu anahudumiwa kama vile anavyokwenda kwenye hospitali ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, hili la Kahe analolizungumza hapa, ni kweli pale Kahe kuna tatizo; nikisimama hapa nikasema hakuna tatizo pale; tulichofanya kuititia Mkoo ni kwamba, tumeingiza katika bajeti, huu utaratibu ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu ameuzungumzia wa bajaji siyo *ambulance* kama ulivyosema hapa. Kwa kuwa ninamjua Mheshimiwa Mrema, nikitoka hapa atanikaba ataniambia lete *ambulance*; *ambulance* bado, lakini bajaji hizo nimezungumza mimi na Mkoo na wamesema kwamba, wameingiza katika bajeti ili kuhakikisha kwamba, zinasaidia hapo Kahe katika kipindi cha mpito, lakini baadaye *ambulance* ziweze kutafutwa kwa utaratibu wa kawaida ambao tumeuzungumzia hapa.

Na. 92

**Wafanyabiashara na Wavuvi wa Tanzania  
kusumbuliwa Kenya**

**MHE. HAJI KHATIB KAI** aliuliza:-

Tanzania, Kenya na Uganda ni nchi zilizo katika Shirikisho la Afrika Mashariki na nchi hizo hushirikiana katika mambo mengi ya kiuchumi ikiwemo biashara lakini wafanyabiashara na wavuvi wanaoingia au wanaotumia Bandari ya Shimoni Kenya hulazimika kubakia ndani ya vyombo muda mrefu kwa kisingizio cha kutokuwepo Maafisa Uhamiaji na Wavuvi wanaoingia Kenya wanaonewa hata kwa kuwapiga pamoja na kuwanyang'anya haki zao mwaka 2007:-

(a) Je, kwa nini Wafanyabiashara na Wavuvi hao wa Tanzania wanapata usumbufu kama huo wanapoingia nchini Kenya kwa shughuli zao?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya hali hiyo ili kusitokee tena usumbufu usio wa lazima?

#### **NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ninaomba kujibu la swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna idadi kubwa ya Watanzania hususan kutoka Kaskazini mwa Kisiwa cha Pemba, wanaofanya shughuli zao katika maeneo ya Mombasa nchini Kenya. Miongoni mwao wapo wanaofanya biashara ndogondogo za kusafirisha bidhaa za matumizi ya kawaida, ambapo sehemu kubwa ya wafanyabiashara hawa hupitia eneo la Shimoni.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanaoingia Kenya kama Wavuvi ni wale wanaoweka kambi (dago), kwa msimu ambao kwa kawaida hufikia katika Vijiji vya Kipini, Mayungu, Ngomeni, Takaungu, Mtwapa, Kongowe, Vanga, Majoreni na Gasi. Kwa kawaida, Wavuvi hawa wanafanya shughuli zao bila kusumbuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwambao wa Mashariki wa Kenya, boti haziruhusiwi kuegesha (kufunga gati), nyakati za usiku. Boti zinazofika katika maeneo hayo usiku, hulazimika kusubiri hadi asubuhi kwa ajili ya ukaguzi na kuruhusiwa kushusha abiria na mizigo. Mara nyingine usumbufu hutokana na wahusika kutokuwa na hati sahihi za kusafiria wanapoingia nchini Kenya na itafaa Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wizara yetu na wahusika wengine, wasaidie kuwaelimisha Wananchi wanaoingia nchini Kenya, kuhakikisha kwamba, wanazo hati sahihi za kusafiria na kwamba vyombo vyao vifike bandarini asubuhi, badala ya kufika usiku na kulazimika kusubiri kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vitendo vya mwaka 2007, Wizara inamwomba Mheshimiwa Mbunge, awasilishe vielezo kamili ili suala hili liweze kuwasilishwa katika ngazi ya Jumuiya kwa ajili ya kupata ufumbuzi muafaka.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri alisema, usumbufu wanaoupata ni kutokana na wahusika

kutokuwa na hati sahihi. Mimi hili ninalikataa na ninasema kwa kulijua, wasafiri wote huwa wako na hati zao sahihi ila kinachoendelea ni uonevu, unyanyasaji na udhalilishaji:-

- (a) Je, Waziri atashirikiana na mimi kuona ni vipi uonevu huu hauendelei?
- (b) Nchi yetu ya Tanzania inasifika sana kwa ukarimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na hii ni kutokana na mapokezi mazuri ya raia wanaotoka katika Jumuiya za nchi hii. Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika wa Watanzania hasa wale wanaotoka Kisiwa cha Pemba kwa sababu ndiyo walio karibu zaidi na Kenya na wao wajihisi wako nyumbani?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**  
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, jibu la ziada la Mheshimiwa Mbunge ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kabisa uhusiano baina ya Tanzania hasa Kaskazini Pemba na Mombasa, ulianza tangu enzi za ujima, Ukoloni wa Sultani na mpaka hivi sasa. Kwa hiyo, katika jibu langu mama nilielezea kwamba, Wizara ishirikiane naye ili kuwaelimisha Wananchi.

Mheshimiwa Spika, inafaa nieleze hapa kwamba, katika Muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na katika Kanuni za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Ibara ya 5(1) na (2)(a) na (b) zinasema kwamba, mtu ye yote ambaye anatakiwa aingie katika nchi jirani, anatakiwa lazima awe na hati za kusafiria na zilizo *valid*. Sasa Mheshimiwa Waziri alipotuletea suala hili, tulilichukua kwa undani zaidi na kusema kwa nini tusubiri taratibu za Jumuiya ziwe zinafanya kazi. Kwa hiyo, kwa busara ya Wizara, tuliwasiliana na Ubalozi wetu kule Mombasa na hili ndiyo jibu ambalo wametupatia kwamba, wasafiri wanaotoka kule huwa wengi wao wanaingia katika boti za abiria na boti hizo huwa zinawachukua wao isivyo halali na wakifika kule, Askari wa Uhambaji na wa Forodha huwa wanawadadisi vibaya sana juu ya kutokuwa na hati. Hili ndiyo jibu ambalo ninaweza kulitoa.

## KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni mazuri, lakini nilikuwa ninamsihi Mheshimiwa Kai, azingatie Kanuni ya 61 ambayo inatutaka sisi sote tunapozungumzia jambo humu ambalo tuna maslahi nalo, basi tuseme hivyo ili tusije kupata adhabu bure. Taarifa zilizoko Serikalini ni kwamba, Mheshimiwa Kai ana boti kadhaa ambazo zinafanya biashara hiyo. (*Makofii/Kicheko*)

Nilitegemea na hajachelewa, hata hivi sasa anaweza kukiri hilo ili adhabu inayotakiwa kupelekwa kule kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kwa muujibu wa 61(3), isije ikamchukia. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kai, hebu jaribu ku-*declare* tu, mimi sitakupeleka huko kabla.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, suala alilosema Waziri wa Afrika Mashariki ni kweli, nina boti hizo. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Basi, kwa kosa la kwanza Spika hakupeleki huko. (*Kicheko*)

Na. 93

### **Madaktari wa Magonjwa ya Wanawake Kufanya Ziara**

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE** aliuliza:-

Wanawake wengi wanapatwa na magonjwa mengi hasa yanayohusiana na uzazi kama vile matezi kwenye matumbo ya uzazi, ugumba na kadhalika:-

Je, kwa nini kundi la Madaktari Bingwa wa mambo ya wanawake wasiwe wanafanya ziara kuwatemeblea wanawake sehemu mbalimbali kwenye nchi yetu kama wanavyofanya MEWATA ili kusaidia Wanawake wengi zaidi Mikoani?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mchungaji Dokta Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kusogeza huduma za kibingwa karibu na Wananchi wakiwemo Wanawake, Serikali imezipandisha madaraja Hospitali zote za Mikoa, Hospitali tatu za Manispaa za Dar es Salaam na Hospitali tisa za Mashirika ya Kujitolea, ambazo nyingi zipo sehemu za vijijini kwa kuzifanya kuwa Hospitali za Rufaa.

Hospitali hizi zitawezeshwa kwa kuwa na Wataalam Mabingwa wa fani mbalimbali, ikiwa ni pamoja na fani ya Magonjwa ya Wanawake na vifaa tiba vya kisasa vya kutosha. Wataalam hawa watakuwa na utaratibu wa kutembelea vituo vingine vya kutolea huduma katika maeneo yao, kwa madhumuni ya kutoa msaada endelevu na wa kitaalam zaidi kwa Wananchi, wakiwemo Wanawake pale unapohitajika. Katika kipindi cha 2008/2009 - 2010/2011, jumla ya Madaktari Bingwa 126 wamepangiwa kufanya kazi katika Hospitali za Mikoa. Aidha, jumla ya madaktari 522 wanaendelea na masomo ya

ubingwa katika fani mbalimbali za afya. Baada ya kuhitimu, tutaendelea kuwapangia sehemu mbalimbali kulingana na mahitaji.

Kupitia Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), Serikali inakusudia kuziwesha Hospitali zote za Wilaya hapa nchini kuwa na Madaktari Bingwa.

Mheshimiwa Spika, hatua hii pamoja na ile niliyoitaja hapo awali, kwa pamoja zitasaidia sana kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya za kibingwa kwa Wananchi wakiwemo Wanawake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua nilizoiainisha hapo juu, Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi na vyama mbalimbali vya wataalam wa afya kama vile Chama cha Madaktari Wanawake (MEWATA) na Chama cha Madaktari wa Magonjwa ya Wanawake (*Association of Gynaecologists and Obstetricians of Tanzania - AGOTA*) ili kuhakikisha kuwa, vinaendelea kutoa huduma zinazostahili kwa Wananchi wakiwemo Wanawake.

Mheshimiwa Spika, Hospitali za Mashirika ya Dini ambazo zimepandishwa hadhi kuwa Hospitali za Rufaa ni kama ifuatavyo: Hospitali ya Peramiho - Songea, Hospitali ya Mtakatifu Gasper - Itigi, Hospitali ya *Ndanda Mission* - Mtwara, *Arusha Lutheran Medical Centre* - Arusha, *Nyangao Hospital* – Mtwara, Hospitali ya Mtakatifu Francis - Ifakara, Ilembula Mission Hospital - Njombe, Kabanga Hospital - Kigoma na Hospitali ya Hyrom - Mbulu.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri sana ya Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Ugumba ni tatizo la kifamilia kati ya mume na mke lakini lawama zote hutupiwa mwanamke peke yake. Vilevile husababisha manyanyaso katika ndoa na hata kuvunjika ndoa na hata mwanamume kuoa mwanamke mwagine au kupata nyumba ndogo ili apate kuzaa wakati tatizo pengine ni la mwanamume. Ningependa kumwuliza Waziri kwamba ugumba wa wanaume unajuliakanaje; unagundulikaje na unatibikaje ili wote tuweze kushughulikiwa kikamilifu? (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Endelea, muda unakwisha.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Swali la pili.

(ii) Ningependa kutoa shukrani kwa ajili ya kupandishwa kwa *St. Francis Hospital* pale Ifakara kuwa Hospitali ya Rufaa; lakini ningependa niulize swali moja. Kwa kuwa Wananchi wa Mlimba, Kibaoni na Kidatu wanategemea hospitali moja tu; na kwa kuwa Wanawake wanaoshindwa kujifungua au wanaosumbuliwa na matatizo wakati wa kujifungua inabidi watoke Mlimba, Masagati au Uchindile ambako ni kilomita 200

kufika Ifakara na barabara ni mbaya; je, Wizara inaweza kuvipandisha vituo hivi vya afya viwili ambavyo ni Mlimba na Kibaoni, viwe vituo vya afya? (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, suala la ugumba, kubainika kwake kwa mwanamme inabidi sharti wakapimwe hospitali. Kwa sababu kigezo cha rahisi sana tunachokichukulia kwa mwanamke kuwa mgumba ni kutokupata mimba na kuzaa. Kwa wanaume vigezo hivyo vinakuwa vigumu kwa sababu lile tendo la kupata mimba nalo anachangia. Sasa unaweza ukachangia kwa mbegu, lakini zile mbegu zinaweza nazo zisiweze kusababisha mimba. Sasa basi kuweza kusaidia, baba huyu naye anatakiwa aende hospitali, pale kuna mbinu za kibaiolojia, tutaweza kugundua kama, mbegu zake hizo zinaweza kusababisha mimba.

Vilevile ninaomba nichangie au nitoe maelekezo kwamba, akina baba nao wakati mwininge kwa sababu ya staili za maisha, nazo zinasababisha wasiweze kuwajibika sawasawa na kusababisha mimba labda. Aina ya vyakula tunavyokula kama nilivyoeleza jana, ambavyo vinaweza vikasababisha matatizo ya figo na matatizo ya moyo, nazo zinachangia huyu baba kutokuwezesha kutunga mimba. Vilevile matatizo mengine ni ya maambukizo ya magonjwa, kama unapata magonjwa ya ngono mara kwa mara, unaelekea kutokusababisha mimba katika ndoa. Zaidi ya hapo, tunajitahidi kwa kiasi kikubwa, Serikali kupitia Wizara ya Afya, tunatoa maelekezo ya kitaalam; namna gani kuhusu uzazi na mpango wa uzazi. Kwa hiyo, ninawasihi tena akina baba wapate fursa vilevile ya kwenda kuhudhuria kliniki; kule kuna elimu ya kutosha, inaweza ikakusaidia kuhusu suala la uzazi.

Mheshimiwa Rwakatare, ametoa ombi la kuwezesha Vituo vya Mlimba na Kituo cha Afya cha Ifakara Mjini ili viwezesheve navyo kutoa huduma kama Hospitali za Wilaya ambazo tumeeleza nazo siku za usoni tunazipanga zitoe huduma au ziwekwe na Daktari Bingwa pamoja na daktari anayeshughulikia magonjwa ya akina mama.

Hili ni suala la Halmashauri, ninamshauri Mheshimiwa Rwakatare, aende kwenye Halmashauri yake husika, wapange katika vituo hivi viwili kipi wanapendekeza iwe Hospitali ya Wilaya.

Hospitali ya Mtakatifu Francis pale Ifakara, ambayo imepandishwa hadhi, itaendelea kutoa huduma kama Hospitali ya Wilaya pamoja na kuwahudumia hawa akina mama. Ninakubaliana naye kwamba, kwa mazingira ya kijiografia, Hospitali ya Mlimba au Kituo cha Afya Mlimba, kipo mbali sana na Wananchi wanaokaa kule; kwa kweli wanateseka kupata zile Hospitali za Wilaya. Kwa hiyo na mimi ninakubaliana naye kwamba, maombi yatakapoletwa kupitia Halmashauri yake, yanapelekwa Wizarani, sisi tutakipandisha kile Kituo cha Afya Mlimba kuwa Hospitali Teule ya Wilaya au kama wao wameamua kwamba, wanaipanga kuwa Hospitali ya Wilaya basi moja kwa moja tunaipasisha na itaendelea kutoa huduma hizo za Wilaya.

**SPIKA:** Ninamruhusu Waziri aseme hayo maneno makubwa ya mwanzo. Ametumia muda mwinci sana, kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Faith Mitambo, atauliza swali hilo.

### **Ujenzi wa Barabara ya Liwale hadi Utet e**

**MHE. FAITH M. MITAMBO** aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga Barabara ya Liwale hadi Utete kupitia Mbuga ya Hifadhi ya Selous; barabara hiyo ni fupi kwa kuelekea Dar es Salaam hivyo itapunguza gharama za usafiri kati ya Liwale na Dar es Salaam na pia kuboresha Sekta ya Utalii wa ndani ya Hifadhi ya Selous:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo?

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swal la Mheshimiwa Faith Mitambo, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali iliahidi kutengeneza Barabara ya Liwale – Kingupira – Utete na ni kweli pia kwamba, Barabara hii ikitengenezwa, itapunguza gharama za usafiri kati ya Liwale na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Barabara hii itapitia katika Hifadhi za Taifa, mchakato wake wa ujenzi ni mrefu, unaohitaji muafaka kwanza na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuangalia namna bora ya kutekeleza ahadi hii ya Serikali na wakati huo huo tukizingatia masuala ya mazingira. Serikali bado ipo kwenye hatua ya awali ya kutafuta muafaka.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kumwuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Barabara ya Liwale – Ilonga – Mahenge ni kiunganishi kati ya Mikoa ya Lindi na Morogoro. Je, ni lini Serikali itaifufua Barabara hii ili Wananchi wa Lindi na Mtwara waweze kuitumia kama *shortcut* ya kwenda Mahenge hadi Mikumi na kuiunganisha mikoa mingine kwenda Dodoma – Iringa na Mbeya?

(ii) Je, Serikali ina mikakati ipi ya kuhakikisha kwamba Barabara ya Nangurukulu – Liwale inaimarishwa ili iweze kupidika kipindi chote cha kiangazi na masika kwa sababu Barabara hiyo kwa sasa ina uwezo wa kupidika kipindi cha kiangazi tu? Ahsante Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nangulukuru hadi Liwale, yenye jumla ya kilomita 231,

Serikali imekuwa ikijitahidi kuitengeneza na inahudumiwa na Wizara kupitia Meneja wa TANROAD. Katika kipindi cha karibu miaka mitatu kuanzia mwaka 2008/2009, zaidi ya shilingi bilioni mbili zimetumika katika kutengeneza maeneo korofii kama vile ya Miguruwe, Kikwegea, Njinjo na kadhalika. Kwa hiyo, ninapenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kuihudumia hii barabara yenyewe jumla ya kilomita 231 ili iweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka.

Kuhusu barabara zingine ambazo amezitaja ambazo ni fupi zaidi kufika Morogoro na kuunganisha na Morogoro na Mikoa mingine; Tanzania nzima ina jumla ya kilomita 86,000; kwa hiyo, tutakuwa tunaziangalia barabara kulingana na hali halisi ya bajeti yetu na kila barabara itakuwa inahudumiwa kulingana na watusika wanaohusika. Zile barabara ambazo ziko chini ya Halmashauri ya Wilaya, zitaendelea kuhudumiwa kwa kutumia fedha za *Road Fund*, lakini Barabara za Mikoa na za Taifa nazo zitaendelea kuhudumiwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. ANTHONY G. MBASSA:** Ninakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuniona. Ninaomba nimwulize jirani yangu Mheshimiwa Magufuli, swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa matatizo yaliyoko kwenye swali la msingi ni sawa sawa na tatizo lililoko katika Jimbo la Biharamulo Magharibi.

Je, ni lini Barabara ya Bwanga mpaka Karelebezo itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Hivi barabara zenu; basi kwa sababu Waziri anazijua, lakini ni swali jipya.

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, Barabara aliyoitaja ya kutoka Biharamlo - Karelebezo hadi Uyovu iko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM, ukurasa wa 76 na ina urefu wa kilomita 112. Barabara hii imeshafanyiwa *design*. Kwa hiyo, fedha zitakopatikana, itatengenezwa kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ninakushukuru, nilijua tu unaweza hivi. Tunaendelea na swali linalofuata; Mheshimiwa David Kafulila, atauliza kwa niaba ya Mheshimiwa Moses Machali.

Na. 95

### **Ujenzi wa Daraja la Malagarasi**

**MHE. MOSES J. MACHALI (K.N.Y. MHE. DAVID Z. KAFULILA)** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitoa ahadi mara kadhaa za kujenga Daraja la Mto Malagarasi ambalo ni la msaada mkubwa kwa kuunganisha Mkoa wa Kigoma na Tabora:-

Je, Serikali inaweza kuwahakikishia Wananchi wa Wilaya mpya ya Uvinza na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla ni lini ujenzi huo utachukua muda gani kukamilika?

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swal la Mheshimiwa David Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Ujenzi wa Daraja la Mto Malagarasi ulisainiwa tarehe 21 Oktoba, 2010 kati ya Wakala wa Barabara (*TANROADS*), kwa niaba ya Serikali ya Tanzania na Mkandarasi *M/S Hanil Engineering & Construction Co. Ltd*, kutoka Korea.

Aina ya Mkataba ni wa Sanifu na Jenga (*Design and Build Contract*). Mkataba unahuishisha usanifu wa km 48, ujenzi wa daraja pamoja na ujenzi wa km 11 za barabara kwa kiwango cha lami, kwa gharama ya Dola za Kimarekani 28.783 ambazo ni karibu bilioni 43.

Mheshimiwa Spika, Mhandisi Mshauri ni *M/S Cheil Engineering Co. Ltd* kutoka Korea. Gharama za Mkataba wake ni Dola za Kimarekani 882,000.

Mkandarasi alikabidhiwa eneo la Mradi tarehe 10 Desemba, 2010. Hivi sasa Mkandarasi anaendelea na kazi ya maandalizi (*mobilization*) na ujenzi wa kambi. Ujenzi utachukua muda wa miezi 36 na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wote kwa ujumla kwamba, Serikali inafuatilia ahadi na mipango yote kwa makini kabisa na Daraja la Malagarasi na Barabara nyinginezo zilizo katika Mpango wa Serikali, zitatekelezwa hatua kwa hatua.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa ili niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri, maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Kafulila.

**SPIKA:** Hayo ni ya kwako siyo ya Mheshimiwa Kafulila.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Spika.

- (i) Kilomita 48 za lami zitaanza kujengwa lini mpaka ziweze kukamilika?
- (ii) Kwa mujibu wa Taarifa ya Bajeti ya iliyokuwa Wizara ya Miundombinu kwa Bunge la Tisa, Barabara ya Kidawe - Kasulu iliyoko Mkoani Kigoma, takriban kilomita 50, ilitengewa shilingi bilioni sita ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, Waziri anatamka kwamba Barabara ile itaanza kujengwa lini kwa kiwango cha lami kwa sababu mpaka dakika hii hakuna kinachoendelea?

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Daraja la Malagarasi pamoja na kilomita 48, limegawanywa katika *lot* mbili; *lot* ya kwanza itahusisha ujenzi wa kilomita 11 pamoja na kutengeneza madaraja matatu, ambapo daraja moja kubwa ni la urefu wa mita 200, lingine la pili lina mita 50, linalofuata lina mita 25 na daraja hili litakuwa na urefu wa kilomita 2.75 na litakuwa na upana, yaani *two line*, lakini pia litakuwa na barabara ya waenda kwa miguu kama lilivyo Daraja la Mkapa au Daraja la Umoja. Hiyo ndiyo itahusisha *lot* ya kwanza.

*Lot* ya pili itahusisha ujenzi wa kilomita 37 na ndiyo maana ujenzi wa daraja lote pamoja na barabara, tunafanya kwa *design and construct*. Fedha zilizopo ni za *lot* namba moja. *Lot* ya pili tunaendelea kutafuta, inawezekana katika bajeti inayokuja fedha hizo nazo zitaweza kupatikana kwa ajili ya kuendelea katika *lot* ya pili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Barabara ya Kidawe – Kasulu ameeleza hapa Mheshimiwa Machali kwamba, ilipangiwa shilingi bilioni sita kwa ajili ya kuanza kujengwa na ina urefu wa kilomita 50. Yale yote yaliyopitishwa katika Bunge hili, yataendelea kutekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

Kwa hiyo, tuendelee kusubiri fedha zitakapopatikana tutaendelea kushughulikia na hiyo Barabara ya kutoka Kidawe hadi Kasulu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo tunamaliza; wewe umejibiwa tena mwongozo halafu inakuwaje?

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa za Bajeti ya Mwaka 2010/2011, kiasi cha shilingi bilioni sita ni fedha za ndani ambazo zimetengwa, lakini hakuna kazi ambayo inaendelea katika Barabara ya Kidawe – Kasulu.

Majibu ya Mheshimiwa Waziri yanaonesha pesa zitakavyoweza kupatikana, lakini kwenye Bajeti inaonesha pesa zilizotengwa. Sasa barabara ile itaanza kujengwa lini; majibu ya Mheshimiwa Waziri bado hayajaweza kukidhi viwango.

**SPIKA:** Pesa zinaweza kuonekana kwenye bajeti lakini zisipatikane, ndivyo alivyokujibu. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Mheshimiwa Kayombo atauliza swali hilo.

## **Ahadi ya Wakulima Katika Vyama vya Ushirika**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais katika Ziara za Kampeni za Uchaguzi Mkuu 2010 Mbinga Mjini aliahidi kulipa Fedha za Wakulima waliokuwa Wanachama wa MBICU:-

(a) Je, ni lini sasa Wakulima hao watalipwa?

(b) Hali kadhalika, Waziri wa Kilimo alipokuwa akizungumza na Baraza la Madiwani la Mbinga aliahidi kuwa atahakikisha Ushirika wa MBIFACU unafanya kazi. Je, Serikali imetekeleza namna gani ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza ahadi alizotoa Mheshimiwa Rais katika Kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010, ikiwa ni pamoja na kuwalipa waliokuwa Wanachama wa Vyama vya Ushirika. Aidha, ziko changamoto zinazojitokeza; kwa mfano, baada ya kuwalipa Wakulima waliouza kahawa yao mwaka 2001/2002 kuititia Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima Mbinga (*MBIFACU*), walijitokeza Wakulima wengine waliokuwa wanakidai Chama Mfu cha *Mbinga Cooperatives Union Ltd (MBICU)*, ambacho kilikuwa chini ya mfilisi kuanzia mwaka wa 1999.

Mheshimiwa Spika, wakulima waliokuwa wanavidai Vyama vya Ushirika nchini kote walihakikiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwaka 2005. Wakulima waliostahili kulipwa walitambuliwa na kuwasilishwa Serikalini kwa malipo.

Hata hivyo, mchakato huo haukuhusisha madai na madeni yaliyokuwa chini ya utaratibu wa ufilisi wa Vyama vya Ushirika kama *MBICU*. Wakulima wanaoidai *MBICU* wanashauriwa wawasilishe uthibitisho wa madai yao kwa mfilisi wa *MBICU* kwa kuwa Vyama vya Ushirika vilivyo chini ya ufislisi wadai wake watalipwa kwa utaratibu wa ufilisi.

Mheshimiwa Spika, hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa kwa lengo la kukifufua Chama cha Ushirika cha *MBIFACU* ni pamoja na zifuatazo:-

(1) Afisa Muandamizi wa Ushirika amepelekwa Wilayani Mbinga, kusaidia kuiandaa *MBIFACU* kutekeleza majukumu yake.

(2) Kusaidia Vyama vya Msingi kuandaa mipango ya biashara na mahitaji ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kahawa yao.

(3) Kuwajengea uwezo Maafisa Ushirika, Madiwani na Watendaji wa Vyama Vya Ushirika ili waweze kusimamia biashara ya Kahawa chini ya mfumo wa stakabadhi ghalani.

(4) Kujadiliana na Benki za *CRDB* na *NMB* ili ziweze kukopesha Vyama vya Ushirika Wilayani humo.

(5) Kukiwezesha kiwanda cha kukoboa kahawa cha Mbinga, kiendelee kukoboa kahawa.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais anaahidi kuwalipa wakulima, alikuwa anajua kwamba kile chama kipo chini ya mfilisi. Tulinweleza kwamba Serikali siku zote inasema watalipwa kutokana na Sheria ya Mfilisi ambayo inataka kuuzwa kwa mali zote za ushirika na bado Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba wakulima hawa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, nadhani haunitendei haki. Endelea Mheshimiwa Kayombo.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Vyama vilivyokuwa na madeni vilikuwa vingi, lakini ni viwili tu, hiki cha Mbinga na kile cha Musoma ndivyo ambavyo viliwekwa chini ya mfilisi. Uamuzi wa kuweka Vyama hivi chini ya mfilisi ulikuwa ni wa Serikali na mfilisi huyu ni Serikali yenye. Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga tayari imeshapeleka taarifa hizi katika Wizara ya Kilimo, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu. Je, ni kwa nini sasa Serikali hiyo hiyo inawabagua wananchi wa Mbinga, kwa kuwaambia wauze mali zao kupitia Sheria ya Mfilisi na wakati wanaushirika wengine kama *KNCU* na *KCU* Serikali imechukua madeni yao?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa Mbinga alilipa chama kimojawapo ambacho kipo chini ya *MBICU* Sh. 4,000,000/=, na kwa kuwa pia zipo taarifa ambazo zinaonesha wakulima wengine ambao walikuwa chini ya mfilisi wamelipwa, Serikali sasa ipo tayari kuwalipa wakulima wa Mbinga?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Serikali nia yake ni kuendelea kulipa madeni yote ya ushirika ya huko nyuma. Lakini changamoto zilizopo ni kwamba baadhi ya vyama na hasa baadhi ya wakulima, hawafuati taratibu. Kwa mfano, hawa wakulima ambao wanakidai chama cha *MBICU* wamejitokeza baada ya kuona wakulima wengine wanadai. Sasa inakuwa ni vigumu kwa Serikali kuanza kuibua tena madeni wakati hawa wakulima wameibuka nyuma.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo tunachokifanya hivi sasa ni kwamba tunaendelea kuyahakiki madeni haya. Maana sio rahisi wakiona wakulima wenzao

wamelipwa na wao wakaibuka wakaja wakasema na sisi tunadai, Serikali ikaingia moja kwa moja tu ikaanza kulipa. Kwa hiyo, tunachokifanya sasa ni kuhakikisha kwamba madeni haya yahakikiwe na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu, ambao ndio utaratibu na tukishapata uhakika huo, hawa wakulima wanaoidai *MBICU* nao watalipwa.

Mheshimiwa Spika, lakini ninataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Kayombo, kwamba kweli mfilisi ni Serikali. Lakini mfilisi huyu ni yule Afisa Ushirika wa Mkoa na kwa Mkoa ule, mfilisi wa sasa ni ndugu Watson Nganiwa, ambaye ameteuliwa baada ya mfilisi wa kwanza kufariki. Mfilisi anapoteuliwa anapewa hadidu za rejea. Sasa kazi hii inaendelea na ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Kayombo kwamba wakulima wale wanaoidai *MBIFACU* na wao taratibu hizi zitakapokwisha wataweza kulipwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni lazima tukumbuke kwamba zipo rufaa ambazo zimepelekwa Mahakani. Ukishapeleka jambo Mahakamani ni lazima pia taratibu zifuatwe, kwamba rufaa zile za Mahakama zipite ndipo uamuzi mwингine uendelee. Lakini kwa ujumla wake ni kwamba wakulima wote watalipwa na ninamhakikishia Mheshimiwa Kayombo kwa jinsi anavyolifutilia jambo hili, hawa wakulima watalipwa.

Mheshimiwa Spika, pia nadhani aliuliza kuhusu wakulima ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwalipa Sh. 4,000,000/=. Jambo ni lile lile kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokwenda akatoa Sh. 4,000,000/= watu wakaanza tena kuja na sisi tunataka tulipwe. Lakini utaratibu ni lazima ufuatwe. Kwa hiyo, tutafuata utaratibu wa kuwahakiki wote wanaodai na hatimaye wakulima wote tutawalipa.

Na. 97

### **Kilimo cha Umwagiliaji**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, kilimo cha umwagiliaji Mkoani Mtwara kimepunguza kwa kiasi gani athari za ukame na mvua zisizoaminika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji kina nafasi ya kimkakati ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kwa kupunguza athari zinazotokana na ukame na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika usalama wa chakula.

Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 imeielekeza Serikali kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2015 asilimia 25 ya chakula chote nthini itokane na kilimo cha umwagiliaji. Aidha, mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji (*National Irrigation*

*Master Plan*) wa mwaka 2002, ulibaini hekta 1,332,700 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Mtwara.

Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.05 ili kuendeleza miradi ya kupanua miundombinu ya umwagiliaji katika Mkoa wa Mtwara. Miradi itakayofaidika ni pamoja na Skimu ya Ndanda (350ha) iliyoko Wilaya ya Masasi, Litehu (300ha) na Lipwale (450ha) zilizoko Wilaya ya Tandahimba na kupanua skimu ya Kitere (160ha) iliyopo Wilaya ya Mtwara Vijijini.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kilimo cha umwagiliaji kuwa kinga dhidi ya athari za ukame na mvua zisizoaminika katika Mkoa wa Mtwara yanaonekana katika skimu za Kitere na Makondeko (Newala) ambazo uzalishaji wa Mpunga katika skimu hizo umeongezeka kutoka tani 1.8/ha hadi wastani wa tani 5.0/ha. Ongezeko hili la tija katika uzalishaji sasa linanufaisha kaya zaidi ya 1,160.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, inaonekana kwamba kati ya hekta ambazo ziligundulika kufaa kwa kilimo cha umwagiliaji mwaka 2002 Mkoani Mtwara, ni asilimia 0.09 tu ambazo zinatumika hadi kufikia sasa mwaka 2011.

Je, ni lini sasa Serikali itatumia eneo lote Mkoani Mtwara kikamilifu kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ili iweze kutimiza azma yake ifikapo mwaka 2015?

Swali la pili. Katika maeneo ambayo yametajwa, sijasikia eneo la Malamba. Eneo hili Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara yake Mkoani Mtwara, aliahidi kwamba wakulima wa eneo hili watawezesha kuendesha kilimo cha umwagiliaji. Je, ni lini sasa wakulima wa Kijiji cha Malamba kule Wilayani Tandahimba watawezesha kuendesha kilimo cha umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mkoa wa Mtwara una eneo dogo sana la kilimo cha umwagiliaji. Kama alivyosema mwenyewe, wakati tulipoandaa mpango kabambe wa kilimo cha umwagiliaji mashambani, a *National Irrigation Master Plan* mwaka 2002 zaidi ya miaka 10, tulikuwa na vigezo tulivyofuata wakati huo. Ndio maana kipindi hicho tulikuja na maeneo ya aina tatu kwamba katika nchi nzima kuna eneo la hekta 2,300,000 zenye uwezekano mkubwa, yaani *high irrigation development, potential* ni milioni 4.8 zenye uwezekano wa kati na milioni 22.3 zenye uwezekano mdogo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara uliwekwa katika huo uwezekano mdogo. Lakini wakati huo vigezo vilikuwa ni vingi ambavyo vilikuwa ni vikwazo ikiwa ni pamoja na huduma za kijamii kama barabara, raslimali za maji na udongo. Sasa hivi vigezo vile vimeanza kupungua, barabara kwenda Mtwara ipo, unateleza, daraja la Mkapa lipo, huduma za simu sasa hivi unaweza hata ukapiga kwa kiganja na gesi ipo.

Kwa hiyo, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba vile vikwazo viliviyokuwepo sasa vinaanza kutoka taratibu. Kwa hiyo, chini ya programu ya

kuendeleza Sekta ya Kilimo eneo linalomwagiliwa katika Mkoa wa Mtwara, litaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bwawa la Malamba katika ziara ya Waziri Mkuu...

**SPIKA:** Naomba muda. Chungeni muda, tupo nje ya muda.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, pia nilikuwepo. Nilichokuwa nimeahidi wakati ule nikiwa Naibu Waziri wa Maji, nilikuwa natazama uwezekano wa kutumia programu zetu mbili za kuendeleza Sekta ya Maji na programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo ili kupunguza gharama za Serikali. Kwa sababu kama kila sekta itatengeneza bwawa lake, maji ya kunywa bwawa lake, umwagiliaji bwawa lake, basi kwanza ardhi yenyewe haitoshi.

Kwa hiyo, tutaendelea kuangalia uwezekano wa kutumia sekta hizi zote mbili ili hatimaye tuweze kujenga bwawa kubwa la Malamba kule Tandahimba ili liwanufaishe watu sio kwa kilimo cha umwagiliaji tu, bali ni pamoja na maji ya kunywa na matumizi mengine.

Na. 98

### **Tatizo la Maji Bumbuli**

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA** aliuliza:-

Upatikanaji wa maji umekuwa wa shida sana katika Jimbo la Bumbuli, ikiwemo Bumbuli Kaya na Bumbuli Misheni:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza matatizo ya maji yanayowakabili wananchi wa Bumbuli?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto inatekeleza miradi ya Vijiji 10 kuitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Vijiji vya Bumbuli Kaya na Bumbuli Misheni ni mionganini mwa Vijiji 10 katika Programu hiyo. Vijiji vingine ni Kweminyasa, Kwadoe/Kwekitui/Kwalei, Mgwashi, Erente, Ngulu, Mlola/Lwandai, Malo/Mwangoi, Kivingo na Shume/Gologolo/Madala.

Mheshimiwa Spika, hatua ya utekelezaji iliyofikiwa hadi sasa ni kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ilimwajiri Mtaalamu Mshauri ambaye ni *M/S COWI Tanzania Consulting Engineers and Planners Limited* ambaye amekamilisha usanifu wa kina wa miradi, michoro ya miradi na makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata

Mkandarasi atakayejenga miundombinu ya maji. Jumla ya shilingi milioni 172 zitatumika kama gharama ya kumlipa Mtaalam Mshauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Halmashauri ya Wilaya imetenga shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa miradi hiyo. Ujenzi wa miundombinu hiyo utaanza mwaka wa fedha 2011/2012. Baada ya kukamilisha ujenzi wa miradi hiyo matatizo ya maji yanayowakabili wananchi wa Bumbuli Kaya na Bumbuli Misheni yatakwisha.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninalo swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, miradi hii ya maji kwa mradi huu wa vijiji 10 kwa kila Wilaya, umekuwa na matatizo makubwa ya ucheleweshaji, kwanza mingi imechelewa, kwa mfano huu wa Bumbuli pesa zilitolewa toka mwaka 2009, lakini kazi haijaanza mpaka leo. Lakini kumekuwa na tatizo lingine la ukadiriaji, kwamba Mhandisi Mshauri, mfano mwingine kwenye huu mradi wa Bumbuli, mwanzo walikadiria shilingi milioni 350 baada ya kwenda na kurudi na Wahandisi wa Halmashauri wakashusha mpaka ikafikia shilingi milioni 273 na tatizo hili lipo kila mahali la ukadiriaji wa juu na wakati gharama ni za chini.

Je, pamoja na taarifa nzuri Mheshimiwa Waziri aliyoitoa Bungeni kuhusu *status* ya miradi hii: Je, Serikali ipo tayari kuleta taarifa nyingine Bungeni inayoonesha orodha ya miradi yote iliyachelewa, sababu za ucheleweshaji, hasara iliyopatikana kutokana na ucheleweshaji huo na hatua zilizochukuliwa kutokana na hasara hiyo katika Bunge lijalo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba baada ya kutoa Kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji wa mradi huu, yapo maeneo ambayo Halmashauri zimechelewesha na yapo maeneo ambayo Halmashauri zimefanya vizuri. Sasa taarifa ile ni kamilifu. Tunachosema ni kwamba kwa mfano katika Vijiji 10, Halmashauri kama imeweza kupata maji katika Vijiji vitatu, vile Vijiji vingine vitaendelezwa katika mwaka huu wa fedha mpaka Juni, 2012. Kuanzia Julai, 2012 tunaingia awamu ya pili. Kwa hiyo, vile Vijiji vingine vitaingizwa kwenye awamu ya pili ambayo ni programu inayoendelea.

Na. 99

### **Miundombinu ya Maji Musoma Kupitwa na Wakati**

**MHE. VICENT J. NYERERE** aliuliza:-

Manispaa ya Musoma na vitongoji vyake ina miundombinu ya maji ambayo imekwishapitwa na wakati na haina tena uwezo wa kuwashudumia watu wa Manispaa hiyo ikilinganishwa na ongezeko la idadi ya watu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi hao maji safi na salama?

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Vicent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa miundombinu ya maji katika Manispaa ya Musoma na Vitongoji vyake haitoshelezi mahitaji ya sasa kutokana na ongezeko la idadi ya watu. Pia miundombinu hiyo imechakaa kwa kuwa ilijengwa muda mrefu zaidi ya miaka 20 iliyopita na hivyo kusababisha kuzorota kwa huduma ya maji safi kwa wakazi wa Manispaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kulitambua tatizo hilo, tumeanza kutekeleza miradi ya maji safi na uondoaji wa majitaka katika Manispaa ya Musoma na Vitongoji vyake kwa awamu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia shirika lake la *AFD* imeshakamilisha kazi zifuatazo: Upembusi yakinifu, usanifu wa miundombinu na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni. Awamu ya pili itahusisha ujenzi wa miundombinu ifuatayo: chanzo kipyaa na mtambo wa kusafisha maji, vitajengwa katika eneo la Bukanga, tanki lenye ukubwa wa mita za ujazo 5000, bomba kuu, mabomba ya kusambaza maji, ukarabati wa mabomba yaliyochakaa na miundombinu ya majitaka. Gharama kwa ajili ya utekelezaji wa kazi ya awamu ya pili ni shilingi bilioni 50.

Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kuwasilishwa makabrasha ya zabuni *AFD* ili kupata kibali cha kutangaza *pre-qualification of contractors*. Inatarajiwa kabla ya mwezi Mei mwaka huu 2011, kibali kitakuwa kimepatikana na matangazo ya zabuni kwa ajili ya Wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu yatatolewa. Mkandarasi wa kujenga mradi ataajiriwa mwezi Novemba, 2011 na ujenzi utakamilika mwezi Desemba, 2013.

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, mradi huu nimeusikia tangu nikiwa shule na mpaka sasa haujatekelezeka na kipindi cha kukamilisha mradi ni mwaka 2013. Je, Waziri haoni ni kipindi muafaka cha kuwapatia pampu za dharura wakazi wa Musoma Mjini ili waepukane na matatizo yaliyopo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, suala la maji katika Manispaa ya Musoma linasimamiwa na Mamlaka ya Maji ya Musoma. Kwa sasa hivi kuna pampu tisa ambazo zinafanya kazi kati ya 10. Kwa hiyo, hili moja ambalo linashughulikiwa ni ili kuweza kutatua matatizo ya muda mfupi katika Mji wa Musoma waweze kupata maji.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na tumeongeza muda. Lakini sasa hivi ninao wageni wafuatao kwenye *Speaker's Gallery*. Wageni hawa ni Balozi wa Switzaland - Mheshimiwa Adrian Sichelarata, yupo Mheshimiwa Balozi wa Japan - Mheshimiwa Hiloshi Nakagawa; Balozi wa Norway - Mheshimiwa Iguna Prestic; yupo Mheshimiwa Juna Alfom Pango, huyu ndiye Balozi tuseme *Dean of Diplomatic*

*Court*, Balozi wa DRC. Hawa mabalozi mtu akiwa amekaa sana ndiyo anakuwa kiongozi wa wensiwe.

Lakini tunao mabalozi kutoka Namibia, Mheshimiwa Japhet Isack, Balozi wa Angola - Mheshimiwa Abrosio Lukoki, Balozi wa Zimbabwe - Ndugu Eliza Chomoyo, tunaye Mheshimiwa Balozi wa Afrika Kusini - Mheshimiwa Tundusie Chuliza, Mheshimiwa Kaimu Balozi wa Zambia - Mheshimiwa Patrick Ngoma na Mwambata wa ubalozi wa Malawi - Ndugu *Often Toyolani*. (*Makofî*)

Tunawakaribisha wote katika shughuli zetu za Bunge *and I am sure I am going to see some of you after this question hour. Yesterday we were unable to see you because we had quite a long day here, so it was not possible but we are arranging to see you today. Thank you. You are welcome.*

Baada ya hapo, tuna matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Maendeleo ya Jamii - Mheshimiwa Jenister Mhagama anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuwa leo tarehe 14 saa 5.00 asubuhi kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, ni saa 5.00 hii.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge la Hesabu za Serikali - Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali kuwa, kutakuwa na kikao cha Kamati leo saa 7.00 mchana, katika Ukumbi Na. 227.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira - Mheshimiwa Abdulkarim Shah, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo kutakuwa na kikao saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 219.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama - Mheshimiwa Mussa Zungu anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na kikao kitakachofanyika katika Ukumbi Na. 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya UKIMWI - Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na kikao leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa C. Naona kuna wengine humo mtafahamiana mkifika huko.

Kuna tangazo la Utawala wanaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba kampuni ya Serengeti *Breweries Limited* watafanya uzinduzi wa kinywaji aina ya *John Worker*. Haya, tunatangaza biashara hapa katika *hotel* ya Dodoma huko usiku leo wanaopenda kwenda kuzindua huko waende, hii siyo sehemu ya kazi.

Kuna Wabunge akinamama mlipokea mwaliko wa Mheshimiwa Mke wa Waziri Mkuu kwa ajili ya shughuli tarehe 16, tumeahirisha kwa sababu tarehe 16 kuna *TBL* imeamua kuwapongeza Wabunge katika Ukumbi wake. Kwa hiyo, kutakuwa na shughuli ya Wabunge wote. Kwa hiyo, ule mwaliko mtapewa taarifa wakati mwininge.

Baada ya kutangaza hayo, Waheshimiwa Wabunge kama mlivyoona tuna wageni pale, itabidi nikawaone. Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Naibu Spika aweze kuendelea na kazi kwa niaba yangu.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Katibu, shughuli inayofuata!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Naam!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Katibu, shughuli inayofuata. (*Makofi*)

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **AZIMIO**

**Azimio la Kuridhia Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika**  
**(The SADC Protocol On Science, Technology And Innovation)**

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na kutuwezesha leo kuwepo hapa Bungeni. Napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na Watanzania ambao wamemchangua kuongoza nchi yetu kwa kipindi kingine kwa miaka mitano. (*Makofi*)

Vilevile nampongeza sana Dr. Mohamed Ally Bilali - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikuwa mgombea mwenza wa Rais wetu. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa kwanza kuniteua kuwa Mbunge na pili kwa kuniamini na kuniteua kuwa katika Baraza lake la Mawaziri kama Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. (*Makofi*)

Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda - Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Namshukuru pia kwa maelezo yake ya mara kwa mara ambayo yameniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo. Nawapongeza pia Mawaziri wote walioteuliwa kushika nyadhifa hizo na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa na Watanzania waliowachagua kuwa wawakilishi wao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Anne Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano ya uhai wa Bunge hili akiwa ni Spika wa kwanza mwanamke. Pia nakupongeza wewe mwenyewe kwa kushika nafasi ya Naibu Spika kwa kipindi cha miaka mitano ya uhai wa Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi haziwezi kukamilika bila kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa hatua kubwa iliyopigwa katika kupanga safu ya uongozi katika Kamati Kuu na katika safu ya utendaji. Nampongeza Bwana Wilson Mukama kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Aidha, nampongeza Mheshimiwa John Chilligati - Mbunge na Bwana Vuai Ali Vuai kwa kuteuliwa kuwa Manaibu Makatibu Wakuu wa Tanzania Bara na Zanzibar. Vilevile nawapongeza wote waliochaguliwa na kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi hapo tarehe 11 Aprili, 2011. Baada ya pongezi hizom sasa naomba niende kwenye Azimio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaleta Azimio linalohusu Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu au bidaa ya maendeleo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*The SADC Protocol on Science, Technology and Innovation*) ambalo linaomba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulikubali na kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa maelezo zaidi kuhusu Itifaki hii, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Miundombinu - Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba na Wajumbe wote wa Kamati ambao walijadili Azimio hili na kutoa maoni yao katika kikao cha Kamati hiyo tarehe 11 Aprili, 2011.

Maoni waliyotoa yamesaidia katika kuboresha Azimio. Aidha, naomba nimshukuru Waziri Kivuli wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia - Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mbunge kwa ushirikiano mkubwa na maoni aliyotoa kama Waziri Kivuli ambayo pia tumeyazingatia katika kuboresha Azimio hili. Hii ni pamoja na pendekazo la kutumia neno bidaa baada ya ubunifu ikiwa ni tafsiri ya *innovation*. Kutokana na wengi kufahamu ubunifu kama ni tafsiri ya neno *innovation*, tumeafiki kutumia maneno haya mawili katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii inahusu kuimarisha ushirikiano kati ya nyanja za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika nchi wanachama. Itifaki hii itakuza ushirikiano katika masuala ya utafiti na maendeleo, ugharamiaji wa tafiti za kikanda pamoja na kukuza tafiti kuhusu teknolojia mpya na zile zinazojitokeza.

Itifaki hii inalenga pia katika juhudi za kuimarisha Sera ya Sayansi na Teknolojia za Nchi Wanachama. Ili kuhakikisha kuwa malengo ya Itifaki hii yanafikiwa pamoja na mambo mengine aliyoeleza, Itifaki hii inapendekeza kuanzishwa kwa kitengo cha

Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Bidaa ndani ya Sekretarieti ya SADC, *the SADC Science, Technology and Innovation Unit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii ilisainiwa na Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika SADC uliofanyika tarehe 17 Agosti, 2008 Mjini Santon Johannesburg Afrika Kusini. Baadhi ya nchi za SADC ambazo zimeshasaini na kuridhia Itifaki hii ni pamoja na Afrika Kusini, Msumbiji, Botswana, Malawi na Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi napenda kuwasilisha Azimio hili kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA**, Itifaki hii inahusu kuimarisha ushirikiano katika masuala ya Sayansi, teknolojia na ubunifu (bidaa) katika nchi wanachama itakuwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Kitengo cha Sayansi na Teknolojia, Ubunifu (bidaa) ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. *The SADC Science, Technology and Innovation Unit* iliyo sainiwa na Wakuu wa Nchi husika mnamo tarehe 17 Agosti, 2008 huko Santon Johannesburg Afrika Kusini.

**KWA KUWA**, lengo kubwa ya Itifaki hii ni kuimarisha ushirikiano na kukuza maendeleo uhalishaji na umahiri katika sayansi, teknolojia na ubunifu kwa nchi wanachama ili hatimaye ziweze kufanya mambo yafuatayo:-

- (i) Kuanzisha mifumo itakayo imarisha uhusiano wa kikanda katika Sayansi Teknolojia na ubunifu bidaa;
- (ii) Kuweka muundo wa kusimamia na kuratibu utekelezaji wa programu za sayansi, teknolojia na ubunifu *and* (bidaa) kikanda;
- (iii) Kukuza utungaji wa sera za pamoja za sayansi, teknolojia na ubunifu; na
- (iv) Kukuza ushirikiano katika masuala ya tafiti na maendeleo, ugharamiaji wa tafiti za kikanda pamoja na kukuza utafiti kuhusu teknoloji mpya na zile zinazojitokeza.

**KWA KUWA**, nchi tano za SADC zimekwishasaini na kuridhia Itifaki hii ambazo ni pamoja na Afrika Kusini, Msumbiji, Botswana, Malawi na Zambia ni vizuri kwa Tanzania kuridhia Itifaki hii pia;

**KWA KUWA**, chimbuko la Azimio hili ni kutekeleza mkataba uliounda Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*The SADC Treaty*) kifungu cha 21(3)(e) pamoja na kutekeleza maamuzi ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi za SADC waliokutana huko Santon Johannesburg Afrika Kusini tarehe 17 Agosti;

KWA KUWA, baadhi ya vipengele muhimu katika Itifaki hii ni kama ifuatavyo:-

(i) Vifungu Na. 2 hadi 5 vinatoa malengo ya kuanzisha Itifaki sheria na Kanuni maeneo ya ushirikiano na mfumo wa utaratibu na uwezeshaji.

(ii) Vifungu Na. 6 na 7 vinatoa maelezo juu ya masuala ya kifedha na ubadilishanaji wa taarifa kwa kutumia viashiria vya sayansi, teknolojia na ubunifu *into break at bidaa*.

(iii) Kifungu Na. 8 kinatoa maelezo ya jinsi ya kuweka mfumo endelevu wa utaratibu na uwezeshaji wa maeneo ya ushirikiano kwa kuanzisha viashiria vya sayansi, teknolojia na ubunifu bidaa, yaani tathmini na udhibiti.

(iv) Vifungu vingine vinatoa maelezo juu ya jinsi ya kuridhia pamoja na mambo mengine ya msingi ambayo yanalingana na vipengele vingine vilivyoko katika Itifaki nyingine za *SADC*.

Kwa, kuridhia Itifaki hii, Tanzania itanufaika na mambo yafuatayo:-

(a) Wataalam wa Tanzania watashirikiana na wa nchi nyingine za *SADC* katika masuala ya tafiti, na ubadilishanaji wa taarifa zinazohusu sayansi, teknolojia na ubunifu ambayo tunaita vilevile ni bidaa; (*Makofi*)

(b) Katika faida hizo ubadilishanaji uzoefu juu ya matumizi na matokeo ya tafiti mbalimbali na jinsi teknolojia zinazotokana na tafiti hizo zinavyoweza kuongeza tija katika nchi zetu za *SADC*.

(c) Mwisho, kutoa fursa kwa masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu kupewa kipaumbele katika mipango ya nchi zetu za *SADC*.

KWA KUWA, kulingana na ibara ya 15 ya Itifaki hii, nchi wanachama zitaridhia Itifaki hii kulingana na taratibu za nchi husika na kwa hiyo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndilo lenye mamlaka ya kuridhia Itifaki hii;

KWA KUWA, hakutakuwepo na gharama yoyote katika kuridhia Itifaki hii zaidi ya michango ya kawaida ya kila mwaka ya Serikali kwenye *SADC*;

HIVYO BASI, Waheshimiwa Wabunge wanaombwa kutafakari mapendekezo yaliyomo katika Azimio hili na kukubali Itifaki ya sayansi, teknolojia na ubunifu (bidaa) ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika iridhiwe kwa mujibu wa ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ili kuiweka nchi katika nafasi nzuri ya kushirikiana na nchi nyingine za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika;

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Profesa. Sasa naomba kumwita Msemaji wa Kamati iliyopitia Azimio lililo mbele yetu.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuongea mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba uniruhusu nitumie nafasi hii kwanza kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kigoma Mjini kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao. (*Makofi*)

Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na Watanzania na kwa kazi nzuri anayofanya ya kuendeleza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia uniruhusu nimpongeze Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kuteuliwa na Rais kuendelea na wadhifa wa Waziri Mkuu wa nchi yetu na kwa kazi nzuri anayofanya ya kuendeleza Taifa letu. Nachukua nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri wote waliopewa nyadhifa hizo na Mheshimiwa Rais, nawaomba waendelee kuchapa kazi ili tuweze kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu tena nikipongeze Chama changu kwa mageuzi makubwa yaliyofanyika. Kwa kweli ni dalili njema na inayotuhakikishia ushindi huko tunakokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijafanya jambo jema nisipowashukuru familia yangu hasa mke wangu Iveti ambaye amenivumilia sana wakati wote wa pilikapilika za kampeni na amekuwa ananiunga mkono katika kipindi chote cha kazi zangu kama Mbunge, pia na kijana wangu Bizi na mtoto wangu wa kile Irakoze. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Bidaa (Ubunifu) ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (*The SADC Protocol On Science, Technology and Innovation*).

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Anne S. Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wewe Mheshimiwa Job Ndugai kuwa Naibu Spika wa Bunge letu. Kamati yangu inawatachia heri na kuwaombea kwa Mwenyezi

Mungu ili awawezeshe kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge hili kwa ufanisi mkubwa.

Aidha, nawapongeza Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote za Bunge kwa kuchaguliwa kwao kuongoza Kamati zao katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kunichagua kuwa Mwenyeekiti wao. Hakika ni heshima kubwa kwangu, nami nitaienzi daima kwa kushirikiana nao vizuri na kufanya kazi kwa bidii ili tuweze kutekeleza wajibu wetu katika kuendeleza miundombinu ya nchi hii. (*Makofi*)

Aidha, nawapongeza Wajumbe wa Kamati hii kwa kunipa heshima ya kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba – Mwenyeekiti na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela - Makamu Mwenyeekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Lolesia Jeremiah M. Bukwimba, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Ritta Enester Kabati, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, Mheshimiwa Regia Eselatus Mtema, Mheshimiwa Mbarouk Rajab Mohamed, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu na Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Rukia K. Ahmed, Mheshimiwa Kasikira Rosweeter Faustin, Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mheshimiwa Inocent Edward Kalogeresi, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mheshimiwa Saidi Amour Arfi, Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machemli, Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Rita Louise Mlaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa Itifaki hii italinufaisha Taifa letu katika Nyanja mbalimbali zikiwemo, kuwezesha wataalam wa Tanzania kushirikiana na wataalam wa nchi nyingine katika masuala ya utafiti na ubadilishanaji wa taarifa zinazohusu Sayansi, Technolojia na Bidaa (ubunifu); kuwezesha ubadilishanaji wa uzoefu kuhusu matumizi na matokeo ya tafiti mbalimbali na jinsi teknolojia zinazotokana na tafiti hizo, zinavyowenza kuongeza tija katika nchi za SADC na kutoa fursa kwa masuala ya Sayansi, Teknolojia na Bidaa kupewa kipaumbele katika mipango ya nchi.

Ibara ya 6(1) inazitaka nchi wanachama kutenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza Itifaki hii ndani ya nchi zao. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa kuridhiwa kwake hakutaiiongezea gharama nchi yetu kwani michango inayotolewa sasa na nchi yetu kwa

ajili ya SADC itatosha kuendesha Idara na majukumu mengine yatakayotokana na utekelezaji wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati baada ya kupokea maelezo kutoka Serikalini kuhusu Itifaki hii, Kamati ilijadili na kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Itifaki hii, kwani katika ulimwengu wa leo, maendeleo ya kiuchumi hayawezi kupatikana bila kutumia sayansi na teknolojia. Aidha, ushirikiano unaokusudiwa kuanzishwa utasaidia kukuza na kuendeleza sayansi na teknolojia hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kunufaika na Itifaki hii, juhudzi zifanywe kuwekeza katika masuala ya sayansi na utafiti kama Ibara ya 2(d) ya Itifaki hiyo inavyoeleza. Aidha, kusudio la kutenga 1% ya pato ghafi la Taifa kwa ajili ya utafiti litekelezwe kwa vitendo. Nchi za mashariki ya mbali kama vile China, India, Indonesia, Malaysia na nyingine nyingi zimeendelea kiuchumi kwa sababu ya kutilia mkazo katika sayansi, teknolojia na bidaa.

Nchi yetu ifanye bidii kuchangamkia fursa zitakazojitokeza kutokana na utekelezaji wa Itifaki hii kwani Idara na vitengo mbalimbali vitaanzishwa ambavyo vinaweza kutoa ajira kwa Watanzania katika Idara na vitengo hivyo. Kama utekelezaji wa Itafiki hii utahitaji kuwa na Makao Makuu, Kamati inashauri Serikali ishawishi Makao Makuu yake yawe nchini mwetu kwa mujibu wa Ibara ya 5(1), 5(3)(d).

Ibara ya 2(h) ya Itifaki hii inaeleza azma ya kutambua, kuthamini na kukuza vipaji na teknolojia ya wazawa. Kamati inashauri Taifa letu lihimize wananchi kuwa wabunifu na juhudzi za kitaifa zifanywe kuendeleza na ubunifu huo badala ya hali ya sasa ambapo hakuna mpango rasmi wa kutambua na kuendeleza vipaji nchini. Kwa mfano, gunduzi mbalimbali zimefanyika na wazawa hapa nchini, lakini zimepotea kwa kukosa msukumo wa kitaifa na kuachiwa wagunduzi kuijendezea wenyewe.

Taifa letu linahimiza sana masomo ya sayansi na teknolojia ikiwemo kuanzisha Vyuo mbalimbali vilivyoyikita katika taaluma za sayansi na teknolojia. Itifaki hii (Ibara 2(l) inahimiza uondoaji wa vikwazo kwa wataalam kufanya kazi katika nchi yoyote katika ukanda huu. Kamati inashauri wataalam wetu wanaohitimu vyuo hivyo wapewe vivutio ili wasishawishike kutumia utaalamu wao nje ya nchi kama mwelekeo ulivyo sasa hapa nchini.

Kabla ya kuridhia Itifaki hii, Serikali iweke wazi bajeti itakayohitajika kuitekeleza kama Ibara ya 6 (1) ya Itifaki hii inavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 (f) ya Itifaki hii inaeleza uanzishwaji wa utaratibu wa kutumia vipaji vya Waafrika waishio nje ya Bara la Afrika. Kuna wataalam wengi sana walio nje ya nchi yetu. Kamati inashauri uandaliwe utaratibu wa kuwatambua

Watanzania hawa ili iweze kuwatumia katika sayansi, teknolojia na bidaa badala ya kutegemea wataalam wasio Watanzania.

Juhudi za makusudi zifanywe kuimarisha Taasisi za Utafiti na Teknolojia zilizopo hapa nchini Ibara ya 2(k) inayohimiza ushirikiano wa Taasisi za aina hiyo katika nchi wanachama. Udhifu wa Taasisi zetu utasababisha utegemezi mkubwa kwa tafiti na bidaa mbalimbali jambo ambalo litavunja heshima ya nchi na wataalam wetu kutothaminiwa.

Juhudi zifanywe ili kuoanisha sera za sayansi, teknolojia na bidaa zilizopo hapa nchini na zile zitakazotungwa baada ya utekelezaji wa Itifaki hii kuanza kama Ibara 2(c) inavyoeleza. Uoanishaji huu utaondoa mgongano wa utekelezaji wa sera hizi mbili, sera za ndani ya nchi na sera za utekelezaji wa Itifaki. Serikali ijipange vizuri na kuondoa urasimu katika kutekeleza maamuzi mbalimbali yatakayokuwa yanaamuliwa na mamlaka zilizoainishwa kwenye Ibara 5(3) na 5(5).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia - Mheshimiwa Prof. Makame M. Mbarawa, Naibu Waziri - Mheshimiwa Charles M. Kitwanga, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo - Dr. Florens Turuka na Maofisa wengine wa Wizara hiyo kwa ushirikiano wao na kuwasilisha Azimio hili mbele ya Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru tena Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa maoni na ushauri walioutoa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Itifaki hii kwa manufaa ya nchi yetu na vizazi vijavyo. Aidha, nampongeza Katibu wa Kamati hii, Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi kwa kazi nzuri ya kuandaa taarifa hii kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni hayo, Kamati katika ujumla wake haina pingamizi juu ya kuridhiwa kwa Azimio hili na inaliomba Bunge lako Tukufu ikubali kuliridhia ili kuendeleza ushirikiano wa nchi zetu katika Nyanja za sayansi, teknolojia na bidaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni haya, Kamati yangu inaunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba - Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. Sasa naomba nimkaribishe Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Azimio hili, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi.

**MHE. PROF. KULIKOYELA KAHIGI - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuongea nikiwa na hadhi ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu masuala ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kuchukua fursa hii kwanza kutoa shukrani zangu za dhati kwa

Kiongozi wa Upinzani kwa imani yake kwangu kwa kunitua ili niisimamie Wizara hii. Ahsante sana.

Mheshima Naibu Spika pili, nakushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani hapa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kanuni ya 53(6)(c), toleo la mwaka 2007.

Tatu, kwa unyenyekevu mkubwa, naomba nitoe shukrani kwa Chama changu cha CHADEMA pamoja na wananchi wote wa Jimbo la Bukombe kwa kushikamana nami katika mchakato mzima uliopelekea mimi kuwa hapa Bungeni ili niwawakilishe. Nawashukuru sana, na ninawaahidi kwamba nitawatumikia kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la *Itifaki* ambayo imeletwa mbele yetu ili Bunge hili Tukufu liiridhie ni kukuza ushirikiano, maendeleo, uhawilishaji na umahiri wa sayansi, teknolojia na bidaa/ubunifu/ugunduzi katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizo Kusini mwa Afrika. Hili ni lengo la maana sana, hasa ikizingatiwa kuwa bila kukuza kwa upangilifu na umakini, sayansi na teknolojia na ubunifu, hakuna maendeleo yoyote ya maana kiteknolojia yatakayotokea katika sekta zote husika: kilimo, ufugaji, afya, elimu, viwanda, na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kusisitiza kuwa tofauti kubwa kuliko zote ya kimaendeleo baina ya nchi zilizoendelea na nchi ambazo zinaendelea hukutwa katika kiwango cha usambaaji na utumiaji wa sayansi na teknolojia katika maeneo mbalimbali ya maisha. Nchi huanza kupiga hatua za kimaendeleo inapokamilisha zoezi la kuhawilisha sayansi na teknolojia na kuanza kufanya ugunduzi katika maeneo mbalimbali ambayo yanalenga utatuzi wa matatizo yanayowakabili wananchi wake. Bila kufanya hivyo maendeleo hususua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya (2) hadi ya (5) katika Itifaki zinahusu malengo, misingi, maeneo ya ushirikiano na taratibu za kiasasi. Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na ibara hizi. Tunapenda kuongeza kwamba mambo haya yanayolezwu katika Itifaki, siyo mageni hapa nchini. Yanafanana na yanaoana na dhima za Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Tume hiyo mwaka 1986 - 5(1) – (4) na pia yanawiana na Sera ya Sayansi na Teknolojia ya Taifa ya mwaka 1995.

Jambo jipya la tija ambalo litaletwa na Itifaki hapa nchini ni ushirikiano na uunganishaji wa nguvu za nchi za Jumuiya katika kukuza sayansi, teknolojia na ubunifu, jambo ambalo linapaswa kuungwa mkono, hasa kwa kuzingatia kwamba “*umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu*” hasa tunapopambana na utandawazi wa kimaghribi. Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo pia na ibara zilizobaki (yaani 6 hadi 19).

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri. Kambi Rasmi ya Upinzani haipingani kimsingi na azimio, lakini inaishauri Serikali kutumia fursa hii kujipanga vizuri na kurekebisha mapungufu mengi yaliyopo katika utekelezaji wa Sera ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapungufu hayo yako katika maeneo matatu, jambo la kwanza ni utafiti. Utafiti ni mionganoni mwa maeneo ambayo angalau Tanzania inaweza kujivunia. Ni tafiti nyingi ambazo zimefanyika toka tupate Uhuru. Swali la kujiuliza ni: Je, ni tafiti ngapi zimetumika kuleta maendeleo? Ni tafiti ngapi ambazo matokeo yake yamesambazwa na kuwa sehemu ya ujuzi wa wananchi wengi? Je, ni tafiti ngapi ambazo Serikali imezigharimia?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo hapa ni kusuasua kwa Serikali kugharimia tafiti za kitaalamu. Tafiti nyingi zinagharimiwa na mashirika ya nje. Tunaamini kuwa hakuna nchi ambayo imeendelea kwa kugharamiwa tafiti na nchi za nje. Inafaa Serikali ijipange vizuri hapa, ianze kubeba jukumu la kugharimia tafiti katika Vyuo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubunifu/ugunduzi ni mionganoni mwa mambo ambayo hayakupangwa vizuri hapa nchini. Katika taratibu za Tume na vituo vingine vya utafiti, hakuna namna ya kumsaidia mgunduzi/mvumbuzi ambaye hayuko katika kituo hicho. Wagunduzi wengi hufa na magunduzi yao. Labda tungejifunza kutokana na tukio la hivi karibuni linalomhusu kijana Said Omari wa Zanzibar, ambaye ametengeneza gari lake la pili na ambaye Waziri wa Kazi na Uwezeshaji wa *SMZ* amemwahidi kumsaidia ili akapate mafunzo zaidi Japan au nchi nyingine. Tutafute njia iliyopangwa vizuri ya kuwaendeleza wagunduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhawilishaji wa teknolojia ni mchakato wa kuhawilisha stadi, maarifa, teknolojia, njia za uundaji wa vitu, mifano ya vitu vilivyoundwa kutoka kwenye Vituo vya Utafiti kwenda kwa watumiaji kuhakikisha kuwa maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia yanasaambaa. Teknolojia ikiwafikia wengi wakaikubali wataifanya kuwa yao, na wanaweza kuikuza hadi kuibua vitu vipya, michakato mipyaa au huduma mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba uhawilishaji ni kiungo dhaifu katika utekelezaji wa Sera ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania. Ni kweli kuwa Tanzania ina Vyuo Vikuu na Vyuo vingine ambavyo vinahusika na utafiti katika sayansi na teknolojia katika nyanja mbalimbali.

Mifano ya Vyuo Vikuu ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya cha Muhimbili, Taasisi ya Raslimali za Maji ya Rwegarulila, na kadhalika. Vyuo kama hivi hujitahidi kuhakikisha kuwa namna fulani ya uhawilishaji inatokea kwa njia za mafunzo, semina, warsha na nyinginezoo.

Pia kuna Kituo cha Ubunifu na Uhawilishaji wa Teknolojia (*Technology Development and Transfer Center*) kilichorithi majukumu ya Sayansi na Teknolojia yaliyokuwa yamebebwa na Taasisi ya Bidaa ya Uzalishaji (*Institute of Production Innovation*) kilichoko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hali kadhalika, Serikali kupitia Idara mbalimbali, inaendeleza taratibu mbalimbali za uhawilishaji wa sayansi na teknolojia katika sekta mbalimbali, hasa kuwafikia wananchi wa kawaida. Hili linafanya kupitia programu za kilimo, ufugaji, uvuvi, afya, na kadhalika. Hata hivyo, programu hizi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali, mathalan upungufu wa Maafisa Ugani, upungufu wa vifaa na matatizo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uhawilishaji wa teknolojia uwe na manufaa kwa watu wengi zaidi na uwe endelevu, mfumo thabiti wa uhawilishaji unahitajika. Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa mapendekezo yafuatayo:-

Sera ya Sayansi na Teknolojia ipitiwe ili izingatie changamoto za sasa; Kituo cha Ubunifu na Uhawilishaji cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiimarishe kisera na kimajukumu, pamoja na majukumu mengine, kiratibu uhawilishaji wa sayansi na teknolojia nchini kote, ni kwamba hakuna mfumo ambao unaeleweka kwa kweli wa uhawilishaji wa sayansi na teknolojia ambao unaratibiwa na asasi moja.

Kwa jinsi tunavyofahamu sisi, inawezekana tunaweza kupata maelezo kutoka kwa Waziri, lakini tunachopendekeza ni kwamba kuwe na mfumo mzuri ambao unaratibiwa mahali pamoja; njia mbalimbali za uhawilishaji wa teknolojia ziimarishe ikiwemo msisitizo wa matendo uimarishe katika vyuo vya ufundi, Vyombo vya habari (radio, TV, magazeti na vinginevyo) vitumike zaidi katika shughuli ya uhawilishaji katika kupeleka maarifa na taarifa mbalimbali kwa wananchi, mafunzo kazini yaimarishe na Semina na Warsha.

Utaratibu huu wa uhawilishaji uimarishe kwa kuhakikisha vifaa muafaka vinatumika. Kama nilivyosema, kuna mambo mengine ambayo lazima yaimarishe, mengine ambayo ninaweza kufikiria sasa hivi ni mafunzo ya ugani na mengineyo ambayo yapo yanaendelea sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa azimio hili liridhiwe, lakini Serikali itumie fursa hii iliyojileta yenewe kujipanga vizuri ili isahihishe mapungufu yaliyo katika utekelezaji wa Sera ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi - Mbunge wa Bukombe na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Sasa baada ya hapa ninaomba tuendelee na uchangiaji katika jambo hili lililo mbele yetu. Mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa atafuatia.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niendelee kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na kunipa nafasi ya kuchangia kama mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa heshima na taadhima, nichukue nafasi niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kunipitisha jana kuwa Mwenyekiti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba niwaahidi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, sitawaangusha. Tutafanya kazi kwa kufuata taratibu na kanuni, lakini pia tutashirikiana katika kila jambo kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nikuthibitishie wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Spika kwamba nitafanya kazi kwa kufuata miongozo yenu kwa kuwa ninyi ndio mtakuwa viongozi wetu katika Bunge letu mkitusadia kufanya kazi hiyo. Naomba nikushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye *agenda* yenyewe ambayo inatuambia tukubali kuridhia azimio hili la SADC linalohusu masuala ya sayansi, teknolojia na utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasahau ninaomba kwanza kuunga mkono hoja hii ya kuridhia azimio husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba bila kuzingatia masuala ya sayansi na teknolojia, kwa kweli hakuna maendeleo. Lakini niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwa kiasi kikubwa imelielewa suala hili na unaona kila siku imekuwa ikiweka mkazo wa dhati katika maeneo mbalimbali yanayohusu masuala ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nishauri mambo yafuatayo: Kwanza, ni suala la ubunifu. Suala la ubinifu ni suala la msingi. Ukiangalia kwenye azimio lenyewe, malengo ya azimio kipengele cha 2(d) kinasisitiza suala zima la kuhakikisha tunaibua ubunifu katika nchi zetu za SADC kwa manufaa ya maendeleo ya nchi zetu, lakini pia kwa kujenga misingi imara ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesoma historia, nchi nyingi za Ulaya zimeendelea kwa sababu ya ubunifu. Viwanda vikubwa hivi ambavyo viko sasa hivi kwenye nchi za Ulaya, vimewasaidia wamepiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Ukiangalia karne ya 10, 11 hivi maendeleo ya nchi za Ulaya yalikuwa ni sawa sawa na nchi za Afrika tukiwemo Tanzania. Lakini sisi tulikuwa tunaongoza katika teknolojia ya umwagiliaji ambayo hata Ulaya haikuwepo na mfano mzuri wa teknolojia ya umwagiliaji ulikuwa katika nchi ya Misri. Misri kule ndiyo walioanzisha matumizi ya kalenda kwa sababu ya ubunifu, lakini kalenda sasa hivi inatumika Ulimwengu mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unaona kabisa sisi tunayo makumbusho ya kale hata kule Loliondo kwa Babu kuna mambo mengi ya kale, lakini yalikuwa yanaonesha ubunifu tulikuwa nao toka enzi zile za mababu zetu. Ninachotaka kusema ni nini? Ubunifu ni kitu cha msingi sana katika maendeleo ya Taifa lolote, na tukitaka kuendelea

mbele zaidi tuwaweke vizuri vijana wetu hawa wabunifu. Sasa hivi katika kila kona ya nchi yetu utasikia kuna kijana kaunda gari, hivi akishaunda gari inaishia wapi? Amewezeshwa vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Ruvuma, Mbanga kuna kijana amejitengenezea gari yake na anaendelea nayo, inamsaidia kubeba mazao shambani na anaendelea kuifanyia kazi. Ukikutana na mke wake anasema wala sikuota kama siku moja nitakuwa na gari, lakini mume wangu ametengeneza haka kagari, ukikaangalia kako kako, lakini kanafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kijana huyu akiwezeshwa, nchi yetu itatengeneza magari mangapi? Tutaachana na hii habari ya kuhangaika na uagizaji wa magari kutoka nje ambayo yanamaliza pesa nyingi. Ninachotaka kusema tu ni kwamba, ubunifu ni kitu cha msingi, tukizingatie sana na ndicho kitakachotusaidia kuwa na maendeleo endelevu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu hiyo hiyo ya pili imezungumzwa sana sana kukuza vipaji vyta watoto wetu katika mashule kwenye eneo la sayansi na teknolojia. Naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imeona umuhimu huu watoto wetu wanaofaulu vizuri masomo ya sayansi, wamekuwa wakipewa kipaumbele kwenye Vyuo vikuu vyetu, lakini nadhani juhudhi iongezwe. Hebu tuiangalie mitaala yetu kwenye shule zetu kwa sasa hivi ikoje? Hivi mitaala yetu inaendana na sayansi na teknolojia ya wakati wa sasa? Hivi sayansi tunayoifundisha inaweza kweli kugusana kabisa na mahitaji tunayoyataka kwa sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Kilimo Kwanza. Hivi kwenye hiki kilimo kwanza tuna-*apply* nini azimio hili kuhamishia kwenye utendaji wa mpango wetu mkakati wa kukuza kilimo? Tunahitaji matrekta, tunahitaji mbegu bora na za kisasa, tunahitaji madawa ya kusaidia mazao yetu, tunahitaji vitu vingi vingi tu pale na ukivitazama vile vitu vyote vinaangukia katika kutekeleza azimio tutakaloridhia leo. Kwa hiyo, utaona kwamba sera zetu zimeshajiunganisha vizuri tu na azimio hili, lakini hapa kazi kubwa hebu tujipange vizuri tuchukue sasa faida ya azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye hili azimio, yapo mambo mazuri, upo uwezeshaji wa kujihusisha kikanda. Sasa kama sisi tunakosa hiki, tunaweza kukipata kwa wenzetu na kwa kuwa sisi tayari tuna mipango yetu ndani ya nchi, kwa hiyo tutakaporidhia azimio hili tunaweza kujikuta tuna faida kubwa sana na nimetoa mfano wa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuboreshe agenda tulizonazo kwa kuridhia mikataba hii, lakini kwa faida ya nchi yetu na kwa maendeleo ya nchi yetu na hasa katika sekta ya kiuchumi na kupambana na umasikini. Ni wakati muafaka tufanye maamuzi sahihi na maamuzi sahihi ni kama haya tunayokusudia kuyafanya leo. (*Makofi*)

Sehemu hiyo hiyo ya pili ya malengo ya hii Itifaki imeelezwa wazi kwamba, ni lazima nchi wanachama baada ya kuridhia hili azimio hebu waangalie kuongeza bajeti kwenye masuala ya utafiti. Kwenye suala la utafiti, bado tuko hoi, hebu tuanze kuona umuhimu wa kuwekeza zaidi na zaidi kwenye eneo hili la utafiti. Tunavyo Vyuo vingi vinavyoshughulika na masuala ya utafiti: Je, bajeti tunayoitenga kusaidia tafiti mbalimbali itatusaidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Peramiho linaongoza kwa kilimo cha mahindi katika Mkoa wa Ruvuma. Kila mwaka kupitia Mpango wa Kilimo Kwanza na ruzuku ya kilimo tunawahamasisha wakulima wetu watumie mbolea na mbegu bora lakini tulijikuta hatuna mbegu mpaka tutegemee mbegu zinazozalishwa Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napata shida kidogo kwa sababu mbegu nyingine kweli ni nzuri, lakini nyingine ulikuwa unaona kabisa kwambahaziendani na mazingira halisi ya maeneo yetu. Inawezekana kule Kenya tunapishana usiku kidogo, kwa hiyo, inapozalishwa kule inakuja kupandwa kwenye usiku kidogo wa Jimbo la Peramiho, ni lazima itasinyaa, haitaweza kustawi vizuri kama inavyostawi kule Kenya. Ama mbegu labda tuzitoe nchi za Ulaya labda hali ya hewa ilivyo kule na utafiti tunaoufanya kwetu kuhusiana na aina ya udongo tuliyonayo, kiasi cha mbolea na tindikali iliyoko kwenye udongo wetu vinalingana namna gani? Lakini lengo letu jema la kuwaendeleza Wakulima wetu, tunafanya nini?

Kwa hiyo, haya yote unagundua kabisa bila kufanya utafiti hata tukiwa na mipango mizuri kiasi gani hatutaweza kufika.

Kwa hiyo, ninaomba sana tunaporidhia azimio hili, hebu tufikiri tunafanya nini ili kuongeza bajeti. Tunaongezaje bajeti kwenye masuala ya utafiti ili yaweze kuwasaidia wananchi wetu na hasa asilimia kubwa ya Watanzania ambao wao ni wakulima? Kwa hiyo, tuboreshe mitaala. Tuwawezesha watoto wetu wasome, tuongeze bajeti kwenye utafiti, wanapomaliza watarudi kuja kuwa wataalam wazuri na watatusaidia sana kuendeleza nchi yetu na sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba wapo wataalam wetu wazuri sana tunawasomesha hapa Tanzania, wanasona kwa kiwango kizuri kweli, lakini imekuwa homa fulani, badala ya kufanya kazi ndani ya nchi yetu wanakimbilia nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifika huko nje unaweza kwenda kwenye hospitali kwa mfano, unakutana na daktari mzuri, bingwa na ana heshima kubwa kweli, lakini ni Mtanzania. Unaweza kwenda kwenye sekta ya kilimo mahali fulani unakutana na mtafiti mzuri, anafanya kazi nzuri lakini yuko nje ya nchi yetu ya Tanzania.

Nadhani baada ya kuridhia Azimio hili tuone namna gani hawa Watanzania wenzetu wanajenga moyo wa uzalendo, wanarudisha yale mambo mema nyumbani kwao. Tujenge tabia ya kuwatambua kujua wanachokifanya nje na mahitaji tuliyonayo katika nchi yetu tuwashawishi warudi watusaidie. Hata kama hawarudi kwa maana ya kufanya kazi tuwe na *forum* ambayo itawasaidia kurudi na kushirikiana na timu za mabingwa

walioko katika nchi yetu kufanya kazi kwa pamoja kwa faida ya Watanzania na kwa faida yetu na kwa faida ya nchi yetu. Hilo ni suala la msingi sana na ni suala la muhimu na kwa kweli ni lazima pia lenyewe tulitazame kwa namna yake ili liweze kufanya kazi nzuri ya kutuendeleza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio limeonyesha humu ziko tafiti nyingine za kawaida kabisa za kijamii. Lakini hazijatambuliwa, hazijapewa nguvu na mvuto wa kuonekana zinaweza kusaidia. Nyingi sana na Waheshimiwa Wabunge hapa wakipewa nafasi yoyote wakaeleza kwenye Majimbo yao kuna watafiti wangapi wa kawaida tu, tena wengine wala sio wasomi wamejifanyia tafiti zao kulingana na mazingira wanayoishi. Lakini zimekuwa zikisaidia sana kwa namna moja au nyingine katika mazingira yale. Ebu tuanze kuwatambua wale, tuhamishe utafiti wao ule kuwa wa kisayansi zaidi, tuhamishe ubunifu wao ule wanaotumia katika maeneo yao kuwa ya kitaalam zaidi, halafu tuuingize kwenye mipango yetu tuufanyie utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili ni la msingi kabisa kwa maendeleo yetu ya Watanzania, Azimio hili ni la msingi kabisa. Nilikwenda kutembelea nchi ya Malaysia mwaka jana tulimkuta mjasiriamali mmoja aliyeanza kwa kuunganisha baiskeli lakini sasa hivi ni mfanyakishara mkubwa sana, anaongoza kwa kuwa mfanyakishara mkubwa katika nchi ya Malaysia. Lakini ukisikia historia yake alivyoanza alisaidiwa sana na Serikali yake, alianza kwenye utafiti mdogo akarudi baadaye kuwa mfanyakishara, leo amekuwa akisikika ulimwengu mzima kwa sababu tu ya kile alichoanza nacho kidogo na akapewa *support* kubwa sana na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Kamati imefanya kazi nzuri sana. Naipongeza Serikali imetuletea Azimio hili wakati muafaka. Naomba baada ya kuridhia basi sasa tutengeneze mikakati ya ndani ya kuona namna gani haya tunayoridhia yaendane na mipango mizuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, yaendane na sera nzuri za Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, kwa manufaa ya Watanzania na hivyo maendeleo endelevu na umaskini wetu utapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima tena naomba niseme naunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia moja na naiombea kheri Serikali yetu itekeleze Azimio hili kwa nia njema kama ilivyolileta kwa nia njema ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama. Kama nilivyosema mwanzo sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa. Mheshimiwa Mohamed Mnyaa atakuwa anachangia hoja ilivoletwa mbele yetu na Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kuchangia Azimio hili. La kwanza, niiombe radhi Kamati yangu kwamba siku walivokutana mimi sikuwepo, kwa hivo,

hawakuweza kupata *input* yangu lakini nitatumia *forum* hii leo kuweka *input* yangu na naomba Bunge lifikirie makini mambo nitakayoyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwamba nitoe angalizo kuwa hizi *Protocols* nyingi sana kwa kawaida kuanzia *Head of States* wanaposaini mpaka kuptishwa hapa katika Bunge, kuwa-*ratified* inachukua miaka mingi wakati mwingine miaka mitatu, minne, mitano, sita au saba. Kusema kweli hapo pana jambo, ina maana zile *States* zinatazama undani kuna tatizo gani na je, watafaidika hizo nchi na itifaki hizo, ndio sababu zinachukua miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika angalizo hilo naomba baada ya hizi Protokoli kuwa *signed*, Bunge lako Tukufu lisivamiwe mara kwa mara kupewa itifaki hizo siku hiyo hiyo kabla Wabunge hawajapata nafasi ya kuzipitia na wakachambua kwa undani wakaona mna kitu gani katika Itifaki hizi. Hili ni tatizo katika dakika kumi hizi walizopata Waheshimiwa Wabunge ziliposambazwa humu Bungeni hawawezi kuwajua kuna nini ndani ya itifaki hii. Ni Serikali tu tangu waliposaini wanajua lakini Wabunge hawajui na haiwezi kufanya kazi itifaki hii mpaka tupitishe Azimio hapa Bungeni ili kuweza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya angalizo hilo naomba niisifu Tanzania sasa kwa ku-*ratify* itifaki nyingi katika *SADC*. Mpaka sasa hivi katika *Protocol 35* zilizotolewa na *SADC* Tanzania imesha-*ratify* 23. Afrika ya Kusini 22, kwa hivyo Tanzania tumesha-*ratify* 23 na leo tukipitisha Azimio hili itakuwa tumesha-*ratify* 24 na zitabakia 11. Afrika ya Kusini wame-*ratify* 22 bado 13. Mozambique 22 bado 13, Namibia nao wao 23 bado 11. Zimbabwe wame-*ratify* 15 tu bado 20. Angola wame-*ratify* 9 tu bado 26 na kadhalika, naweza kuzitaja ziko nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi ningependa tujue ni kwa nini wengine wanar-*ratify* haraka na kwa wingi na wengine tunachelewa au wanachelewa na kwa nini Tanzania tujipeleke haraka haraka ku-*ratify* kila Azimio, ni kwamba tunahitaji wakati. Nitolee mfano, katika *SADC Protocol Trekker* ambayo nakala yake ninayo hapa na moja katika *Protocol* muhimu ambayo ya *Gender and Development*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yako na Bunge hili, ni nchi mbili tu zilizosaini na ku-*ratify* ambayo ni Tanzania na Zimbabwe. Nchi mbili ambazo zimekataa hata kusaini ambaao ni Botswana na Mauritius na zilizobakia zote nchi hizi hazija-*ratify* ambayo kwa sisi Tanzania tunaona masuala ya *Gender Development* ni masuala muhimu lakini angalieni wenzetu namna gani walivyopiga stop kwanza ku-*ratify* Maazimio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya angalizo hizo na hili la mwanzo naomba sasa niingie katika Azimio lenyewe. Katika Azimio lenyewe Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba kuna nchi tano ambazo tayari zimeshapitisha Azimio hili ambayo ni Afrika Kusini, Mozambique, Botswana, Malawi na Zambia. Lakini narudia tena, katika *SADC* wenyewe *SADC-NGO* ambaao kuna *document* wametoa hii wanaita *SADC Protocol Trekker* ambaao wamefuatilia nchi zilizosaini, zilizo-*ratify* na kadhalika mpaka sasa hivi ni nchi mbili tu katika hii *Protocol* ya *Science, Technology and Innovation* ambazo

zimesaini au zilizo-*ratify* ambazo ni Mozambique ambayo ilisaini tarehe 23 Machi, 2009 na Mauritius tarehe 13 Juni, 2009 na nchi mbili zimekataa katakata hata kusaini ambayo ni Malawi na Seychelles. Kwa maana hiyo, hiyo ndio hali halisi mpaka Desemba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningewomba katika *stage* hii Mheshimiwa Waziri atuambie katika hii *development* ya miezi mitatu inawezekana kweli ziko nchi nyingine zimesha-*ratify* sasa atupatie uthibitisho wa hizo nchi tatu nyingine ambazo kama zime-*ratify* katika kipindi hiki cha karibuni ambapo uwezekano huo mkubwa upo, lakini mpaka sasa hivi katika rekodi zilizopo ni nchi mbili tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nichangie katika Azimio hili ni katika ibara ya 2(a) ya hiyo *Protocol* yenye ambayo inazungumzia kufuta au kuondoa vikwazo vya mzunguko wa Wanasyansi na *technologists* ndani ya wanachama wa SADC kwa madhumuni ya elimu, utafiti na ushirikiano katika programu ya *STI*. Hii lazima tuwe waangalifu sana. Hii *article* ukiiangalia kwa undani inaendana na *Protocol* nyingine ambayo *Protocol* hiyo inahusiana na 2005 ya *facilitation of movement of persons* ambayo hiyo mpaka sasa hivi Tanzania hatuja-*ratify*, hatujapitisha Azimio hilo, *Facilitation movement* katika nchi za SADC Tanzania bado hatujapitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tutakopopitisha Azimio hili la *Science and Technology* katika ibara hii ina maana sasa tunaruhusu ile *movement*, kwa hapa inazungumzia *movement* ya Wanasyansi na *Technologists* kuwe na *movement* katika kueneza elimu na utafiti wa mambo haya wanayohusika. Lakini sasa pia tuwe waangalifu katika *Protocol* ya *movement of people*, Tanzania hatujasaini, tunasaini katika *Protocol* hii ya *Science, Technology and Innovation* ambayo tukisaini hii kwa mujibu wa Article 2(n) ina maana sasa ile *movement of people* itakuwepo ingawaje hapa wanazungumzwa Wanasyansi na Watafiti wengine, lakini tuna uhakika gani sasa hiyo *movement of people* hawawezi wakajiingiza na watu wengine ambao hawahusiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ningependa tuwe na angalizo na tuwe waangalifu wakubwa tusiwe na haraka kuitisha Azimio ikawa kwa nchi ni matatizo. Wakati Tanzania ikitafakari kwa nini hawajapitisha Azimio la *Facilitation of Movement of Person*, leo tunakuja kuitisha Azimio la Sayansi halafu wakati huo huo kimo kipengele cha *Movement of People* kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tutakoporidhia hili Azimio linaloruhusu *Movement* ya hao tunaowaita Wanasyansi na Wanateknolojia kwa shughuli za utafiti, je, *movement* zao zitakuwa *controlled* namna gani? Tumeshajipanga? Ina maana ni mambo ambayo kwanza tujitayarische kabla ya kuitisha Azimio hili. Tujitayarische nayo kwa sababu wanaweza wakaja Wanasyansi wengi sana na Wanasyansi watakaokuja tunajua ni namna gani tuna tofauti. Nchi ya mwanzo inawenza kufaidika hapa ni nchi ya Afrika ya Kusini. Afrika ya Kusini *level* yao ya kielimu na *level* yetu tunatofautiana sana. Watu wanaweza wakaja wakafanya tafiti ndani ya nchi yetu, wakafanya madudu ambayo sisi hatuoni kwa sababu ya upeo wa macho yetu. Inawezekana yakafanyika mambo chungu nzima tusijue, ikawa kama unavyochukuliwa

mchanga na mambo mengine sisi hatuoni, halafu tutabakia hapa kumbe tunaharibiwa rasilimali zetu, ikawa kwa njia hii ya utafiti kumbe watu wanafanya mambo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, inafaa na sisi tujipange kwanza, tusivamie haya mambo, tuje tunafanya nini na tutazame sababu za wenzetu kwa nini wasi-*ratify* haraka. Tunapenda na sisi kuelimika, tunapenda na sisi tuwe katika hali nzuri ya kisayansi na kiteknolojia na ndiyo sababu nzuri sana ya maendeleo. Lakini maendeleo yote yana hasara zake na kama hukuwa mwangalifu kuna matatizo makubwa. Napenda angalizo hilo litazamwe vizuri na mimi sitokuwa rahisi sana kupitisha Azimio hili ikiwa Mheshimiwa Waziri hajatoa sababu za msingi katika mada zote hizo ambazo nimezitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *Article 4(l)* na (p), *Article* ya 4(p) ya itifaki hii ambayo inazungumzia kuongeza juhudzi za kufikia angalau asilimia moja ya *GDP* katika matumizi ya utafiti wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia. Ni kweli Mheshimiwa Waziri alitureleza katika Kamati kwamba Serikali imekubali kuongeza fedha katika mambo haya, lakini je, tutatimiza asilimia moja ya *GDP* yetu, hicho kiwango atakachopata atatuhakikisha Wizara yake itapata hizo fedha? Kwa sababu tunajua hivi sasa bado ni tegemezi na shughuli zote za Sayansi na Teknolojia hivi sasa kwa mipango iliyopo tunaitegemea Serikali ya Sweden. Je, hii *one percent* na hiki ni kifungu cha itifaki yenyewe kwamba ni sharti la kutimiza, je, Tanzania kweli itaweza kutoa kila mwaka wa bajeti *at least* kiwango ambacho kitafikia asilimia moja ya *GDP*. Ni suala la kujiuliza kabla ya kuvamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *Article 2 (n), (o)* na (p) ya itifaki hii ambayo inazungumzia kuongeza njia za kufikia za kufundisha na kujifunza *Basic Science* na Hisabati katika ngazi zote za elimu. Hiki kifungu kinazungumzia katika kukuza au kupata Wanasyansi na wanataluma mbalimbali katika mambo haya ya teknolojia na kwa maana hiyo kifungu hiki kinazungumzia kwamba tutafute njia ya kuongezea njia za kufundishia. Hivi sasa unaelewa vizuri katika nchi yetu tofauti kubwa tuliyonayo. Kwa sababu tunapozungumza masuala haya sisi tuko tayari lakini inapokuwa tofauti kubwa baina ya nchi wanachama wa *SADC* zinazo-*ratify* itifaki hii, halafu tukawa nao ni nani atafaidika mwanzo vizuri, je, masharti ni yepi, wako tayari wao katika ushirikiano huu wa kutusaidia, tunaelewa matatizo ya elimu hasa sayansi na *mathematics* ndani ni makubwa mno na hakuna asiyefahamu.

Mheshimiwa Waziri atueleze je, ina maana nchi za *SADC* ambao wameridhia itifaki hii na wao watakuwa tayari kutuletea walimu wa sayansi, *mathematics* na kadhalika ili na sisi angalau tunyanyuke katika masomo hayo, tufikie *level* walizonazo wao. Kwa sababu kitendo hicho cha kuridhia tu kiendane na mikataba yenyewe. Humu ndani katika itifaki yenyewe hakijaeleza namna gani tutasaidiana. Wanasema tu ushirikiano, lakini waseme ushirikiano uwe wa namna gani. Sasa kama Mheshimiwa Waziri atatufafanulia ushirikiano wa namna gani hapo tunaweza tukasema hili ni jambo zuri. Kwa maana hiyo ni lazima tuwe waangalifu katika suala hili na kuna *article* ambayo inazungumzia hawa *African Diaspora*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile angalizo lingine ni *African Diaspora*, tukipitisha Azimio hili inahitajika katika hicho kifungu cha itifaki hii kinachozungumzia ushirikiano na *African Diaspora*. Tunaelewa vizuri sijui tutashirikiana vipi wakati hivi sasa nchi yetu Tanzania imekimbiwa na wataalam wengi sana wa afya, Madaktari wengi sana wako Botswana, Afrika ya Kusini, Wahandisi wengi sana wako Ulaya, Marekani, sisi tutashirikiana nao vipi ikiwa kwanza hatujitayarisha, hao *African Diaspora* watakuwa tayari vipi kushirikiana nao na kutusaidia sisi ikiwa mazingira ya nchi yetu hivi sasa sio mazuri ya kuwafanya watu hao wavutike na kuwepo hapa badala yake wanaondoka wanakimbilia hizo nchi za wenzetu. Halafu leo tunataka kupitisha Azimio bila ya kujitayarisha na hayo.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hiyo ni kengele ya kwanza?

**WABUNGE FULANI:** Ya pili.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Haya basi kama ni kengele ya pili. Nashukuru kwa mchango wangu na naomba Bunge hili lifikirie kwa makini kupitisha Azimio hili kutokana na sababu hizo za msingi nilizozitoa na ikiwa kutahitajika *details zingine* kuhusu hiyo *SADC Protocol Trekker* ninayo na nitakuwa tayari kulipa Bunge lako hili Tukufu. Ahsante sana nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Mnyaa kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa. Sasa Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed akifuatiwa na Mheshimiwa Regia Mtema. Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika kuridhia Azimio hili. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako hili Tukufu kuchangia hoja, naomba kwanza nitoe shukrani kwa wananchi na wapiga kura wote ambaa wamenichagua kutoka katika Jimbo la Ole lililoko Kaskazini ya Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nikupongeze wewe binafsi na naomba nimpongeze Waziri na Serikali kwa ujumla lakini bila kusahau na Kamati ambayo imeweza kuwasilisha mapendekezo haya na vilevile na maoni ambayo yametoka kutoka kwa wachangiaji waliopita. Lengo na madhumuni ya Azimio hili yanaonekana ni mazuri, yenye manufaa na ambayo yanaweza kukwamua uchumi wa nchi yetu hapa ulipo na kwenda mbele zaidi. Nataka kusema kwamba, nchi yoyote duniani kama inahitaji au ina udhati wa kweli katika kuwaondolea matatizo ya uchumi mgumu wa wananchi wake basi ni lazima iangalie kwa mapana zaidi sekta hii ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Waziri ametueleza, Kamati imeeleza, tumeridhika na maeleo mazuri na malengo mazuri nawaomba na nawashauri Wabunge wenzangu tuweze kuunga mkono hoja hii ili Serikali iweze kuingia na kushirikiana na

nchi hizi kwa kupitia *SADC* kuweza kuimarisha taaluma nzima ya sayansi na teknolojia na utafiti. Wahenga walizungumza na bado wanaendelea kuzungumza kwamba, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niingie katika vipengele vya Azimio hili. *Article 2, Objectives, item (e)*, “*optimise public and private investment in research and development with a region leverage external contributors*”. Hiki kipengele ni kizuri na kinatoa mwelekeo mzuri lakini napata mashaka kidogo na inabidi Wizara iwe na uangalifu mkubwa wa hali ya juu. Katika Wizara hii ya Sayansi na Teknolojia kuna kitengo cha *COSTECH* iko Tume hii. Hii Tume kwa mujibu wa ripoti ya Waziri inafanya kazi vizuri sana katika suala zima la sayansi na teknolojia. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba tutakapokuja kuridhia Azimio hili tusije tukajisahau. Tukaja tukaicha *COSTECH* tukaanza kuangalia hii *Block* kwa madhumuni tu kwamba tunakwenda kwa sababu ya umoja wetu wa *SADC*. Naomba kwanza hiki cha kwetu tuhakikishe kwamba nacho tunakiendezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Serikali ya Sweden imeweza kuisaidia *COSTECH* Bilioni 4.8 kwa ajili ya utafiti wa sayansi katika kipindi cha 2009-2013 na kama nilivyosema katika *Article* hii lengo lao moja hawa ni: “*...and leverage external contributors*”. Sasa tusije tukaacha mbachao wetu kwa mswala unaopita. *COSTECH* wamefika pazuri na wanaendelea pazuri. Lakini vilevile *COSTECH* hii hii ilianza kwa shilingi milioni 53 mwaka 1990, sasa hivi imeweza kuongeza mtaji au mapato yake na maingizo ambayo yanafikia bilioni nne kwa mwaka 2009/2010. Sasa hii ni dhahiri inaonesha namna gani *COSTECH* wanavyofanya kazi vizuri. Natoa angalizo tena tusije tukaacha mbachao wetu kwa mswala unaopita, tukaja tukajisahau tukaona kwamba hii *Block* itatusaidia zaidi hili la kwetu tukaweza kulidharau. Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kipengele *item number 4(e)*. Mheshimiwa Mnyaa alikidasia hiki na mimi kidogo nikitolee angalizo zaidi. *Areas of cooperation*, maeneo yale ya ushirikiano, kinasema: “*Forging strong partnership with African Diaspora with a view to advancing the scientific and technologist, technology development of the region.*” Sawa tunakubali lakini sasa hii *African Diaspora* hebu tuiangalie kwa upana wake. Tutazame ilikuwaje hii ikatokea, hawa ni wataalam ambaa kil mmoja ana fani yake. Lakini tatizo la hawa hasa katika nchi yetu ya Tanzania ni kwamba hawa wataalam tuliwadharau. Serikali ilikuwa haiwalipi malipo mazuri, ilikuwa haiwatunzi, haiwajali. Sasa wakaona bora wengi wao waanze kutafuta maeneo mengine ya kuweza kwenda kutafuta maslahi yaliyo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba hawa ambaa tunao tuweze kuwadhibiti na tuweze kuwa nao, tuwape maslahi mazuri ili tuweze kuwatumia. Kuna mfano mkubwa, wako wengi hawa, kwa mfano, nchi za Marekani, nchi za Ulaya au kwa mfano mwingine Sweden kuna Dr. Masley Nzota, huyu ni Mtaalam wa Upembuzi wa Vyama, ni Mtanzania, sasa hivi yuko Sweden anaendesha nchi ya Sweden katika masuala haya. Tulimwacha, tukambeza wenzetu wakamchukua. Sasa hapa lazima tuwe makini katika hili.

Mheshimiwa Niibu Spika, lakini vilevile tuwe na tahadhari kubwa kwa sababu kuna kipengele ambacho kinasema au kinazungumzia huu mwenendo wa hawa wanasayansi. Tusije tukajikuta kwamba hawa wanasayansi ambao wanakimbilia katika nchi hizi hizi za SADC ambazo nazo huenda au ambazo zimesharidhia. Baada ya kutumika hapa kwetu, kwa kutumia kipengele hiki wakaenda kutumika nchi nyingine japokuwa kwamba tutakuwa katika *block*, lakini ile faida na mantiki haswa ambayo tunaikusudia kama sisi hapa tutakuwa tumeikosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende Article 6, inasema: “*Financially provision. Item (i) Member states shall insure allocation of the financial resources in their budget for the implementation of this protocol in their respective states.*” Hapa napata wasiwasi. Wasiwasi ninaoupata ni kwamba, bajeti zetu bado zinasuasua. Tutakubali kuridhia na Serikali itasaini lakini naiomba Serikali iwe na dhamira ya dhati katika hili. Tusiwe weledi wa kusaini *protocol* hizi wakati utekelezaji ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kutoa mfano, katika hili Wizara hii katika Bajeti ya mwaka 2010/2011, ilipangiwa shilingi bilioni 11.3, hiyo ndiyo fedha ambayo Wizara ilitengewa. Lakini la ajabu ni kwamba hadi kufikia Januari 2011, Wizara hii kwa mujibu wa ripoti ya Waziri ambayo aliiwasilisha katika Kamati ya Miundombinu, Wizara ilishapokea bilioni 4.4 tu. Sasa hiki kipengele kinazungumzia suala la *members ku-insure allocation financially resources in their budget*. Sasa hapa napo inabidi Serikali ipaangalie kwa uangalifu mkubwa na Wizara inabidi yenye ikubali kuchukua hatua za makusudi kuibana Serikali japo kuwa yenye ni Serikali ili kuhakikisha inakwenda sambamba na hiki kipengele ambacho tutakiridhia. Bila ya hivyo itakuwa mmeliambia uongo Bunge zima na hamtoliambia uongo kwa wananchi tu Watanzania bali itakuwa mmesema uongo katika Jumuiya za Kimataifa. Kwa hiyo, lazima bajeti hii iwe sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofit*)

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kueleza kwamba nami ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu na kwa kuona muhimu wa Azimio lililoko mbele yetu kwa kuwa Wizara ililetta taarifa yake au pendekezo lake kwenye Kamati yetu tukajiridhisha na kuipitia na kwa kuona umuhimu wa Azimio hili ambalo lina faida kubwa kwa Taifa la Tanzania naomba niunge mkono hoja kwa kupitisha Azimio hili. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala moja ambalo ningependa Wizara au kama Taifa tuweze kulitilia mkazo tunapopitisha Azimio letu siku ya leo. Kwamba mojawapo ya maeneo ya ushirikiano ambayo Azimio linasema ni pamoja na *promotion of gender equity and access to science, technology and innovation* kitu ambacho kimenifanya niunge mkono hoja hii kwa kuwa natambua kabisa suala hili ni nyeti na lina umuhimu mkubwa kwa makundi yaliyoko pembezoni ili kuweza kuwa na *access* ya kupata elimu inayohusiana na sayansi, teknolojia na ubunifu. Kwa kutambua ushirikiano wetu wa nyuma na SADC ambako walitilia mkazo kuongeza idadi ya wanawake kwenye vyombo vyaya maamuzi na leo hii tunaona kabisa angalau Tanzania tumejkwamua, idadi

ya wanawake imeongezeka kuanzia kwenye Bunge, kwenye vyombo vingine mbalimbali kwa mfano, wanawake wengi leo hii ni Majaji. Vilevile hata kwenye maofisi mbalimbali idadi ya wanawake imeongezeka kutokana na ushirikiano wetu na Jumuiya hii ya *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa pia Azimio hili linaonekana kwamba nchi ambazo zitaridhia Azimio hili tutafaidika na kundi la wanawake kuweza kupata elimu ya sayansi, teknolojia na ubunifu, basi nilikuwa ninasisitiza kwamba mara nyingi wanawake walioko pembezoni wamekuwa wakisahaulika na sote tunatambua kule vijiji ni suala zima la sayansi. teknolojia na ubunifu liko nyuma sana basi ni wakati sasa Wizara kutilia mkazo tutakapokwenda kufaidika na Azimio hili katika umoja wetu katika Jumuiya ya *SADC*, basi maeneo ya vipaumbele yawe ni vijiji ni.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii sote tunatambua kabisa kwamba wanawake au wanafunzi ambao wanasona masomo ya sayansi ni wachache, ndiyo maana tuna Wahandisi wachache, Madaktari wachache wanawake na Marubani na maeneo mengine ambayo yanahusika moja kwa moja na sayansi na teknolojia, basi inasisitiza kwamba Wizara ione umuhimu wa kuhamasisha na kupeleka bajeti kubwa kwa ajili ya kuweza kuhakikisha kwamba wanawake walioko pembezo na wanafunzi wanaosoma sayansi waweze kupewa vipaumbele wanapoingia Chuo Kikuu na hatimaye waweze kuwa kwa wingi kwenye kupata elimu ya juu na vilevile kwenye maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo tunapozungumzia *gender* au tunapozungumzia jinsia hatuzungumzii wanawake au wanaume peke yao lakini tunazungumzia vilevile jamii ya watu wenyе ulemavu. Nikiwa kama Mbunge mwenye ulemavu ambaye ninaathirika moja kwa moja na masuala mazima ya sayansi na teknolojia basi naiomba Wizara leo tukiwa tunaridhia *protocol* hii iweke mkazo kwenye jamii ya watu wenyе ulemavu ili tuweze ku-access elimu ya sayansi na teknolojia. Leo hii sote tunatambua kabisa kwamba nchini kwetu kumekuwa na tatizo la miundombinu mbalimbali inayowakumba watu wenyе ulemavu. Kwa mfano, kupata kujifunza lugha ya alama ili kuendana sambamba na wenzetu viziwi imekuwa ni changamoto katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hata maandishi ya nukta nundu, naamanisha *brail* kwa wenzetu wasioona imekuwa ni changamoto. Kwa hiyo, ninapoona sasa nchi yetu inaridhia *protocol* hii ya *SADC* naamini kwamba jamii ya watu wenyе ulemavu tutakwenda kufaidika na kuweza ku-access elimu hii ambayo unapatikana kwenye Vyuo Vikuu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo niliyoyazungumza ya kukumbuka jamii ya watu wenyе ulemavu ambao tunaathirika na teknolojia, lakini naamini vilevile Wizara yako itatilia hata kwenye masuala ya upitikaji. Leo hii tunaona hata ndani ya Bunge imekuwa ni tatizo kwa sisi watu wenyе ulemavu kuweza kufika kule juu kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge tunapata shida, hakuna *lift* na ngazi zenyewe ni taabu na maeneo mengine vilevile ya Serikali ambayo ni *public* imekuwa ni tatizo ambalo linafanana na hapa. Kwa hiyo, naamini sasa ni wakati muafaka wa Serikali yetu kuridhia *protocol* hii ili na jamii ya watu wenyе ulemavu tuweze kupata *access* katika elimu ya

sayansi, teknolojia pamoja na ubunifu na hatimaye tuweze kufanya mambo ya msingi ambayo yatasaidia jamii yetu ya Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo machache, naunga mkono hoja ili tuweze kuridhia Azimio letu. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Azimio la Itifaki ya Sayansi na Teknolojia ya *SADC*. Niseme tu kwamba Azimio hili ni la muhimu kwa Taifa letu na linagusa maisha ya wananchi wa Jimbo ambao wamenituma kuja kuwawakilisha, Jimbo ambalo lina vyuo mbalimbali vinavyoguswa na masuala haya ya sayansi na teknolojia. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Maji na Chuo cha Usafirishaji Mabibo, Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbezi na Vyuo vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inagusa vile vile maisha ya Watanzania wenyе vipaji mbalimbali ambao wanataka kunufaika kutokana na vipaji vyao. Lakini, pamoja na umuhimu wa Azimio hili kwa hoja ambazo nimezieleza kwenye utangulizi, yapo mambo ambayo ningependa kuyachangia. Niseme vile vile kwamba naunga mkono na kupongeza Kambi ya Upinzani kwa hotuba waliyoitoa na naungana vile vile na Kamati ambayo imewasilisha taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mheshimiwa Mnyaa na nimpongeze kwa kweli, yeye amekuwa Mbunge wetu kwenye Bunge la *SADC*. Mambo mawili aliyozungumza yanahitaji Serikali iyatolee majibu ya kina kwa sababu hoja aliyozungumza kuhusiana na idadi ya nchi ambazo zimesaini Azimio hili, nchi ambazo hazikusaini na nchi ambazo hazikuridhia, ni hoja ambayo, kama taarifa iko kama alivyozungumza mpaka hivi sasa, kama haijabadilika katika miezi mitatu iliyopita, tafsiri yake ni kwamba Serikali inapaswa kubadili Sehemu ya *Tatu* ya Azimio hili linalotaja nchi na *status* ya kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inanirejesha kwenye hoja ambayo niliizungumza kwenye mchango wangu wakati tunachangia hoja ya Azimio la *UNESCO*. Bunge letu Tukufu, nitoe tahadhari tu, kama litendelea kutumia mfumo huu kuridhia Maazimio ya Kimataifa, kuna mashaka kwamba tunaweza kugeuka kuwa *rubber stamp*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoa tahadhari wakati tunajadili Azimio la *UNESCO* kwamba kwa mamlaka tuliyopewa na Katiba, kama tunaridhia Azimio, ni lazima Azimio tunaloletewa liwe na *signature*. Nashukuru Azimio la leo lina *Signature* ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliyoysaini mwaka 2008. Lakini, kuwe vile vile na *Instruments* za nchi ambazo zimefanya *ratification* ili sisi tunapojadili tuweze kurejea. Kwa mujibu wa Azimio tunalolijadili hivi sasa, Azimio lenyewe lime-*provide* Kifungu cha 18 cha Azimio kinasema kuhusu *depositing*, kwamba nchi zilizoridhia, zinasema baada ya nchi kuridhia hili Azimio, wakisha-*deposit* hizo *Instruments* kwa *Executive Secretary*, yule Katibu Mtendaji wa *SADC* anatakiwa asambaze kwa *Member States Certified Copies* (zile copy ambazo zimeidhinishwa) za hati za nchi ambazo zimeridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitarajia na pengine hili liwe hitaji kwenye mikataba inayofuata tunayoletewa, tukiletewa mkataba tuletewe vile vile viambatanisho vyenye *Instruments za Ratification* kwa sababu kuna mambo ya ziada yanayokuwemo mle ambayo ni muhimu kama Wabunge wakati tunajadili kuridhia Azimio tuweze kuyafahamu kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijarejea kwenye vifungu vingine, niseme suala la pili kuhusiana na utaratibu tunaotumia wa kuridhia Maazimio mbalimbali. Azimio hili limesainiwa na Rais wetu mwaka 2008, sisi tunaliridhia leo mwaka 2011. Ni vizuri Kanuni zetu na utaratibu wetu wa kuletewa Maazimio haya ukaboreshwali ili Rais anaposaini ama kiongozi mwingine yejote wa Kiserikali mwenye mamlaka ya kusaini kwa niaba ya nchi yetu, anaposaini mikataba hii ya Kimataifa, akirejea ndani ya nchi, Bunge linalofuata, hata kama hatujadili hilo Azimio, tuletewe hilo Azimio kama hati zinazowekwa mezani na Serikali, kwamba Serikali yetu katika kipindi kilichopita tulikwenda nchi hii na tumesaini Azimio hili, tunaleta kama hati ya Serikali ili Wabunge wawe na muda wa kutosha wa kutafakari. Maana yake hili lingepatikana Bungeni toka mwaka 2008, lingetafakariwa, leo tungkuja hapa tukiwa tayari tumekwishafanya *consultation* ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri katika hili suala la *movement* ya watu, kama Tanzania haikusaini Itifaki inayozungumzwa ya kuhusiana na *movement* ya watu, ningeomba Mheshimiwa Waziri afanye marekebisho kwenye Azimio hili, a-*insert* kifungu cha 10 ili kifungu cha 10 kisomeke kuwa kifungu cha 11. A-*insert* kifungu cha 10 ambacho kitamke wazi kwamba kwa kuwa Serikali yetu bado iko katika hatua ya kuridhia Azimio *so and so*, alitaje hilo Azimio na iendelee kwamba ili aweze kuweka mipaka ya utekelezaji wa kifungu cha 2(1) cha Azimio tunaloridhia leo ili utata ambao anauzungumza Mheshimiwa Mnyaa uondoke, tuweze kuliridhia Azimio, lakini turidhie tukiwa na angalizo hapa liweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia sana hili Azimio, sioni matatizo makubwa ya kisheria ya kifungu 2(l) kama tutaridhia kwa sababu tu kiko kwenye upande wa malengo (*objectives*) na kimesema: “*Moving towards elimination...*” ya hiyo, yaani kuelekea kuondoa hiyo mipaka. Halijasema moja kwa moja kwamba tukishasaini hili Azimio, tunafunga mipaka. Lakini pamoja na hayo maelezo niliyoyatoa, bado kuna haja ya kuwa na *clause* maalum kwenye Azimio letu kwa ajili ya kutimiza matakwa haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi kwenye masuala ya ujumla. Mimi binafsi naunga mkono kuridhiwa kwa Azimio hili pamoja na hayo maangalizo niliyoyatoa ambayo ni muhimu yakazingatiwa kwenye Azimio. Lakini, wajumbe wetu watakaokwenda kutuwakilisha baada ya kuridhiwa kwa Azimio hili, maana kuna vyombo vinaundwa, watakaokwenda kutuwakilisha, wakifika kule, lazima wa-*move* hoja kadhaa za *amendment* kwa kutumia *Article* 12 ya Azimio lenyewe tunalolipitisha leo. Nasema hivyo kwa sababu, ukienda kwenye *Article* ya 4, Ibara ya 4 au Kifungu cha 4 cha Azimio tunalolipitisha leo, kipengele cha (k) kinachozungumzia *commitment* ya kutenga asilimia moja ya Pato la Taifa kwa ajili ya masuala ya utafiti. Kifungu hiki kinasomeka na

nitaomba nikisome: “*Intensification of efforts to attain at least one percent of Gross Domestic Product (GDP) expenditure on research on development by 2010.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, sijajua mantiki ya waliosaini hili Azimio, wakalisaini 2008 na Azimio likasema kwamba hii ilipaswa kutekelezwa kuitia Azimio lenyewe ifikapo 2010. 2010 imekwishapita, sasa ni 2011, Tanzania hatujatimiza hiki kigezo. Ni vizuri *amendment* ikafanyika kwenye kifungu hiki na naamini kuna nchi nyingine hazijatimiza hili. *Amendment* ikafanyika kwenye hiki kifungu ili kukawa na muda wa ziada wa utekelezaji. Kuna kasoro nyingi sana kwenye hili Azimio lenyewe, lakini kwa kuwa Bunge hili haliwezi kuligeuza Azimio hili, nitoe wito tu kwa watu wetu watakaokwenda kutuwakilisha baada ya kuunda hivi vyombo. Jambo la kwanza ambalo waende nalo ni kufanya *amendment* na sisi Wabunge tuko tayari na mimi binafsi niko tayari kuchangia ni maeneo gani ambayo wakienda kule kutuwakilisha wahakikishe kwamba yanafanyiwa marekebisho ili Azimio hili liweze kuwa na tija ile inayokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa napo kuna haja ya kufanyika marekebisho kidogo. Serikali imesema kwamba Azimio hili halitatuingiza, nasoma kipengele cha (9) cha Azimio lenyewe: “Kwa kuwa hakutakuwepo na gharama yoyote katika kuridhia Itifaki zaidi ya michango ya kawaida ya kila mwaka ya Serikali”. Hili Azimio nalo linapaswa lirkebishe lugha kwa maana ya kwamba hakutakuwepo na gharama yoyote. Mtu akija kuangalia utekelezaji anaweza akadhani kweli kwamba hakutakuwepo na gharama yoyote, lakini ukiangalia kwenye Azimio lenyewe tunalokwenda kuliridhia, kuna gharama za aina mbili tutakazoingia ukiondoa michango tutakayolipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kwanza ipo kwenye *Article* ya 5, hizi taasisi zitakazoundwa na Azimio hili tunaloliunda, kuna vyombo viwili hapa ambavyo vitatugusa moja kwa moja, cha kwanza ni *Inter-Ministerial Technical Committee (Sectorial Committee)* hii Kamati ya Mawaziri. Pili, ni Kamati ya Maafisa Wakuu (*Committee of Senior Officers*). Hizi kamati zote ni *organs*, zitakuwa na vikao, zitakuwa na taratibu ambazo kwa vyovypote vile lazima kwenye Bajeti ya Serikali tutakuja kuingiza gharama za ushiriki wetu na taratibu zetu kwenye hivi vikao husika. Kwa hiyo, kuliacha hili Azimio kusomeka tu moja kwa moja kwamba ukiondoa mchango utakaolipa, hatutaingia gharama zozote inaweza kuwa na mashaka kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri kukawa na *qualification*, kukawekwa neno ambalo litaonyesha kwamba hakuna gharama zingine tutakazolipia kule, lakini ibaki ionekane kwamba kuna gharama tutakazoingia ingawaje siyo gharama kubwa. Na nitoe wito tu kwa Serikali, katika utekelezaji wa Azimio hili, sina tatizo na Mawaziri kwenda kutuwakilisha ama Waziri husika kutuwakilishi kwenye *Sectorial Ministerial Committee* ya Sayansi na Teknolojia. Lakini, itakapokuja *Committee of Senior Officers*, ni vizuri sana pamoja na kuwa *Seniority* kule kwenye Wizara, najua Katibu Mkuu ndiye *Senior Officer* ukiondoa Waziri, ni vizuri katika masuala haya ya Sayansi na Teknolojia, kwenye hii *Committee* ya *Senior Officers*, Tanzania ikaenda kuwakilishwa na watu kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) ili kweli wakaenda kufanya kazi ya kitalaam na wakaisaidia nchi katika masuala ya kitalaam. Kwa hiyo, hili nilitaka nitoe kama angalizo wakati wa utekelezaji wa Mkataba husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba upitishwaji wa hili Azimio, ni vizuri ukaenda sambamba na Taifa letu kuongeza nguvu za ziada katika kutumia vyuo vyetu. Wengi wamezungumza kuhusu faida inayotokana na ubadilishanaji wa maarifa, taarifa ya Sayansi na Teknolojia na masuala kama hayo, kutokana na Azimio hili. Lakini, kuna changamoto moja naiona ambayo ni muhimu Serikali ikaishughulikia. Mara nyingi Serikali ambaye ndiye mtumiaji mkubwa wa pesa kwa sababu Serikali ina bajeti, inafanya manunuizi, inafanya vitu mbalimbali, inapotaka kufanya manunuizi, wakati mwingine inakwenda kununua nje vitu ambavyo vingeweza kupatikana kwa wazalishaji wa ndani kutoka kwenye vyuo vyetu na taasisi zetu. Au wakati mwingine inatumia utaalam wa pembeni wakati ingetumia utalaam wa vyuo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitolee mfano tu, sasa hivi *EWURA*, wana utaratibu wa kuweka vinasaba kwenye mafuta kuzuia uchakachuaji na kuzuia *dumping* ya mafuta ambayo yanakwenda nchi zingine vile vile. Vinasaba vinavyowekwa na *EWURA*, kampuni iliyopewa kazi ya vinasaba, imepewa kampuni ya nje. Lakini, ukiangalia jambo lenyewe linalofanyika, maabara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Watalaam wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wangeweza kupata na tungeweza kuwajengea uwezo, tungepata tija ya maana sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa hilo kama mfano tu, lakini yako maeneo mengi ambayo kama Taifa kama tunataka kukuza Sayansi na Teknolojia, lazima vile vile Serikali haswa, kabla hata ya watu binafsi, Serikali haswa, ifanye maamuzi ya dhati kwamba masuala yote yanayohusu teknolojia, sayansi, ubunifu tunakwenda kutafuta nje kama tu ndani ya vyuo vyetu, ndani ya taasisi zetu hakuna *option* nyingine, ndipo ambapo tunaweza kufanya huo ubadilishanaji na mambo mengine kama ambavyo nimeeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie hili la *Diaspora* ambalo limetajwa kwenye kifungu cha (4) cha Azimio hili lililoko hapa mbele yetu. Naungana na rai iliyomo kwenye hili Azimio na maudhui ya Azimio. Sasa, tukilipitisha hili Azimio leo na naamini tutalipitisha na mimi binafsi naunga mkono pamoja na maangalizo yote hayo, naunga mkono tulipitishe Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukilipitisha hili Azimio, ni vizuri Wizara ya Mambo ya Nje, pamoja na kuwa siyo ya Sayansi na Teknolojia, lakini kwa kuwa yenye ndiyo ina Idara ya *Diaspora*, ndani ya Wizara ya Mambo ya Nje, Idara inahusika na Watanzania wanaoishi nje ya nchi, Wizara ya Mambo ya Nje ikayapitia haya maudhui ya hili Azimio, ikaangalia katika programu zake za *Diaspora* pale Wizarani, ina-align vipi ili kuhakikisha kwamba Wanasyansi wa Tanzania walioko.....

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Azimio hili muhimu. Nianze pia kwa kusema namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa mmoja mionganoni mwa wale Marais 14 walioitia saini mapendekezo hayo ya kuanzishwa kwa Itifaki hii katika nchi za Kusini mwa Afrika za *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, jambo moja kubwa niseme pia kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati ile ya Mindombinu, nimetoa mchango wangu kule umesikika, lakini bado yapo mengine mapya ambayo pengine ni vizuri nikayaongeza hivi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ambalo tungependa kuanza kwa wananchi, waelewe kwamba tunapokuwa na tafiti ambazo zinalenga kusaidia Jumuiya na kwa utaratibu huu wa kuingia katika Itifaki hii ya *SADC*, maana yake ni kwamba tunaongeza wigo wa eneo ambalo manufaa ya tafiti zetu tutakazokuwa tunazipata kutoka kwa wale wabunifu, tunaongeza wigo wa eneo ambalo tafiti hizo zitatumika. Badala ya kutumika katika nchi moja tu ya Tanzania, tafiti hizo na manufaa yake sasa yatakwenda zaidi katika eneo kubwa zaidi, yaani katika nchi karibu zote 14 katika mpango wa nchi za *SADC*. Kwa hiyo, hayo ni manufaa makubwa sana na ni lazima yawe yanawatia moyo wale watafiti na wabunifu na wale ambao ubunifu wao utazaa matunda kwa maana kwamba wanalo eneo kubwa zaidi la kutumia utafiti wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuseme kwamba, tumekuwa na wabunifu wengi. Ukitizama katika maonyesho yanayoendelea kila mwaka ya Saba Saba, ukiingia ndani mle, utaona kazi za wabunifu. Ukipitia katika sehemu za viwanda na biashara na *SIDO*, utaona utafiti mkubwa umefanyika na ubunifu wa hali ya juu umefanyika. Wapo watafiti ambao wameweza kutumia mabaki ya vyakula, takataka mbalimbali, wakawenza kuzichanganya pamoja na wakafanikiwa kupata mkaa ambao unatumika. Vile vile wapo wengi ambao wamefanya kazi ya ubunifu kama huo. Lakini, hebu tuangalie, baada ya kuona yote hayo ambayo watafiti hao na wabunifu hao wameyafanya katika maonesho ya biashara, nini kinachoendelea baada ya maonyesho yale kumalizika?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maonyesho kumalizika, ni wabunifu wachache ambao wanaweza kuendeleza yale waliyoweza kuyabuni kwa sababu moja kubwa. Ili uweze kuwa mbunifu, lazima utakuwa unahitaji kutumia muda wako mwingi sana katika kufikiri jambo na jambo jipy. Lakini, baada ya muda mrefu unaotumia ambao pia ni sehemu ya gharama, ni lazima vile vile uwe na uwezo wako wewe mwenyewe wa kutafuta vifaa vya kuanza kutengeneza hicho unachofikiria kukiibuni. Kwa hiyo, muda utakaotumia ni gharama, lakini na malighafi utakayohitaji ili uweze kuonyesha kile unachokusudia pia ni gharama. Kwa hiyo, baada ya kufanikiwa, unakuta gharama zako tayari ni kubwa na kwa hakika ili uweze kuendeleza utafiti huo, unahitaji msaada mkubwa wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna chombo kimoja cha kusaidia kuratibu sayansi na teknolojia. Chombo hiki lazima tukiwezeshe, ili chombo hicho pia kiweze kuwaratibu wale wabunifu na kiweze kuwawezesha baada ya kufanikiwa kuhakiki na kuthibitisha

ubunifu wao. Bila kufanya hivyo, kwa kweli tutakuwa tunawakatisha tamaa watafiti wetu, tutakuwa tunawakatisha tamaa wabunifu wetu ambao wanafanikiwa katika jitihada wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tuna Chuo cha Utafiti cha Kilimo pale Mlingano katika Jimbo langu la Muheza. Lakini ukienda pale, upo utafiti mkubwa ambao wamekwishafanya na ubunifu mkubwa lakini unaishia wapi, kwa sababu ya uwezo mdogo wa kuendeleza ubunifu huo haupo, kwa sababu Serikali mchango wake ni mdogo kusaidia katika Vyuo hivyo na utafiti katika Vyuo hivyo. Utafiti wowote hasa katika sekta hiyo ya Kilimo unabaki katika mafaili hautumiki. Hili si jambo jema kwa watafiti wetu. Tuwasaidie *COSTECH*, tuwasaidie Chuo cha Utafiti cha Kilimo Mlingano ili waweze kupata uwezo wa kuendeleza utafiti ambao wamefanikiwa kuubuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme kuna Mtanzania mmoja alikwenda kusoma Japan na baadaye wenzetu wa Japan walipomuona uwezo wake mkubwa walimwajiri kule amekaa Japan kwa zaidi ya miaka kumi, lakini kwa sababu ya kuipenda Tanzania amerejea nyumbani. Sasa hivi anatengeneza maboti aina tofauti ya uvuvi, lakini vile vile maboti ambayo yanaweza yakatumika kama *ambulance* katika maeneo ambayo ni ya bahari au maziwa, yupo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kikubwa ambacho anafanya kwa kutengeneza maboti ye ye hatumii mbao kama maboti mengine yalivyo, anatumia aina fulani ya *gypsum*, maboti yale yanakuwa ni mepesi, *yana-speed* kubwa kuliko yale ya mbao lakini vilevile yanatumia mafuta kidogo zaidi kuliko mafuta yanayotumika katika hayo ya mbao. Amefanya utafiti huo, amefanikiwa naomba Watanzania tumuunge mkono na hasa ndugu yangu yule ambaye amekiri kwamba anafanya biashara hiyo ya maboti basi ni vizuri naye akamwona, akajua ni namna gani ataweza kusaidiana naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hao ni wabunifu na wanaipenda Tanzania, angekuwa haipendi nchi yake asingerudi Tanzania, lakini amerudi Tanzania, naomba tumsaidie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika ni lazima pia tuseme utafiti una faida kubwa, tatizo la Watanzania kubwa ni ajira, kwa hiyo tukitumia vizuri utafiti na ubunifu nina hakika tutaweza kuongeza ajira. Tunasafirisha kwenda nchi za nje malighafi kwa wingi sana, tufanye utafiti wa kuhakikisha sasa malighafi hizo hazisafirishwi kwenda nchi za nje zitumike hapa ili tuweze kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile ni lazima tukubali kwamba utafiti si tu unaweza kuongeza ajira, utafiti vilevile unachangia katika kupunguza ajira, teknolojia mpya inapunguza ajira. Katika maeneo ambayo tulikuwa tukifanya kazi kwa mikono sasa kazi hizo kwa teknolojia mpya na ubunifu mpya zinafanyika kwa mashine. Kwa hiyo, wale waliokuwa wakifanya kazi kwa kutumia mikono wanapoteza ajira. Lakini ni lazima tuangalie huku na kule ni kwa kiwango gani utafiti wetu utaongeza ajira dhidi ya kiwango ambacho utafiti utapunguza ajira. Kwa hiyo, tukubaliane na mabadiliko ya teknolojia kwa sababu ni muhimu katika kuboresha uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na Azimio hili liridhiwe na Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa sababu ndiyo nafasi pekee ya kuwawezesha watafiti na wabunifu wa Tanzania kujulikana na nasema hapa wabunifu wote kuwe na utaratibu najua upo, lakini tuuimarishe wa kuwaratibu na kuwapa hati ya ubunifu wao ili wasije wakachukua watu wengine kwa sababu ya uwezo wakachukua ubunifu wa mtu fulani wakauendeleza wao kwa sababu huyu ameshindwa kwa vile hakuwa na uwezo. Tuwaandikishe wabunifu kwa utaratibu kwa kadri ya ubunifu wao na tuwape hati za ubunifu katika maeneo waliyoyafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie kwamba, naunga mkono hoja na nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante. (*Makofî*)

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ili niseme machache kuchangia katika itifaki hii. Pili, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri kwa kuleta Itifaki hii kwa muda wake ingawa imechelewa kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu uko katika maudhui yale ambayo yameelezwa katika itifaki yenyewe, nitalenga kutoa ushauri nini Serikali ifanye ili itifaki hii iwe ina manufaa kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza katika yale madhumuni naomba uniruhusu nisome, katika ile *item* namba (n) inasema kwamba: “*Increase access to the teaching and learning of basic science and mathematics at all levels of the education system*”. Pili ni: “*Promote quality in the teaching and learning of basic science and mathematics at all levels of the education system*”. Sasa haya ni mambo makubwa ambayo ni *fundamental* ili sisi tuweze kukidhi kuwa pamoja katika itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake ni kwamba, moja, tutazame mfumo wa elimu yetu ituwezeshe kuja kuwa sehemu ya washiriki wazuri katika Jumuiya ya walengwa katika Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba katika shule zetu za sekondari ni lazima tuanzie katika zile *basics*, katika shule zetu za sekondari tuseme ni lazima tulenge kuweka vivutio vizuri kwa ajili ya walimu wa sekondari ambao wanafundisha masomo ya sayansi. Jambo la pili, tuweke hamasisho na mashindano kwa ajili ya watoto wetu wa sekondari ambao wanasoma masomo ya sayansi. Kuwe na mashindano Kitaifa ambayo yanalenga watoto wawe na kivutio cha kusoma kwa bidii kwa ajili ya kushindanishwa katika masomo ya sayansi, bila kuwa katika msukumo huo katika sehemu za shule za Sekondari tutakosa msukumo wa kujenga sayansi katika *fundamental* hii ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, Itifaki hii vile vile inasisitiza katika *item* namba (k) inasema: “*Strengthen institutional capacity in research and technology institutions in the region and facilitate institution cooperation and networks*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili hatutafanikiwa ikiwa sasa hatutatazama ni namna gani mfumo wetu wa kufundisha sayansi katika Vyuo vyetu Vikuu na kutumia *science output* ile kwa ajili ya kuboresha uchumi wa nchi. Tutazame kwa namna gani sasa utafiti katika Vyuo vyetu Vikuu unavyoweza ukaungwa mkono kwa nguvu kutokana na bajeti ya Serikali, badala ya kutegemea sehemu kubwa ya bajeti kutoka nchi za nje. Tusipofanya hivyo basi tutaendelea kukwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kama walivyosema wengine, tutazame basi ni namna gani tutaweza tukasaidia wale wabunifu, vivutio Kitaifa viwe wazi katika Mikoa, tutenge sehemu ziwe wazi, tutenge sehemu ya bajeti kwa ajili ya kuhamasisha wabunifu waweze kutambua na iwe msukumo kwa ajili ya kuwahamasisha hao kuingia katika ubunifu utakaokuwa wa manufaa Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, utafiti unaofanyika katika Vyuo Vikuu uweze kuwa katika *transformation* ya *applicability* yaani matumizi halisi katika jamii, mazungumzo haya yalismwa na wazungumzaji wa kwanza na wa pili, ni mapendekezo ya msingi sana. Tuoanishe utafiti, ubunifu na *application* katika maisha ya jamii. Ni kwa kiwango gani utafiti unaofanyika katika Vyuo unavyoweza ukatumika vizuri kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili napendekeza kwamba, ikiwa vyuo tulivyonavyo vyote kwa mfano *Universities zinafanya research mbalimbali*, tunaweza tukalenga ni namna gani tunaweza tukatafiti au tukaanzisha *academies of science properly dedicated* kwa ajili ya *promotion of science and technology* kama hii inayoanzishwa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, itatusaidia ku-*streamline* hiki tunachokizungumza kwamba watoto wetu wanapomaliza sayansi ni namna gani wao wenyewe wanaona mwanga mbele, vyuo gani viro mbele yao ambavyo viro *specialised* kwa ajili ya sayansi na teknolojia katika maeneo yao ambayo watakuwa wanataka kubobe na Taifa liwe tayari kuwasaidia ili baadaye wakitoka wawe sehemu ya jamii ambayo inajenga uchumi kwa kutumia sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili mchango wangu kwa Wizara ni kuomba basi wajipange katika namna ya kutengeneza utaratibu na *interpretation* sahihi zinazoweza kuiwezesha Wizara ambayo ni mtambuka, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili tuweze kuwa pamoja na Wizara ya Elimu katika kuufanya huu mkakati wa kuboresha elimu kutoka ngazi ile ya kwanza kama nilivyosema, Vyuo Vikuu na baadaye tuone matokeo yake ni utafiti unaoboresha uchumi na maisha ya wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dokta William Mgimwa. Muda uliobakia hauruhusu kwa mchangiaji yejote mwagine kuendelea kuchangia na kwa hiyo tukirejea saa kumi na mmoja jioni tutaendelea na uchangiaji kuhusu Azimio letu la Kuridhia Itifaki

ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi hiyo, tutakuwa na wachangiaji watano watakaomalizia mchango wao jioni kabla ya kumwita Waziri kujibu hoja za wachangiaji wote. Nitawataja wachangiaji watatu wa mwanzo ambaeo ni Mheshimiwa Moses Machali, wa pili atakuwa Mheshimiwa Dokta Binilith Mahenge na wa tatu atakuwa Mheshimiwa Godfrey Zambi. Watakaomalizia ni Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla.

Waheshimiwa Wabunge baada ya hayo, nina matangazo machache, tangazo la kwanza linahusiana na Kamati ya sheria ndogo, tangazo hili linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria ndogo anaomba Kamati hiyo ikutane ukumbi wa *basement* kuna jambo la dharura mara baada ya kuahirisha hapa.

Tangazo la pili linawahu Wabunge wa CCM wote, kuna kikao cha Chama Ukumbi wa Msekwa, mara tu baada ya kumaliza shughuli hizi kuna kikao cha haraka, tukitoka hapa sasa hivi. Lakini pia niwakumbushe Wabunge wa CCM kwamba kuanzia saa nane mchana pale Nyerere *Square* katikati ya Mji wetu wa Dodoma, kuna Mkutano mkubwa wa chama wa kutambulisha Katibu Mkuu mpya wa Chama cha Mapinduzi pamoja na Sekretarieti mpya ya Chama cha Mapinduzi, wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nisitishe shughuli hizi za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.53 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, tunaendelea na majadiliano kuhusiana na Azimio lililofikishwa mbele ya Bunge hili na Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia la Kuridhia Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*).

Sasa tunao wachangiaji wetu kama nilivyotangaza kabla ya kusitisha mchana, mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Moses Machali na atafuatiwa na Dkt. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Moses Machali yuko Mtera.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENG:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kuhusu Azimio hili ambalo liko mbele yetu, Azimio ambalo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijatoa mchango wangu, naomba nitumie nafasi hii kuwapa pole wananchi wangu wa Jimbo la Makete kwa maafa makubwa yaliyotokana na mmomonyoko wa udongo ambaeo umekwenda kuharibu barabara karibu

robo kilomita kutoka Njombe mpaka Makete na hivyo kuathiri shughuli zote za usafirishaji pamoja na usafiri wa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kuishukuru sana Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Naibu wake, *TANROAD* Mkoa wa Iringa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Iringa ambao wamechukua haraka na za dharura ili kutatua tatizo hili kunusuru wananchi waweze kuendelea na shughuli zao na hivi ninavyoongea tayari shughuli zinaendelea za kuona kwamba inatafutwa njia mbadala ya kupita. Lile eneo kwa sasa hivi haliwezi kutolewa kile kifusi kwa sababu bado mmomonyoko unaendelea, kwa hiyo, nashukuru sana kwa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Azimio hili kama ifuatavyo. Umuhimu wa sayansi na teknolojia unatambulika duniani kote. Kimsingi, tofauti za maendeleo ya kiuchumi zinatokana hasa na maendeleo ya sayansi na teknolojia na katika nchi za Afrika tuko nyuma. Ni tofauti hizi za maendeleo ya sayansi na teknolojia ambazo zimefanya dunia hii igawike katika makundi mawili, kundi la kwanza likiitwa nchi zilizoendelea na kundi la pili likiitwa nchi zinazoendelea na wengine kimsingi tumepewa jina la nchi zinazoendelea kama nafuu kidogo lakini kimsingi tumekuwa tukiitwa nchi maskini, tumekuwa tukiitwa nchi za ulimwengu wa tatu, sasa nadhani ikaonekana pengine ambayo inakuwa nafuu kidogo ni hii ya kusema nchi zinazoendelea ingawa katika tafsiri sahihi mpaka sasa hatuwezi kujua kwamba nchi zinazoendelea *threshold* yake ni wapi, ni wapi tunaweza tukasema sasa tunaendelea au tumefikia kwenye sehemu ya kuanza kuendelea. Kwa hiyo, ili kuweza kujinasua bila kuwekeza kwenye sayansi, hili halitawezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, umaskini tulionao katika nchi za Afrika, unachangiwa na vitu vingi lakini yako mambo muhimu kama matano ambayo ndiyo yanachangia. Jambo la kwanza ambalo linachangia umaskini ni tatizo tulilonalo na sasa hivi linaendelea la utawala mbovu wa nchi nyingi za Kiafrika (*bad governance*). Jambo la pili ambalo linalochangia, nchi nyingi za Afrika ziko nyuma katika suala zima la kielimu. Jambo la tatu, nchi nyingi za Afrika hatutunzi mazingira, uharibifu wa mazingira ni mbaya kiasi kwamba mara nyingi tuko kwenye hatua za dharura za kutafuta chakula kulisha watu, hatufanyi kazi za maendeleo kwa sababu mazingira yameharibika na kunakuwa na *catastrophe* nyingi. Nne ambalo nadhani ni muhimu sana na ndio maana nimesema nchi nyingi za Afrika ziko nyuma ni sayansi na teknolojia. Kutokana na lengo letu la Taifa linalosema kwamba tunataka kujitegemea itakuwa vigumu sana kujitegemea kama hatutawekeza kwenye sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili limekuja wakati muafaka ingawa ukiangalia kwenye Sera ya Elimu ya mwaka 1985 ambayo imerekebishwa mwaka 1986 ilieleza wazi kabisa kwamba moja ya majukumu ni kuweka mahusiano mazuri na nchi za Kusini kwenye Jumuiya za *SADC* ili kuweza kubadilishana hizi sayansi na teknolojia na pengine hata wataalam wetu kama Azimio linavyosema leo hii. Toka mwaka 1986 mpaka leo mwaka wa 2011 ni muda mrefu umepita, kwa hiyo, kinachofanyika hapa tunatekeleza ile Sera ya mwaka 1986. Hata hivyo, naipongeza sana Serikali kwamba limewezezana na

tayari limeletwa mezani hapa kwa kulijadili, tunaomba tulipitishe ili lianze kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili litatusaidia sana, yako matatizo ambayo wakati mwingi tumekuwa tukikimbilia nchi za Ulaya kutafuta suluhu lakini kama tutakuwa na ushirikiano sisi wenyewe na nchi za jirani za Afrika Kusini na wengine upo uwezekano wa kubadilishana tafiti mbalimbali, matokeo ya tafiti mbalimbali na kufanya tafiti za maeneo sugu kama magonjwa ya malaria, ugonjwa wa UKIMWI na mengine ambayo tunaweza tukapata majibu kwetu humu ndani katika nchi zetu na tukawenza kuzinusuru nchi zetu katika majanga haya makubwa badala ya kutegemea tafiti za kutoka Ulaya kama vile tafiti za Malaria ambazo zinafanywa China wakati wao hali ya kule hailingani na ya kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tuwekeze kwenye sayansi na teknolojia. Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 inaeleza wazi kwamba itawekeza kwenye sayansi na teknolojia na mtaji wa kwanza utakuwa ni utashi wa kisiasa (*political will*) lakini mtaji wa pili ule utashi wa kisiasa utatafsiriwa katika kutenga fedha ili ziweze kwenda kwenye sayansi na teknolojia na kwenye maeneo kama ya utafiti. Mimi naona hili limetekelezwa ingawa lenyewe lilikuwa kwamba kufikia mwaka 2000 tuwe tumeshaanza kutenga asilimia moja ya *GDP* kwa ajili ya shughuli za utafiti, leo ni mwaka 2010 miaka 15 zaidi ndio limeingia. Kwa hiyo, naamini kwamba hilo pia ni utekelezaji wa Sera ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 inayosisitiza uwekezaji kwenye sayansi na teknolojia kwa kutenga fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo langu, kwenye Sera ile ilieleza wazi vipaumbele, iliweka mpaka asilimia fulani kwamba kwenye tafiti za kilimo na mifugo katika ile hela ingeweza kupewa asilimia 30 kwenye tafiti za viwanda, tafiti za usafirishaji, miundombinu wangetenga asilimia 20, kwenye tafiti za maliasili na utalii wangetenga asilimia 15, kwenye tafiti za afya wangetenga asilimia 10 na zingine asilimia 7.5. Sijui ni kwa kiwango gani vile vipaumbele vimezingatiwa kutoka ilipotungwa ile Sera na ile Sera imesema kwamba kila baada ya miaka mitano lazima vile vipaumbele vipitiwe upya kuvi-review kuona je, ndivyo inatakiwa au vipi na sijui ni kwa kiwango gani tumeweza ku-review kila baada ya miaka mitano kuanzia mwaka 1996. Kwa hiyo, nachopendekeza ni kwamba ni vizuri kwa kuwa tayari Serikali imesharidhia hasa kuititia Mheshimiwa Rais kwamba tuwe na asilimia moja ya *GDP* basi ni vizuri tuwe na Sera ambayo itatuelekeza kwamba ni tafiti zipi katika sekta ipi ili ziwe kipaumbele. Pengine tunapokwenda kwa wenzetu huko Afrika Kusini pengine tuwe tunatumia vile vipaumbele tulivyonyavyo, ndio tuelekeze utafiti wetu na pengine ni vizuri zikawa wazi kiasilimia watu waweze kuzifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu mchango wa taasisi za Sayansi na Teknolojia, hapa naongelea kuhusu Vyuo Vikuu. Vyuo Vikuu na taasisi hizi ndio zenye watalaam waliobobe, waliosomea mambo yote tunayoongelea kuhusu utalaam wa sekta mbalimbali iwe kilimo, iwe afya na sehemu zingine zozote zile, hawa watu wako kwenye Vyuo Vikuu lakini vyuo hivi haviwezesewi, vinapewa fedha kidogo sana. Sasa itakuwa vigumu kwa wao kufanya

tafiti kama hawapewi fedha za kutosha. Kwa hiyo, nashauri kama kweli tunataka kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia basi kipaumbele cha kwanza ambacho tunacho tayari, watu wapo tuwekeze kwa kuvipa Vyuo vyetu Vikuu vya Sayansi na Teknolojia fedha za kutosha ili waweze kufanya tafiti na kimsingi hawa ndio wanaoweza wakatembelea na vyuo vingine Afrika Kusini na sehemu zingine. Hapa nichukue nafasi hii kumpungeza sana Mheshimiwa Profesa Mbalawa juzi pale *DIT* kasaini Mkataba wa *Bilateral* na *South Africa* kuhusu *Research Development*, nina imani kwamba wenzetu wa *DIT* na *COSTECH* watatumia nafasi hii vizuri kuiwakilisha nchi yetu, hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu *COSTECH*, nawaomba sana kwa sababu inaonekana kimsingi hawajajitangaza vizuri, watu wengi hawaijui, kwa hiyo, watumie nafasi hii ya kutumia Azimio hili sasa wajitangaze, wajulikane ili waweze kusaidia taasisi mbalimbali ambazo zinaomba fedha kwa ajili ya utafiti. Lakini vilevile tunazo taarifa kwamba yako mambo ambayo yanapelekwa pale yanachukua muda mrefu. Ni vizuri wakaweka wazi taratibu zao na watu wakafahamishwa kwamba *research proposal* zao zimekubalika au hazijakubalika. Vilevile nao pia wangeweza hata kutuletea hata sisi Wabunge *brochure* zao kuonyesha maeneo ambayo wanayapa *priority* kwenye *research* ili tukawambie wenzetu ambao wanajua yale maeneo waweze kuanda hizo *proposal*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na haya ya kuchangia, naomba kusema kwamba naunga mkono hoja na nimwombe Mheshimiwa Waziri aendelee na kuchapa kazi kama alivyoanza, ahsanteni sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, sasa mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Pindi Chana ajiandae.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kuchangia Azimio la Kuridhia Itifiki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuuya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Itifaki hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Ingawa kimsingi kama walivyochangia watangulizi wengine, inachukua muda mrefu sana tangu Wakuu wa Nchi za Afrika au tangu Rais wetu anaposaini, sasa anaposaini siyo kuridhia mpaka linapoletwa Bungeni. Haikubaliki sana kwamba kama Rais amesaini mwaka 2008, Azimio linaletwa Bungeni mwaka 2011. Nachelea kusema mambo mengine inawezekana pia yakapitwa na wakati lakini pia Wabunge hata kama tunetaka kuchangia vizuri muda ambao tunapata Itifaki hii ni mdogo sana. *Imagine* hii Itifaki ndani ya Bunge letu Waziri anaanza kusoma taarifa yake ndio tunapewa, hatuna muda wa kutosha kuweza kusoma na naomba hili kwa wakati mwengine lisahihishwe ili tuweze kupewa *documents* hizi mapema ili tuweze kusoma vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimuulize Mheshimiwa Waziri, tuna Sheria ambayo ilianzisha *COSTECH*, Sheria Na.7 ya mwaka 1986, Sheria ile inazungumzia zaidi masuala ya sayansi na teknolojia, suala la ubunifu (*innovation*) halikuzungumzwa katika Sheria hiyo na mimi nimeisoma vizuri Sheria ile. Sasa leo tunaridhia Azimio ambalo linahusu Sayansi Teknolojia na Ubunifu (*Innovation*) lakini Sheria yenyewe ambayo kwetu imeanzisha *COSTECH* na ambayo inagusa masuala ya sayansi na teknolojia haina *component* ya *innovation*. Sasa nadhani Serikali ione kwamba huu ni upungufu pengine tulipaswa tupidie upya Sheria yetu, tuibadilishe ile *component* ya *innovation* ingekuwepo kwenye Sheria yenyewe. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri alone hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tulikuwa tuna Sera na ipo Sera lakini nazungumzia masuala ya sayansi na teknolojia nadhani miaka miwili iliyopita, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ilikuwa inaandaa Sera mpya ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Sasa hapa sina hakika kama Sera hiyo imeshapitishwa maana nilipita wakati fulani pale *COSTECH* nikaona andiko ambalo lilikuwa linazungumzia Sera ya Sayansi, Teknolojia na *Innovation* ambayo sina hakika kama imepitishwa. Kwa hiyo, ni vizuri Waziri pia aone haya mambo mawili na ni vizuri alifahamishe Bunge lako Tukufu kama hayo mambo mawili yako kwenye hatua gani maana si vizuri tunaridhia Azimio ambalo lina *component* ambayo haiko kwenye Sheria na wala haiko kwenye Sera. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atufahamishe kama hayo yamefanyika, kama hayakufanyika itakuwa ni upungufu kwetu kama Bunge kupitisha Itifaki ambayo inazungumzia *component* ambayo kwenye Sheria yetu na kwenye Sera bado havijawekwa sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka nilizungumzie na kimsingi hili limezungumzwa na wazungumzaji wengi lakini tunalizungumza na kulirudia kwa sababu ya umuhimu wa suala hilo. Hatuwezi kuendelea katika fani hiyo au upande wa sayansi, teknolojia na *innovation* kama Serikali haitakuwa tayari kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya sekta hiyo. Itakuwa vigumu kweli. Mwaka jana Waziri wa Fedha kwenye Bunge lako Tukufu tulipomtaka aeleze fedha za utafiti ziko wapi alipata tabu sana na kwa sababu tunazungumza pia Azimio la Addis Ababa la mwaka 2008 ambalo lilitaka nchi wanachama wa Umoja wa Afrika zitoe asilimia moja kwenye *GDP* yake kwa ajili ya kwenda kwenye masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Sasa tulipomtaka Waziri athibitishe alipata tabu na nakumbuka Waziri Mkuu aliagiza Waziri akaangalie maana Waziri alisema fedha hizo ziko kwenye sekta mbalimbali zinazohusiana na mambo ya utatifi. Sina hakika kama fedha hizo zilipatikana. Kama haliwezi likafanyika, tunaweza tukaridhia Azimio hili tukawapa nafasi wenzetu ku-*interact* na sisi kufanya kazi lakini bado sisi tukabaki nyuma. Kwa hiyo, mimi nataka niiombe Serikali Azimio la Addis Ababa la Mwaka 2008 kuhusu kutenga fedha karibu asilimia moja kama nilivyosema kwenye masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu basi liwe la kweli vinginevyo hakutakuwa na dhamira ya kweli ya kwenda kwenye shughuli za utafiti kama tulivyosema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma pia Sheria namba 7 ya mwaka 1986 ya kuanzisha *COSTECH*, Kifungu cha 5 cha Sheria ile kinasema *COSTECH* ndio taasisi

ambayo ita-*coordinate* shughuli za utafiti katika nchi lakini ukienda *COSTECH*, ukiwasiliana nao bado inaonekana shughuli za utafiti katika nchi hii hazijawa *coordinated* inavyopaswa. Mimi nilikuwa najiuliza hivi, najua Vyuo Vikuu vinafanya utafiti sana na vyuo vingine vingi vinafanya utafiti sana lakini ni kwa kiasi gani shughuli hizi ziko *coordinated*? Ni ngumu kujua. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Waziri wakati tunakwenda kuridhia Itifaki hii pamoja na kwamba atajibu hoja nyingine aone kwamba shughuli za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu zinakuwa *coordinated* sawasawa ili kama mtu anataka habari fulani basi tujue hiyo habari anaweza kuipata wapi? Shughuli za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu zinakuwa *coordinated* sawasawa ili kama mtu anataka habari fulani basi tujue hiyo habari anaweza kuipata wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lingine, wamezungumza pia wazungumzaji wengine, suala hili ni kwamba tumefanikiwa kufanya tafiti nyingi sana lakini tatizo lipo kwenye matumizi ya tafiti zenyewe. Tafiti nyingi tulizofanya, zimetusaidia namna gani kuboresha sekta ya afya, sekta ya kilimo na sekta nyingine ambazo zinazohusiana na masuala ya utafiti. Lakini ukienda kwa watu wa *COSTECH* na mahali pengine ambapo wanafanya utafiti na Vyuo Vikuu, wanakuambia tatizo lao kubwa ni fedha na ndiyo maana nimesema tunaweza tukaridhia hili Azimio kama hakuna *seriousness* kwa upande wa Serikali wa kuhakikisha kwamba taasisi zinazohusika na utafiti zinapewa pesa, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu na naogopa hatutafanikiwa. Mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri kama hutazungumza vizuri na Serikali ambayo wewe ni sehemu yake, hili Azimio linaweza lisitekelezwe kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, amfuate Mheshimiwa Rais, wala hana sababu ya kuogopa maana yeze ameletewa Azimio hili sasa atakaposhindwa kuwafuata na kuona kwamba pesa zinapatikana kwa ajili ya shughuli hizi, tutakuja tumuulize Mheshimiwa Waziri tueleze sasa shughuli hizi zinaenda namna gani, itakuwa ngumu kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nilizungumzie kama nilivyosema kuimarisha *COSTECH* yenyewe, *COSTECH* ina matatizo mengi. Moja, watafiti bado hawatoshi ambao ndiyo wanaotusaidia sana katika shughuli za utafiti maana tunesema si vizuri tukaanza kutekeleza Itifaki hii ambayo inazungumza kwamba kutakuwa na *free movement* ya watafiti katika nchi hizi, kama hatujaimarisha *COSTECH* na kuzalisha wataalamu wengi kwa maana ya utafiti, sisi tunaweza tukakuta tuna watafiti wengi kutoka nchi nyingine kwa sababu sisi wenyeze tuna watafiti wachache sana. Kwa hiyo, naomba tuwe na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba tunazalisha watafiti wengi. Si hivyo tu, tunazalisha watafiti wengi lakini baada ya kuwa tunao, tuangalie namna gani wanaweza wakafanya kazi katika mazingira mazuri na wasiwe na sababu ya kukimbilia nchi nyingine ambako wanaweza wakalipwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza wenzangu hapa asubuhi kwamba wako vijana, Watanzania ambao wameonesha ubunifu katika maeneo mbalimbali na mimi naomba niseme tu wachache. Mmoja nadhani Mheshimiwa Mtangi amemsema hapa, yupo kijana mmoja anaitwa Samuel Lwenje, huyu kijana ameishi Japan kwa muda wa kutosha na muda wake wa kuishi Japan amejifunza namna ya kutengeneza boti tena

za kisasa kabisa. Baada ya kurudi Tanzania ameanza kazi hiyo kwa nguvu yake mwenyewe. Sasa maeneo kama hayo ambayo kijana kama huyo ameamua kurudi nchini na kuanza kufanya kazi hiyo, si vizuri tukawaacha bila msaada, tuwasaidie ili waweze kufanya kazi vizuri na Watanzania waweze kufaidika na teknolojia mpya ya kutengeneza boti. Lakini pia tukimsaidia boti hizo anazotengeneza zinaweza zikawa na bei nafuu na Watanzania wengi kwa maana ya wavuvi wakaweza kuzitumia kwa shughuli zao za uvuvi na kwa maana hiyo kuimarisha mapato yao na shughuli zao za kiuchumi zikaweza kwenda vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo suala la Babu kule Loliondo, Mzee huyu, Mchungaji mstaaifu, mimi naweza kusema amefanya maajabu makubwa, Watanzania wengi inawezekana wengine wanaweza wasilione hili, lakini kwa sababu wengi wamekwenda pia watakuwa wanakubaliana kwamba Babu yule, Mchungaji Ambilikile Mwasapile amefanya kazi kubwa. Mimi naomba nitoe mfano, nilikuwa nasoma gazeti moja, yuko Mjerumani mmoja, mke wake alikuwa na ugonjwa wa *cancer*, ameenda kule amepewa kikombe cha Babu, katika muda wa kama mwezi mmoja ile *cancer* ambapo yule Mjerumani alikuwa amekata tamaa na maisha ya mke wake ameona kile kidonda kimeanza kupona na hivi tunavyozungumza ukifuatilia zile taarifa yule mama ni kama vile amepona, jambo ambalo hakulitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yule Mzee mimi nadhani tunapaswa kum- *support* kama Serikali, kama ambavyo tumeanza lakini tunapaswa kum-*support* zaidi maana hata kwenye Itifaki tukumbuke kuna *indigenous knowledge* katika masuala ya sayansi na hili tunapaswa pia tulifanyie kazi kubwa, tuhakikishe kwamba hawa wanaweza wakasaidiwa na baadaye tukaenda sawa. Lakini huyu Mzee pia kwa watu amba walitibiwa magonjwa ya kisukari na wenyewe wamekiri kabisa kwamba baada ya kupima wamegundua sukari imekwisha. Sasa hii ndiyo elimu ambayo tunapaswa tuijenzi, nina hakika inaweza kutusaidia Watanzania, tusipokuwa vizuri watu wa nje wanaweza wakaja wakaiba maarifa, elimu ya mimea aliyonayo yule Mzee, wakaenda kwingine wakafanya, tukaonekana kwamba sisi hatujamjali, lakini watu wengine wakamjali na wakaonekana wamefanikiwa zaidi kuliko sisi. Kwa hiyo, naomba Serikali yetu isione uzito kwa ajili ya kusaidia maeneo kama haya. Tuisamini *indigenous knowledge* kwa masuala ya sayansi na masuala ya utafiti, nadhani wanaweza kutusaidia na kama nchi tunaweza tukaenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia hayo, naomba niunge mkono hoja, lakini yale masuala ya msingi niliyomwomba Mheshimiwa Waziri ayatolee maelezo au ufanuzi kuhusu Sheria yenyewe, Na.7 ya 1986 kama ina mpango wa kupitiwa ili iwe na *component* ya *innovation*, atueleze kama hilo analiona namna gani na Sera yenyewe ya Sayansi na Teknolojia ambayo ilikuwa haina *component* ya *innovation* imefikia hatua gani vinginevyo, tutakuwa tunapitisha Sera au Itifaki ambayo itakuwa na upungufu kwa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono Itifaki hii, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana na hasa kwa mchango wako mzuri kuhusu Babu, tunaendelea. Mheshimiwa Pindi Chana atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Msola.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani za dhati kwako kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kilolo kwa kuendelea kuniamini kwa kunichagua kwa mara ya pili kuwawakilisha katika Bunge hili na kusema ukweli walinipa ushindi wa kishindo, nasema ahsante sana kwa watu wa Kilolo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nataka kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kuleta Azimio hili mbele ya Bunge lako Tukufu, pamoja na kwamba baadhi ya wachangiaji wanasema kwamba Azimio hili limechelewa, lakini nafikiri huu ni mchakato mambo mengi yanakuja wakati unapokuwa umeafiki na wote tumeona kwamba Azimio liliwekwa saini na Wakuu wa Nchi mwezi wa Agosti mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nachukua nafasi hii kulikumbusha Bunge hili kwamba Azimio kama hili sio la kwanza, mwaka 2009 tulipitisha hapa Azimio kama hili linalohusu Ushirikiano wa Nchi za Afrika Mashariki. Azimio lile lilikuwa na maudhui pamoja na madhumuni kama haya ambayo yameletwa leo hapa. Bajeti yake ambayo inazungumziwa kwamba hakutakuwa na *financial implications* isipokuwa katika kuhudhuria mikutano. Hili ni jambo la kawaida ambalo linawekwa katika Maazimio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, ni muhimu sana kwa wakati huu kwa sababu tunaishi katika karne ya sayansi na teknolojia ama karne ya utandawazi ambapo pana ushindani mkubwa katika mambo mbalimbali na silaha kubwa ya ushindani katika karne hii ya sayansi na teknolojia pamoja na umuhimu wa elimu kwa ujumla, lakini sayansi na teknolojia ndiyo tofali la ujenzi wa nyumba ya kisasa. Kama alivyozungumza Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge kwamba sayansi imekuwa ikifundishwa kwenye shule zetu toka miaka mingi, lakini kusema ukweli hatukuwa na Sera ya kutuelekeza, tunataka hii sayansi itupeleke wapi. Ilikuwa ni baada ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuhudhuria Mkutano wa Sayansi ama kongamano kule India mwaka 1984, alipoona umuhimu na faida kubwa ya sayansi na teknolojia kwa vitendo ndipo aliporudi huku akaanzisha wazo hilo kwamba tuanzishe Sera na Sera hiyo ikaandikwa mwaka 1986 ikaridhiwa tena mwaka 1996. Kwa hiyo, kwa upande wa sayansi na teknolojia kwa nchi yetu kwa kisera sisi bado wachanga, tuna miaka 24 tu. Kwa hiyo, ushirikiano na nchi nyingine kwa upande wa sayansi, teknolojia na ubunifu ni jambo muhimu kama tunataka kupiga hatua katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana, tuna Wanasyansi wachache sana hapa nchini. Kwa maana ya uwiano, siwezi kukumbuka takwimu zote kwamba

uwiano wetu ukoje, lakini nakumbuka kwa mfano, katika nchi hii, tuko watu karibia milioni arobaini na moja, ma-*Engineer* wote ni 8,500 na ukichukua uwiano ni kwamba kuna *Engineer* mmoja katika kila watu 5,000 ukilinganisha na nchi zingine ambazo zimeendelea ambapo ni *Engineer* mmoja kwa watu 250- 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua kwa upande wa Madaktari wa wanadamu, vilevile tuna upungufu mkubwa sana, upungufu ambao uwiano wake ni Daktari mmoja anahudumia watu karibu thelathini elfu na *World Health Organisation* ina recommend kwamba Daktari mmoja ahudumie angalau watu elfu kumi. Kwa hiyo, unaweza kuona jinsi ambavyo tuko nyuma? Nimechagua maeneo mawili tu ya kuyatolea mfano lakini kwa nini tuko nyuma? Tuko nyuma kwa sababu upande wa sayansi na teknolojia haukupewa umuhimu kama nilivyosema ni miaka 24 tu iliyopita ndiyo Sera ya kwanza imeandikwa hapa nchini na kutokana na Sera ya mwaka 1986, ndiyo kwa mara ya kwanza sayansi imetamkwa katika majina ya Wizara, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ilianzishwa mwaka 1990, November, kwa sababu ya kuona ule umuhimu wa sayansi kwamba lazima iwe *incorporated* katika masomo na ifuate ile Sera ambayo ilikuwa imetengenezwa lakini upungufu huu wa Wanasyansi umetokana na nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitembelea vyuo mbalimbali, kuna *Dar es Salaam University College of Education* mwaka 2007 mwishoni. Katika darasa moja la wanafunzi 205, wanafunzi waliokuwa wame-specialise kwenye *mathematics* walikuwa ni wanafunzi saba tu, wale waliokuwa wame-specialise kwenye *physics* walikuwa ni wanafunzi watano katika wanafunzi 205. Nimetembelea *Mkwawa University College of Education*, hivyo hivyo, uwiano wa wale wanaoingia kwenye sayansi ni mdogo sana. Leo tunasifu sana Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho kinalenga kuchukua wanafunzi kufikia arobaini elfu, sasa hivi wako karibu nusu, ishirini elfu lakini wale wanaochukua masomo ya sayansi ni wachache sana, ni chini ya asilimia 20 wale wengine wote wanachukua masomo mengine tu na sababu zake hazijulikani. Hali hii ni mbaya zaidi kwa wasichana, wasichana wengi hawachukui masomo ya sayansi na hasa huko nyuma kwa sababu waliamini kwamba masomo ya sayansi kama *Engineering* basi hiyo ni kazi ambayo inatakiwa kufanywa na mwanaume, lakini kwa leo baada ya mwamko na Vyuo vyenyewe kuanzisha *special program* inaitwa *Pre-entry Program for Female Science Students* imesaidia sana wasichana wengi kujiunga na masomo ya sayansi katika Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ili kusudi tuweze kushiriki vizuri katika haya yote tunayoyazungumza katika Azimio hili lenye madhumuni mazuri sana, nafikiri lazima tuanzie chini kama tunataka kweli kuendeleza sayansi, kwa sababu kama nilivyowaeleza uwiano wetu katika jamii, Wanasyansi ni wachache sana. Tuanze tokea shule hizi za msingi, kulikuwa na somo hili la maarifa ambalo lilikuwa linafundisha kimsingi mambo ya sayansi, twende shule za msingi, *secondary school* mpaka vyuo vikuu tupanue na tutoe motisha kwa wanafunzi wanaochukua masomo ya sayansi ili kusudi waone ule ugumu walioupitia, unathaminika. Huko nyuma mtu ukisema kwamba mimi nachukua masomo ya sayansi alikuwa anatembea hata akijivuna, leo hii mwanafunzi amefanya masomo ya sayansi mpaka *Form Six*, akienda Chuo Kikuu

anaingia kwenye *commerce* ama mambo mengine anaacha masomo ya sayansi, yote hayo kwa sababu watu wanatizama *benefits* zilizoko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko mbele nafikiri ni vizuri tukajipanga vizuri kupanua zaidi masomo ya sayansi na hasa tunavyoingia katika ushirikiano huu wa nchi mbalimbali ili kusudi tuwe na ushindani amba ni mzuri. Lakini vilevile tunazo Kamati nyingi za Bunge hapa, kwa kuzingatia kwamba tunaishi katika karne hii ya sayansi na teknolojia, karne muhimu sana, ya ushindani, ya utandawazi, nashauri Bunge letu Tukufu kwa siku zijazo lione uwezekano wa kuunda Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia mambo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kusudi kweli sayansi, teknolojia na ubunifu viweze kuwekwa mahali pake. Sasa hivi tutakuwa kama tunazungumzia nadharia na hatuipi umuhimu wake kamili. Kamati hii ndiyo ingekuwa kwa kweli iko katikati kufuatilia. Mabunge mengine yanayo Kamati kama hiyo ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza haya machache ambayo nafikiri yatasaidia katika kujadili Azimio hili ambalo mimi naliunga mkono pamoja na yale ambayo yamezungumzwa na wajumbe wengine kusema neno ubunifu limetoka wapi, *COSTECH* ilipoundwa haikuwa hivyo, lakini nafikiri ni wakati muafaka na hayo mengine tutizame namna gani yanaweza kuwa *incorporated* na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Prof. Msolla, kwa kweli mchango wako umesaidia sana katika kuliweka vizuri jambo hili. Sasa naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Pindi Chana ili na yeze aweze kuchangia suala lililo mbele yetu. Mheshimiwa Pindi Chana!

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza sana Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kutuletea *Protocol* hii ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Naiunga mkono hoja na niseme tu kwamba karne hii tuliyokuwa nayo ya *dot.com.technohama*, Azimio hili limekuja wakati muafaka, tunalihitaji katika nchi yetu na hasa katika ushirikiano na nchi za Kusini mwa Afrika. Wenzetu nchi zilizoendelea wamefika mbali sana katika masuala mazima ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Sisi Baba wa Taifa alisema wakati wenzetu wanatembea sisi inabidi tukimbie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maoni machache, baada ya kuridhia Azimio hili, ipo haja ya kuliweka katika utekelezaji. Sasa tunajipanga vipi? Leo tunaridhia maana yake ni *ratification* ni lazima tukubaliane kuli-*domesticate*. Sasa tunali-*domesticate* namna gani? Lazima tujipange vizuri na ninaposema kujipanga, ni muhimu Sera zetu zikawa zinaleweka. Tukawa na Sera nzuri ambazo zinahusiana na masuala mazima ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Sera hizo zianze kuanzia elimu ya msingi na sekondari na tuwe na *combination* ya masomo ya sayansi na teknolojia katika sekondari katika Wilaya zetu, liingie kwenye mitaala, isije ikawa watoto wetu wanamaliza *Form Four*, wanamaliza *Form Six* hawajui hata matumizi madogo madogo ya *computer*. Wenzetu sasa hivi, nchi zilizoendelea masuala haya yapo hadi shule za msingi na shule za awali. Mtu anataka kusafiri kwa nchi zilizoendelea anataka kutumia *underground* anafika *station*, tiketi yenyewe unaipata kwa kubonyeza bonyeza, tiketi inatoka. *Insurance* ya

afya unaenda unaweka hela benki, unapata kadi yako ya *health insurance* unatembea na kadi yako vilevile na *insurance* ya masuala ya *education*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati wenzetu wameshafika mbali sisi jambo hili limefika muda muafaka. Kwa hiyo, nianze kwa kusema ili tuwaonyeshe nchi zingine ambazo nazo zimeridhia ikiwa ni pamoja na Angola, Botswana, Congo, Madagascar, Malawi, Mauritius, Mozambique na Namibia, sisi Tanzania tujitolee kutenga eneo la Sekretarieti. Maana kwenye *protocol* hii imeeleza kwamba kutakuwa kuna eneo ambapo Sekretarieti ya masuala ya Teknolojia, Sayansi na Ubunifu yatakaa sehemu fulani mionganoni mwa zile nchi wanachama. Ukienda ukurasa wa nane, chini ya Article 5(6) kinasema, naomba ninukuu kwa Kiingereza.

*“The SADC Secretariat through the STI Unit shall be located within the SADC Secretariat and shall perform his function as prescribed by the Council”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tukubaliane, sisi Tanzania tuna maeneo mengi mazuri, sisi Tanzania tukubali ku-host maana ni mionganoni mwa nchi za Kusini mwa Afrika ili kuwaonyesha kwamba tuko pamoja lakini vilevile tuko mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ningeomba kwa zile *institution* ambazo huwa zinawasaidiasaidia sana vijana wetu wabunifu, maana asilimia 60 ya Watanzania ni vijana, zipo *institution* zinasaidia sana vijana kama wabunifu wa nyimbo, wanatoa *award*. Sasa na ubunifu wa mambo haya ya kisayansi wawe wanawapa *award*. Kunakuwepo na *proper competition* wabunifu wazuri wakipatikana, wapewe *award* au *certificates* kuwapa moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika ku-*implement* hii *Protocol*, kila Halmashauri ya Wilaya watenge Mkuu wa Idara moja ambaye huyo Mkuu wa Idara katika Halmashauri husika atashughulika na masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Maana kama mambo haya tunatarajia yafanywe na wananchi, ni muhimu tukawa na Idara inayoshiriki mambo haya katika ngazi ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunafikaje kule kwa wananchi. Kwa mfano mimi katika Wilaya ninayotokea ya Ludewa, akipatikana yule Afisa wa Vijana, kila Halmashauri ina Afisa Vijana na Utamaduni, anaratibu masuala haya. Ukiachilia mbali upande wa elimu ya sekondari, kuwepo na sekondari ambazo zina *combination* kwa mfano zinazohusiana na masomo ya sayansi, PCB, PCM, hizo ni *combination* muhimu ikiwa ni pamoja na maabara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za wenzetu hawana rasilimali za kutosha kama Tanzania. Naposema rasilimali masuala haya ya sayansi na teknolojia unahitaji rasilimali, unahitaji *of course, labour power and skill* lakini unahitaji rasilimali ili uweze ukafanya masuala ya kisayansi, sisi Tanzania rasilimali hizo tunazo. Wakati nchi za wenzetu hawana madini, sisi Tanzania tuna dhahabu, tuna almasi, tuna safaya, tuna ruby, tayari mtaji tunao, kama tunataka kufanya masuala mbalimbali ya kisayansi wakati nchi za

wenzetu madini hayo hawana, sisi tunayo. Ukienda Wilaya ya Ludewa, kuna Mchuchuma na Liganga na ndani ya yale madini unakuta kuna madini mengine *vanadium* na *titanium* ambayo yanatumika kama madini kwa ajili ya kutengenezea bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ipo haja ya kuonesha maeneo ambayo masuala haya ya sayansi na teknolojia yanaweza yakafanyika vizuri. Maeneo kama Ludewa, eneo la Kata ya Mkomang'ombe ambako yako madini hayana, Kata ya Mundindi, ni rahisi sana shughuli hizi za kisayansi zikafanyika, lakini tukubaliane kila Halmashauri ya Wilaya itenye eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba Wizara kama tunavyokuwa na siku ya maonesho ya kilimo, maonesho ya sabasaba, tuwe na siku ya maonesho ya shughuli za ubunifu wa sayansi na teknolojia. Vijana wetu wengi ni wabunifu sana, wengine wanabuni masuala ya umeme. Kuna vijana wazuri sana kijiji cha Manga, wanabuni umeme kwa kutumia betri, umeme unawaka. Vijana kama hawa tuwape *award*, tuwatambue. Inatia moyo na mwingine kesho anafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikubaliane kabisa na kuiomba Wizara tuanze sasa kuratibu masuala haya ya sayansi na teknolojia na ubunifu katika ngazi za Serikali za Mitaa, hii itatia moyo sana, licha tu ya kuridhia sasa tumekubaliana jambo hili liwe *domesticated* katika sera zetu, katika sheria zetu na katika utaratibu mbalimbali wa kimaendeleo. Naomba sana tukubaliane baada ya kuridhia Azimio hili, sasa tuweke mipango madhubuti kabisa kwa vijana wetu maana asilimia 60 ni vijana na vijana wa siku hizi wanaelewa sana, tena ni wabunifu sana. Yale maeneo ambako vijana wamebuni shughuli mbalimbali hususani za kisayansi na teknolojia siyo mbaya Wizara ikatoa mwaliko maeneo hayo, vijana hao wakaenda kujisajili, lakini wakajisajili wapi? Wakajisajili Halmashauri, kunakuwa kuna *register*, Wilaya X tunazo shughuli mbalimbali za kisayansi, Wilaya Y tunazo shughuli hizi za ubunifu wa kisayansi, kuna wengine wanabuni kutengeneza vitendea kazi, baiskeli na shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nirudie tena kwa kuunga mkono Azimio hili la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu na katika masuala ya ubunifu, nikimaanisha *intellectual property*, ni muhimu sana tukakubaliana ile Sheria ya *copyright*, mtu anapobuni awe ana hakimiliki ya jambo lile ambalo amelibuni na watu wengine wanapotaka kukopi jambo lile basi wapewe ridhaa na yule mhusika, yule mhusika anakuwa na *copyright* na tumtambue katika ngazi za Serikali za Mitaa. Lakini pia tujitahidi sana kuwapa *award* vijana wetu, wakiambiwa kuna mashindano, kuna maonesho ya masuala haya ya kisayansi kama tunavyofanya sabasaba, wanajiandaa vizuri na nchi yetu tunaratibu vizuri kwamba tuna masuala haya ya kisayansi na teknolojia maana karne hii ya sasa kila kitu ni sayansi na teknolojia. Humu ndani mwenyewe unatumia *microphone*, sayansi na teknolojia, siyo sawa kila kitu tuna-*import*, tuone *made in Tanzania*, *made in Dar es Salaam*, inaleta afya sana. Lakini kitu tukiangalia *made* na nchi nyingine basi hata kama siyo Tanzania iwe ni nchi mojawapo ya Afrika. Kwa hii *regional integration* katika masuala ya sayansi na teknolojia na *innovation*, naomba nipongeze sana. Sisi kama nchi za Afrika tuanze ushirikiano,

unaitwa *South to South Collaboration*, siyo yanatoka nchi za nje *West to South*, ahaaa! *South South Collaboration, South South technology* na baadaye ndiyo tutaangalia jinsi ya kushirikisha nchi zingine zilizoendelea za *Europe* na kadhalika. Lakini niipongeze sana Wizara kwa kutuletea *protocol* hii kwa muda muafaka lakini sasa baada ya kuridhia tukubaliane kuyaweka masuala katika utekelezaji halisi, tu-*domesticate protocol* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu ambao nina imani utazingatiwa na Waziri atakapokuwa anatoa ufanuzi, atatusaidia sana hususani eneo la Ludewa, Mchuchuma na Liganga ambapo masuala mengi ya kisayansi, madini yameshakaa tayari, tuone jinsi gani ya kushirikiana na wananchi wa Wilaya hii ikiwa ni pamoa na Serikali za Mitaa za eneo lile na kushirikiana na wadau na Mbunge wa Jimbo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofifi*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kuwasilisha Azimio hili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niipongeze Kamati ya Miundombinu kwa ushauri kuhusiana na uwasilishaji wa Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya kuridhia Azimio kuhusu Itifaki ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu ni kwanza kuridhia Azimio hili kutaongeza ushindani katika nyanja mbalimbali ikiwemo sekta ya viwanda, utafiti, kuongeza tija kwa wananchi na hivyo kuchochea uchumi wa nchi, kuimarika kwa kuongeza Pato la Taifa. Kama ilivyoelezwa ukurasa wa saba katika Kifungu cha 4(k) *intensification of efforts to attain at least one percent of gross domestic product (GDP) expenditure on research to increase the production.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuridhia Azimio hili kutasaidia upatikanaji wa watalaan mbalimbali wa Sayansi na Taknolojia na ubunifu kuanzia shule za msingi, sekondari na vyuo. Kifungu cha 2(o) katika ukurasa wa tatu (*promote quality in the teaching and learning of basic science and mathematics all level of the education system.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuridhia Azimio hili kutasaidia kutoa fursa sawa kwa jinsia zote katika kuendeleza na kuwakuza wananchi kisayansi kwa kuongeza zana za kujifunzia kwa vitendo katika maabara.

Kifungu cha 4(d) katika ukurasa wa sita (*promotion of gender equity and acces to science, technology and innovation education*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuanzisha mfuko kwa ajili ya kuwasomesha bure watoto wa kike waliofaulu masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuridhia Azimio hili kutasaidia kukuza ushirikiano kwa nchi wanachama katika masuala ya utafiti na maendeleo, pia ugharamiaji wa tafiti za kikanda pamoja na kukuza utafiti za kikanda pamoja na kukuza utafiti kuhusiana na teknolojia mpya na zile zinazojitokeza ikiwa ni pamoja na kubadilishana mawazo na uzoefu (*exchange of ideas through science and technology among the member state*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutaongeza ufahamu kwa wananchi juu ya umuhimu wa sayansi na teknolojia katika karne hii ya utandawazi na uelewa huu ni kwa njia ya makongamano mbalimbali yanayohusu sayansi teknolojia na ubunifu. Kifungu cha 4(1) ukurasa wa 7 (*promotion of public understanding of science, technology and innovation (STI) by launching programmes*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuridhia Azimio hili kutaimarisha mawasiliano (*information system*) kwa nchi wanachama na uboreshaji wa miundombinu ambayo utarahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali zinazohusu nchi wanachama

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Naibu Waziri Mheshimiwa Charles Kitwanga, Katibu Mkuu na watendaji wote. Naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo heshima kubwa kutoa mchango wangu. Nami naunga mkono kuhusu hoja hii na napenda kueleza machache katika kuboresha utekelezaji wa Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sasa kwa nchi yetu na Serikali kutenga fungu la kutosha kwa utafiti na baada ya kupata matokeo ya utafiti huo na kuyaingiza kwenye utekelezaji na matokeo yake tutapata tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini Tanzania wapo Watanzania wenyе vipaji vingi lakini Serikali haijawatambua. Pendekezo langu katika kuwatambua hao tubadili mitaala yetu kuanzia shule za awali ili kutambua vipaji na kuwapa uwezo na kuwaendeleza kulingana na vipaji vyao ili kupata wataalam na kuwatumia kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini wapo Watanzania wengi wenyе vipaji lakini mara wanapogundulika hupewa misukosuko badala ya kuwatengea maeneo maalum na kuwaendeleza kwa manufaa ya nchi. Kwa mfano, katika Wilaya ya Kilombero, Mji wa Ifakara, Kijiji cha Lipangalala alitokea kijana akatengeneza kituo cha redio ambacho kwa majaribio alirusha matangazo na kusikika redioni, lakini badala ya kumwendeleza akapewa misukosuko mpaka kutiwa hatiani. Hapo hapo Ifakara, Kijiji cha Mlabani yuko mwananchi amebuni mashine ya kupandia mpunga lakini hajapewa ushirikiano wa kuendeleza mashine hiyo. Mfano, mwengine ni watengeneza magobole ambao mara wanapogundulika, badala ya kupelekwa jeshini wakaendeleze taaluma zao, hukamatwa na kupelekwa mahakamani. Ni muhimu tukatumia fursa hii kuendeleza vipaji badala ya kuviua.

Mheshimiwa Naibu Spika, asante na naomba kuwasilisha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Naibu Waziri, Mheshimiwa Charles Kitwanga, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kuandaa Azimio la kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naipongeza Kamati ya Miundombinu chini ya uongozi wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Peter Serukamba kwa maoni mazuri sana ambayo Serikali ikiyachukua yatasaidia sana katika utekelezaji wa kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kunufaika na itifaki hii naishauri Serikali kuweka mikakati kabambe katika kuwekeza kwenye masuala ya sayansi na utafiti kama iliyoelezwa kwenye kifungu cha pili.

Vilevile naishauri Serikali kuwa mpango wa kutenga asilimia moja ya Pato ghafi la Taifa kwa ajili ya utafiti litekelezwe kwa haraka. Mpango utasaidia kama zilivyoendelea kiuchumi nchi za China, Indonesia, India, Malaysia na nyingine nyingi kwani ziliweka mkazo katika sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri pia Serikali endapo Itifaki hii itaridhiwa na Bunge hili ni vema sana Serikali kuchangamkia fursa zitakazojitokeza kutohana na utekelezaji wa Itifaki hii kwani idara na vitengo mbalimbali vitakavyoanzishwa vitawezza kutoa ajira kwa vijana na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali endapo Itifaki itaridhiwa ni vyema kuomba makao makuu yake yaye Tanzania itasaidia sana nchi kunufaika na Itifaki hii kwa nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono Azimio la Itifaki mia kwa mia na Mungu awatangulie.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la kuridhia Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika. Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kuzipongeza nchi za Jumuiya kwa kuunganisha nguvu katika kukuza sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zifuatazo ni changamoto ambazo zinatukabili kama nchi katika kuunganisha nguvu. Kwanza Serikali kutowekea maanani wabunifu wadogo wadogo wanaojitokeza nchini, Pili, kuanzisha vituo mbalimbali nchini katika kila Kanda na Mkoa ili kuibua vipaji vya wabunifu wanaoishi *remote areas* (vijijini).

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Serikali kutoa motisha kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi na teknolojia kwani namba ya wanataluma hao bado ni ndogo sana na nne, tofauti ya kimaendeleo ya teknolojia katika nchi wanachama inaweza

kuchangia kupoteza rasilimali za nchi kama dhahabu, wanyama na kadhalika na mfano mzuri ni vyura waliopo mto Malagarasi, vyura ambao inasadikika kuwa hawapo mahali popote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, turidhie itifaki *subject to reservation* katika *protocol* hiyo.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kutekeleza kwa pamoja melengo ya Bunge la *SADC* na hivyo kunipa fursa ya kurejea tena nafasi yangu ya uwakilishi katika Bunge hilo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Azimio hili ambalo litawezesha uendeshaji wa sayansi na teknolojia, hali kadhalika kuwezesha uvumbuzi wa wataalam wetu kwa kushirikiana katika eneo letu la *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale *TIRDO* tunaye mtaalamu mzuri wa kazi na eneo kubwa la kufanya kazi endapo atasaidiwa kwa kushirikiana na wataalam wa Wizara yako, tunaweza kutengeneza kituo cha *ICT* ambacho kitawawezesha wataalam wahitim (*graduates*) ambao hawana ajira, kuwa ni sehemu yao ya kutengeneza vitu vya majaribio kwa matumizi ya watu wetu, hata kama ni kwa kuiga. Watu leo hii sio lazima waajiriwe bali wawe kama *volunteers*; na hivyo kuweza kujua vipaji vilivyopo na wale wanaonekana kufanya vizuri kuchukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili mkataba huu utawezesha pia kuwa na mawasiliano ya karibu na kubadilishana taarifa kama vile za uvushaji wa silaha hatari na kadhalika. Lakini haitoshi tu kuridhia, basi ni vema pia kuainisha kama itifaki hii inaoana na sheria zetu, kama sivyo basi kurekebishwa ili ziende sambamba na itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, itifaki hii pia iwezeshwe kwa kuhakikisha kuwa wananchi wanaofaidika sio wa mijini tu, bali pia na hata wale wanaoishi vijijini ambako kuna rasilimali nydingi na vipaji viliviyolala kwa kukosa kuonekana. Lakini ili kuwezesha tafiti hizi suala la mawasiliano vijijini, bado ni changamoto. Basi mfuko wa mawasiliano vijijini uwezeshwe kwa kupewa pesa za kutosha ili angalau kila Kata iwe na kituo cha mawasiliano ya *internet*. Bado hali yetu ya matumizi ya *ICT* ni ndogo ukilinganisha na nchi nyininge. Tunawapongeza kwa juhudzi za kuridhia itifaki za *SADC*. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwa njia ya maandishi Azimio lililotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie Ibara ya pili ambayo inaelezea kuwa umoja huo kuna uwezekano wa kuwa na makao makuu yake. Mimi nashauri kuwa umoja huu utatusaidia sana nchini kwetu kama vile Azimio linavyosema. Watanzania washawishi makao makuu hayo yawe nchini kwetu Tanzania na hasa Dar es Salaam. Kwa kuwepo kwa makao makuu ya umoja hapa nchini Tanzania itasaidia kuongeza soko la ajira nchini kwetu na hasa katika jiji kubwa kama Dar es Salaam. Pia itasaidia kubadilishana mawazo ya uzoefu wa kazi na watu wengine ambao watawakilisha mataifa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili litatusaidia sana katika sekta ya vijana na wanawake katika ushirikishwaji wa shughuli mbalimbali za kimaendeleo na uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichangie Ibara ya 4 ya Azimio hili ambalo linalezea utaratibu wa Azimio hili ambao utatumika katika kupata wataalam. Azimio hili tulipitishe kwani litatusaidia katika eneo la kutafuta wataalam wa utafiti wa teknolojia. Ushauri wangu tuwatumie nao Watanzania waliopo nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wengi wa Tanzania wenyе ujuzi wa aina mbalimbali tena mabingwa wanaishi nje ya nchi kwa kuogopa kurudi nchini mwao kwa kuogopa kukosa ajira na malipo duni kutokana na uwezo na utaalam walionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Watanzania ambalo wamesomeshwa na fedha za Serikali ya Tanzania wamepata ujuzi na kuutumia katika mataifa mengine si kwa kupenda, ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja Azimio lipitishwe ili tuweze kukuza teknolojia ya ubunifu kwa maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika ambao itakuwa changamoto kwa vijana wetu walio na utalaam ndani na nje ya Tanzania kupata maendeleo. Napenda niwashukuru na kuwapongeza wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu na Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hiyo pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara husika pamoja na wadau kwa kuona haja ya kuwepo kwa azimio hilo sasa. Naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina pingamizi na Itifaki hii, naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono Azimio hili la Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi kwani ni kukuza ushirikiano, maendeleo, uhawilishaji na umahiri wa sayansi, tekinolojia na bidaa/ubunifu/ugunduzi.

Mheshimiwa Waziri tunajua kuwa bila sayansi, teknolojia na ubunifu nchi haiwezi kuwa na maendeleo. Mapendekezo yangu ni kuwa kuwatambua wabunifu, wagunduzi na wavumbuzi na kuwawezesha kuwathamini ili kuwatia moyo kuweza kuendeleza vipaji vyao hivyo katika masuala ya sayansi na tekinolojia. Pia kama Kambi ya Upinzani ilivyosema, Tanzania imajaaliwa katika kufanya tafiti nyingi, lakini zake hazikuleta maendeleo kwa nchi.

Mheshimiwa Waziri napendekeza kuwa ni lazima tafiti zinazofanyika kwanza kabisa ni lazima zigharamiwe na Serikali kwani wafadhili wanaogharamia tafiti hizi hatujui wana malengo gani. Pili tafiti hizo zitumike katika kuleta maendeleo na ziweze kutuletea ujuzi kwa wananchi wengi wa Tanzania. Ni kweli umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Hivyo, Azimio hili ni muhimu sana kwa Taifa letu, lakini inafaa Serikali ijjipange vizuri sana mbali ya kubeba jukumu la kugharamia tafiti katika vyuo vyetu na pia kuwatambua kwa karibu sana wagunduzi/wavumbuzi na kuwashawishi wataalamu waliomkimbia Tanzania warudi kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiridhia Azimio hili na likipita naomba Serikali kupitia Wizara yako iandae mazingira maalum ya kuwatambua wataalamu wa Kitanzania katika sayansi na teknolojia waweze kukubali kurudi nchini na kutumia ujuzi wao ndani ya nchi yao. Kama vile tunavyowawekea vivutio wawekezaji kuja kuwekeza, basi nao wawekewe mazingira mazuri kuja Tanzania. Naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ila napenda kutoa angalizo kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nchi yetu imejaaliwa vipaji vingi kutoka katika kila kona ya nchi yetu. Tumekuwa tukiona Watanzania kama kijana yule wa Manzese ambaye alitengeneza redio na kuweza kurusha matangazo. Vile vile aliweza kuunda kifaa cha ku-*alert* mzazi au mlezi kipindi mtoto analia popote alipo au kama simu inaibiwa, lakini tumeshuhudia Serikali kwa maana ya Wizara kukaa kimya bila kuendeleza kipaji hiki au hivi. Nchi za wenzetu huchangamkia na kuendeleza na ndiyo njia mojawapo ya kuchangia uchumi wa nchi kwa kutoa ajira kulinda fedha au mauzo ya ndani.

Vilevile tulishuhudia Mtanzania kabuni kifaa cha kuzalisha ila hatujui hii teknolojia yake iliishia wapi, wengine waliweza kuunda hadi mashine gani huko Songea na mifano mingine mingi kama yule wa Mbeya aliyebuni baiskeli inayotumia injini ambayo ameitengeneza mwenyewe. Hii ni hatari sana kama hatuendelezi hivi, nashauri chuo kijengwe kwa hivi vipaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha na kuunga mkono Azimio na kukazia iwepo taasisi ya utafiti wa mambo ya sayansi na teknolojia nchini ambayo itaangaza popote kwenye vipaji na kwingleko.

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono itifaki hii ili kutoa kipaumbele katika kupata wataalamu wengi katika nyanja hii pamoja na kuvutia wanafunzi wengi wasome sayansi lazima tuweke vivutio. Moja katika vivutio vikubwa ambavyo nchi kama India, Srilanka na kadhalika ilitumia ni mshahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, waajiriwa wote waliozuza katika teknolojia na sayansi hupewa mshahara mara mbili kuliko wahitimu wengine, hivyo naiomba Serikali kutoa mishahara mikubwa zaidi kwa wahitimu wote watakaohitimu masomo ya sayansi.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia itifaki hii iliyoko mbele yetu katika kuridhia itifaki hii ya sayansi. Sisi kama Watanzania ni vizuri tukawathamini na kuwapa moyo, kama wale wavumbuzi wetu wa *SIDO*. Serikali ni vizuri ikawatupia jicho wabunifu hawa, kwani hutumia muda mrefu kuvumbua mambo ya aina mbalimbali. Naomba Serikali sasa kuwawezesha *SIDO* ili waweze kukidhi haja na kuweza kuongeza ubunifu wa mambo mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika napenda pia kuikumbusha Serikali wale wabunifu ambaao huleta mali zao katika maonyesho ya Sabasaba, ubunifu mzuri katika mabanda yote ya maonesho tunapomaliza maonesho hayo wabunifu hao huenda wapi? Serikali ina mpango gani na wavumbuzi hawa. Ni vizuri kama wavumbuzi hawa baada ya maonyesho wakafuatiliwa kwa karibu na wakawezeshwa ili wapate kufanya kazi hizo kwa upana zaidi ili tuweze kuwa na wabunifu wengi zaidi ambaao pia watakuwa walimu tosha wa vijana wetu kama watajitungaza na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni bora kutenga hiyo asilimia moja ya bajeti kwa utafiti ni bora pesa ya utafiti ikaongezeka na kuzingatia itifaki hii na tukawathamini wavumbuzi wetu, kuridhia azimio hili litakuwa la maana. Pia ni vizuri Chuo cha Nelson Mandela cha Arusha kiongezewe pesa kwani tukipata wavumbuzi wasomi wa ndani ya nchi na wakiwa wasomi wazuri nadhani uvumbuzi huo utaleta tija na itifaki itakua tumeridhia kwa malengo na manufaa ya nchi na wananchi wake. Nashukuru.

**MHE. ZAHRA ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ilipo mbele yetu. Dunia ya sasa, nchi yoyote haiwezi kupata maendeleo bila kuinua sayansi na teknolojia, hivyo suala la kuleta Azimio la Kuridhia Itifaki hii naipongeza Serikali hasa kwa vile haikuwa na gharama yoyote ya kulipia kwa sababu sisi tayari ni wanachama wa *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la muhimu ambalo naishauri Serikali juu ya kuisaidia nchi kuielewa Itifaki hii na kuweza kutumia fursa adhimu ambazo zitajitokeza ili kutoa ajira kubwa kwa Watanzania na kupunguza wimbi kubwa la vijana wetu ambaao hawana kazi zinazoendelea. Watanzania tuna vipaji vy'a kila aina ambaao tukiwatumia vinaweza kutusaidia Serikali ichukue hatua ya kuvifutilia vipaji hivyo. Ahsante sana. Nakushukuru.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kukupongeza wewe pamoja na wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu. Mimi mchango wangu unakuja katika kifungu namba 2.0 kinachosema, “nchi yetu ifanye bidii kuchangamkia fursa zilizojitokeza.”

Sasa mimi kwa kuongezea maoni yangu katika fursa zilizojitokeza, kwa nini tunashindwa kwanza kutimiza uzalendo kwa kuzitumia hizi fursa zilizopo nchini. Ili kuendeleza wabunifu wetu na wagunduzi wetu ambaao ni wazalendo kama huyu kijana Said Omary wa Zanzibar, ambaye mwaka jana aligundua kutengeneza gari na ni Mzanzibari wa mwanzo na juzi tu katengeneza gari lingine. Sasa fursa kama hizi tuzizingatie kwa kujivunia kwamba, Mtanzania mmoja kugundua kutengeneza gari kama tunataka kuwatumia ni lazima tuwatengeneze kwa kuwatafutia utaalamu zaidi na tuwatangaze. Tuna wabunifu wa mambo mbalimbali ila Tanzania tunasahau uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa vijana wapo wengi ila hawajatengenezewa mazingira na mwisho wa siku tutajikuta kwamba tunatumia waliogundua wenzetu na kuviacha vy'a kwetu kwa kutotumia zile fursa tulizonazo. Ni lazima kwanza tukatumia uzalendo kwanza kwa kuwaandaa na kuwatangaza wagunduzi na wabunifu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja wa Rais Yoweri Museveni wa Uganda, kulikuwa kunatakiwa kuchimbwa mafuta akawaita wataalamu wa kizungu wakaleta hoja nyingi pale kuhusu uchimbaji wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Museveni akawaambia basi tokeni kwanza nipange na watu wangu. Rais Museveni akawakusanya vijana wazalendo wa nchi ile ya Uganda na wako Vyuo Vikuu akawapeleka nchi za nje kusoma kuhusu jinsi ya uchimbaji wa mafuta na mambo ya sayansi, teknolojia na ugunduzi. Basi wale vijana sasa ndio waliokuja kuchimba mafuta ya Waganda. Leo hii kwa nini Tanzania hatutumii uzalendo kama wanaotumia wenzetu ambao nchi zao sasa zinaendelea kwa kuwatumia wagunduzi/wabunifu wa ndani ambao ni wazalendo hapo ndipo hiyo sayansi na teknolojia ya ugunduzi/ubunifu ambao tunautaka ndio tutaupata au tutaishia kuwanufaisha wenzetu tu. Naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nitakuwa nimekosea naomba samahani kwani ndio ninajifunza mwanzo ni mgumu.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuleta hoja hii kupitia Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la kuridhia itifaki ya sayansi, teknolojia na ubunifu ya jumuiya ya maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutafuta maendeleo ya nchi tunatakiwa kufanya utafiti na ubunifu kupitia akili, maarifa na juhudhi. Vilevile tunapaswa kujifunza kupitia wenzetu lakini tuige yatakayotufaa kutokana na utamaduni wetu na tuyache yale yatakayokwenda tofauti na utamaduni wetu kama Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi tumekuwa tukitofautiana katika uchumi. Aidha, kutokana na ubora wa ardhi ya nchi husika, malighafi kama madini, mbuga za wanyama, maziwa na bahari na kadhalika. Vyote hivyo ni vitega uchumi vyta nchi. Kwa upande wa kilimo, kuna ardhi ambayo inakubali mazao yote, ila kutokana na kukosa elimu ya ardhi na mimea, kwa maana ya kukosa ubunifu wa kujaribu, nchi inaweza kuwa masikini au Mkoa na hata Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nataka kusema Serikali ifuutilie sana ubunifu kwa wananchi kuhakikisha wanakuwa na ubunifu wa kujaribu hasa kwa upande wa kilimo vijijini. Kwa mfano Wilaya ya Mpanda ardhi yake ni sawa na ardhi ya Wilaya ya Nachingwea. Lakini utaona kuwa Nachingwea wanalima sana zao la nazi aina ya mbata ambazo zinakomaa kwa muda mfupi na kuwaingizia wananchi kipato na pia kiungo kizuri kwa chakula kwa afya za binadamu. Hivyo kwa kutumia ubunifu hata Wilaya ya Mpanda mwananchi anaweza kuchukua mbegu ya zao la nazi au mbaazi na kupeleka kwenye ardhi ya Wilaya ya Mpanda na tayari kwa ubunifu huo mwananchi anaweza kubadilisha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, kama nimekosea naomba radhi mwanzo ni mgumu.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia azimio lililo mbele yetu kwa kuhimiza Serikali ipange mkakati maalumu wa kuhamasisha na uwasaide wasichana/wanawake kusoma masomo ya sayansi na hasa somo la hisabati. Miaka ya nyuma, yaani miaka ya 1970 na 1980 wasichana walikuwa wanachukua masomo ya sayansi ambayo hesabu ni sehemu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwamko huu umepungua katika miaka ya karibuni kutokana na ukosefu wa nguvu ya kujiamini lakini pia hamasa ya Serikari. Ukosefu wa maktaba (*laboratories*) na walimu katika shule na vyuo umekatisha tamaa wanafunzi kusoma masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubunifu alionao mtu na hasa watoto wadogo umechochewa na mafunzo anayoyapata shulenii, nguvu ya fedha ya familia lakini kwa kiasi kikubwa na Serikali. Kwa misingi hii Serikali itenye Bajeti kwa ajili ya kuwawezesha wabunifu kutekeleza na kupata ufanisi kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jambo hili ni mtambuka Wizara ya Elimu iwe na mipango ya kuanzisha shule maalumu za kufundisha masomo ya sayansi na zipatiwe vifaa vya kisasa na walimu ili kujenga misingi kwa kizazi hiki na kijacho ili kukabiliiana na ushindani wa kisayansi kati ya nchi yetu na nchi za SADC. Kwa maoni hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nakushukuru kwa kupata fursa hii adimu kuchangioa hoja hii kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa kuna watu wengi ambaao wanafanya kazi nzuri lakini bado Serikali hajatoa nafasi kwa watu hawa kupewa kipaumbele au kazi yao nzuri kuthaminiwa kwa ajili ya kikazi kijacho. Tunao wazee ambaao wanabuni vifaa mbalimbali vya uhunzi, uchongaji lakini mchango wao bado haujafanyiwa kazi. Wazee hawa baadhi hawakwenda shule, lakini wanao uwezo mkubwa sana wa kuchonga vitu mfano kiko, mithili ya kile ambacho kimepitia katika mashine bora na hata bidhaa wanazozitengeneza kwa ubunifu bado hawana uhakika wa soko lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la wataalamu wetu bado kutothaminiwa ni tatizo kubwa sana. Kuna wataalamu wengi ambaao Serikali imewagharienia katika mafunzo lakini bado hawathamini na matokeo yake watu hawa wanaenda kutafuta mazingira mazuri ya kazi, mfano wataalamu wa uchimbaji madini, uchimbaji mafuta na gesi asilia na wengine ambaao mpaka sasa hata Serikali haitoi nafasi ili wakasome, Taifa hili lazima tujipange na tuone tunaelekea wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda mwafaka sasa suala hili liende sambamba na hali yetu ya elimu, mazingira na fursa tulizo nazo na hili litaleta uwiano yakinifu katika makundi yetu yaani uhalisia wa vijana nchini kupata elimu sahihi ya sayansi, wasome

kwa nadharia na vitendo. Serikali yetu ifanye jitihada za kuweka maabara katika shule zetu za Kata na vifaa viletwe hii ikiwa ni pamoja na idadi kubwa ya walimu wa sayansi. Pia wabunifu wote vijijini na mijini wabainishwe na kazi zao zifuatiliwe na kupewa kipaumbele. Serikali itenye fedha kwa ajili ya kuendeleza vipaji hivi, pia kazi hizi zitunzwe kwa ajili ya kizazi kijacho. Naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika siku hii ya leo na hata kuweza kuchangia katika Bunge hili kupitia maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Serikali kwa kuleta azimio hili hapa Bungeni ili liweze kujadiliwa na kuweza kupidishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuungana na azimio hili ambalo naamini ni chachu ya maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania na pia katika nchi za Kusini mwa Afrika kwani ushirikiano wetu mzuri ndiyo utakaorahisisha maendeleo ya Watanzania wote walio ndani au katika Jumuiya ya nchi za SADC.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naungana na Kambi ya Upinzani Bungeni katika maelezo mazuri iliyotoa kupitia Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mbunge wa Jimbo la Bukombe kama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kuwa Serikali sasa itumie fursa hii kujipanga vizuri ili isahihishe upungufu uliojitekeza katika utekelezaji wa Sera ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kutokana na Serikali kutojali wagunduzi/watafiti mbalimbali ambao wamekuwa wakipoteza muda wao mwingi katika kutambua mambo mbalimbali ambayo yangeweza kusaidia kwa kiwango kikubwa katika kuleta maendeleo kama tu wangesadiana na watafiti hao au wagunduzi ili waweze kufanikiwa na kusonga mbele, wanahitaji malighafi mbalimbali ili kuweza kufanikisha zoezi zima la ugunduzi. Mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine - Morogoro, vyuo vya mafunzo na kadhalika, vikisaidiwa ipasavyo vinawenza kuleta tija ya kutosha katika nchi yetu na hata kuweza kuanzisha viwanda vidogo ambavyo baadaye vitasaidia vijana katika ajira hata maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja na kuomba tena Serikali ichukue juhudhi za makusudi katika kuimarisha taasisi mbalimbali zilizopo nchini ili ziweze kutusaidia katika maendeleo kwa haraka.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ningependa kuchangia kama ifuatavyo kuhusu Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii moja ya faida ni kuwezesha wataalamu wa Tanzania kushirikiana na nchi nyingine katika utafiti na ubadilishaji wa taarifa zinazohusu sayansi, teknolojia na bidaa (ubunifu). Ni vema Wizara hii ikalinganisha manufaa haya na Wizara nyingine kama ya elimu kwa kuwa tunawezaje kupata

wanasayansi watafiti na wabunifu wakati mwongozo uliotolewa na Wizara kwa shule za msingi mwaka huu kwamba maswali ya somo la hesabu kwa darasa la saba wataulizwa kuna *multiple choice* yaani kuchagua? Jibu sahihi kati ya A, B, C au D? Hapo tunajenga watoto kuwa wanasayansi kweli? Kwa maoni yangu tutakuwa tunadumaza vipaji vya watoto; hivyo, hatuwezi kufikia lengo baada ya kuridhia itifaki hii baada ya miaka kadhaa ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara na Taifa kwa ujumla linahimiza masomo ya sayansi na teknolojia kwa kuwa tunaridhia itifaki hii ni vizuri pia Wizara ikaona namna ya kutambua kuainisha vipaji vya watoto shulenii kuanzia ngazi za sekondari ili fursa zitakazojitekeza kutokana na utekelezaji wa itifaki hii zipatikane katika nchi yetu kwa uendelevu, yaani kwa miaka mingi zaidi ili pia tuweze kuwa na uwezo wa kushindanishwa na nchi nyingine. Kwa sasa Wizara ina benki ya watoto wenye vipaji maalum ambao wanaweza kuendelezwa, kukuzwa na kuwa wanasayansi bora, wanateknolojia na wabunifu hodari? Ni vema sasa Wizara ikashirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii ili kuchukua hatua muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kuititia Wizara yake kwa kuleta Azimio la Kuridhia Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Pia naipongeza Kamati ya Miundombinu kwa Kuridhia Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika Azimio hili ni kwamba Waziri pamoa na Wizara yake watalie mkazo zaidi ndani ya nchi yetu na kuwezesha wananchi wake wa Tanzania kuwa na fursa zaidi ya kushiriki ipasavyo kwa ufanisi zaidi. Hivyo basi, naishauri Wizara kuweka mkakati maalum ambao utawashirikisha ipasavyo wananchi wake kwa kufanya mambo mbalimbali kama vile kuboresha elimu ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika nyanja mbalimbali kama vile mitaala shulenii, elimu hii ya sayansi, teknolojia na ubunifu ianzie katika ngazi ya msingi hadi ya juu, japokuwa kwa elimu ya juu inaonekana kidogo. Tunaiomba Wizara izingatie changamoto za sasa katika kuboresha hili, kwani kuboresha elimu ya sayansi na teknolojia itasaidia kwa kiasi kikubwa kupata wabunifu katika nchi yetu. Kufanya hivyo, kutawawezesha wanafunzi na pia wafanyakazi wa Serikali kuwa na elimu ya sayansi na teknolojia ya kutosha kwa kuboresha mitaala shulenii na hata kwa watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napendekeza kwamba Wizara katika Bajeti yake itenye kiwango maalum cha Bajeti kwa ajili ya kutoa elimu ya sayansi na teknolojia kwa Watanzania ili kusaidia kuleta wabunifu zaidi na zaidi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke mkakati maalum kuititia Wizara hii na kuhakikisha ndani ya muda fulani, tuna wabunifu wa kutosha katika nchi yetu ambao kuititia ubunifu wao matumizi na gharama za maisha yetu kupungua kwa kuwa na

wabunifu wa kutosha ndani ya nchi yetu. Pia Wizara kutumia fursa yake kwa kuimarisha njia mbalimbali za uhawilishaji ili kuleta mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo bado naishauri Serikali kuimarisha zaidi njia mbalimbali na kuboresha ili kufikia malengo husika. Naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi naunga mkono hoja. Ila kuna baadhi ya vipengene ambavyo ni muhimu vizingatiwe ili kufanikisha suala hili.

Mheshimiwa Spika, *area of specialization* ni kwamba taasisi zetu za sayansi na teknolojia zifundishe kozi ambao zinaendana na mahitaji ya soko katika nchi yetu. Kwa mfano, mahitaji ya viwanda vya kusindika mazao, nguo, pembejeo, mawasiliano na kadhalika ni muhimu katika nchi yetu. Hivyo basi, vyuo vingi *vi-specialize* katika kozi hizo kwa viwango mbalimbali. Hali kadhalika watoto wetu hususan wale wa kiwango cha digrii ambao wanasona masomo ya sayansi wajitahidi kujikita zaidi katika vitendo kuliko nadharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uanzishwaji wa viwanda, bila viwanda hususan viwanda vidogo vidogo katika nchi yetu, malengo ya sayansi, teknolojia na ubunifu itabaki kuwa nadharia na ndoto tu kwani nchi zilizoendelea kiteknolojia zilienda sambamba na uanzishwaji wa viwanda ambavyo vilisaidia kuthibitisha nadharia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *transfer technology*, hii nayo ni hatari kwa maendeleo ya teknolojia katika nchi yetu. Hivyo, tafiti zifanyike kwa kina ili kulinganisha teknolojia katika nchi zingine za SADC hususan *South Africa*, Ikiwa teknolojia ya nchi hizo ni ya juu ukilinganisha na nchi yetu bado nafikiri kutakuwa na tatizo la ubunifu wa hali ya chini kutoka kwa wataalam wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti zetu ziendane na mazingira halisi ya Tanzania, ushauri utolewe kwa wataalam wetu kufanya utafiti katika mazingira ya Tanzania hususan katika sekta ya dawa badala ya kukimbilia nchi za nje kufanya tafiti kwa ajili ya maslahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti maalum itengwe kwa ajili ya watafiti na wagunduzi. Bajeti hii ilenge kuwasaidia watafiti kufanya utafiti bila matatizo. Motisha itolewe kwa watafiti/wagunduzi ili watafiti wafanye utafiti wao kwa mazingira tulivu. Naunga mkono hoja!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Misungwi, kwa kunichagua kwa kura nyingi sana na vilevile kwa kuchagua Madiwani wote katika Kata 27 kutoka Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwape pole wananchi wa Misungwi, kwa kuondokewa na Diwani wa Kata ya Lubili, Mheshimiwa Jeremiah Shitungulu. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru tena Mheshimiwa Rais, kwa kuniteua katika nafasi hii ya Unaibu Waziri. Niwapongeze, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikupongeze Mheshimiwa Spika, Naibu Spika kwa kuchaguliwa katika nafasi hizo mlizonazo lakini vilevile niwapongeze Mawaziri na Naibu Mawaziri wenzangu wote. Vilevile nitoe pongezi zangu kwa Wabunge wote ambao mko hapa mkifanya kazi hizi ambazo wananchi waliowachagua wamewatumeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwashukuru Wabunge wote kwa michango yao mizuri sana ambayo nina uhakika itatusaidia sana katika utekelezaji wa Itifaki hii. Nijikite kidogo tu katika hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nianze na hoja ambayo iliuliza ni kwa nini tupitishe Itifaki hii haraka haraka, ni hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa. Vilevile nizungumzie hoja ambayo imesema kwamba idadi ya nchi ambazo zimeridhia Itifaki hii ni mbili na ikaungwa mkono na Mheshimiwa John Mnyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili suala la kwa nini tunaridhia, kwanza kabla ya kuridhia Waheshimiwa Marais wetu walisaini kule Johnannesburg lakini baada ya kurudi hatuji tu hapa moja kwa moja, kunakuwa na mchakato unaohakikisha kwamba kitu hiki kinacholetwa hapa watu wote wanaohusika wamekubaliana nacho? Cha kwanza wataalam mbalimbali wanaipitia Itifaki hiyo halafu wadau mbalimbali kama sisi, vyuo vikuu, *research institutions* zote zimepitia na zote zimekubaliana na sisi kwamba tuulete hapa Bungeni uweze kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu idadi ya nchi, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mnyaa na Mheshimiwa Mnyika, yale tuliyoyasema katika Azimio letu ndiyo yaliyo sahihi. Yawezewekana jarida alilonalo Mheshimiwa Mnyaa liliandaliwa mapema lakini mpaka kufikia hatua ya kuchapishwa, nchi nyingi tayari zilikuwa zimesharidhia. Kwa kumthibitishia tu, wiki iliyopita Waziri wa Sayansi na Teknolojia wa Afrika Kusini alikuwa hapa kwa ajili ya kusaini itifaki nyingine ambayo ni *bilateral* na alituthibitishia kwamba wamesharidhia kule Afrika Kusini. Kwa hiyo, yale tuliyowasilisha ni sahihi na naomba Bunge lako liweke rekodi hiyo kama tulivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna hoja iliyojitokeza ya namna watu watakavyoingia katika nchi yetu kwa kigezo cha kwamba ni watafiti na vilevile tukaelezwa kwamba hizi *treaty* mbili zinapingana. Lakini labda niseme kidogo kwamba Azimio hili linaleta Itifaki inayozungumzia Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Hawa wataalam waanze kuja katika nchi zetu polepole na kushirikiana. Taratibu zote zinazomtaka mtaalam kuja kushirikiana hapa nchini kwetu ikiwa ni pamoja na kuomba *visa* kwa nchi ambazo hatuna Itifaki nazo za watu kwenda *freely* yaani ile *free movement*, kama ile Itifaki aliyosema Mheshimiwa Mnyaa kwamba hatujairidhia, havina uhusiano

kabisa, tunasema kuwe na ushirikiano ambao ni *swift*, mtu anayetaka kuja kufanya *research* Tanzania, mtu anayetaka kwenda kufanya *research South Africa* basi ule mpangilio au mchakato wa kuweza kwenda kufanya utafiti upungue na uwe ni nafuu zaidi lakini masharti ya kuingia na kutoka nchini yanaendelea kubaki kama Sheria zilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limezungumzia pesa kiasi gani, je, tumeshaanza kutoa *one percent* ya *GDP*? Niliambie Bunge lako Tukufu pamoja na Azimio la Addis Ababa, karibu nchi zote za Afrika hazijafikia huko lakini zimeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliambie tu Bunge lako Tukufu kwamba kwa mwaka huu katika eneo hili Tanzania imetenga shilingi bilioni 30 na tunaelekea kule pole pole kulingana na uwezo wa bajeti yetu hadi tutakapofika 1% kama ambavyo Serikali imeji-*commit* katika kukubaliana na azimio la kule Addis Ababa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambayo imetolewa kwamba wataalamu sisi tunao wachache sana, kuna *gape* kubwa sana. Katika nchi za SADC Tanzania ni ya pili kwa wataalamu wa sayansi na teknolojia, lakini pamoja na hivyo *South Africa* wenyeewe wataalamu walionao hawatoshi. Lakini kwa kuridhia Itifaki hii na kwa kushirikiana katika sayansi na teknolojia na kwa vile tutakuwa na mahusiano ya karibu, basi hawa wataalamu, hawa watafiti wachache, hawa walimu wachache tunaweza ku-share wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na tunaweza kufanyaje, nitoe mfano tu, sasa hivi kutokana na teknolojia mtu anaweza akatoa mhadhara akiwa Dodoma lakini wanafunzi wapo Dar es Salaam kwa sababu ya teknolojia, kuna kitu wanaita *tele-conferencing*. Sasa kwa kuridhia itifaki hii itatufanya pale tunapokubaliana, tutakapokuwa tumeweka mikakati, mwalimu hata kama yupo *Cape Town*, aweze kufundisha katika Chuo Kikuu chetu hapa Dodoma kwa kutumia hiyo teknolojia. Hakuna *movement* lakini mtu anatoa *lecture* na wanafunzi wetu wanapata, kwa hivyo, jambo hili ni jema sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo au hoja nyingine imetolewa kwamba je, *COSTECH* haitaathirika na kuridhia itifaki hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu niseme kwamba itifaki hii haiondoi mipango ya kila nchi. Kila nchi ina mipango yake, lakini kinachofanyika hapa ni kuweka nguvu kwa pamoja kwa kushirikiana na zile *research* ambazo tutaona kwamba kwa mipango yetu ni vyema tukashirikiana na wenzetu, basi zile pesa tunaziweka kwa pamoja au pale tutakapoonaa kwamba ni vizuri kuomba kwa wafadhili kwa pamoja, basi tutaweka kwa pamoja. Lakini mipango yetu ambayo inahusiana na *COSTECH* haiwezi kuathiriwa kabisa kwa sababu tuna mambo yetu ya ndani na haya ni mambo ya mashirikiano na kwa mipango tuliyonayo sidhani kama ni vyema sana tukaweza kuacha *COSTECH* isiendo kama tulivyojipangia kuwatumia au kuwashawishi wataalamu wetu ambao wapo nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na mikakati tuliyonayo kwanza tunaboresha wataalamu wetu au watafiti wetu kwa kuwapa elimu, kwa kuwapa vifaa vya kisasa na kwa kuhakikisha kwamba wanaboreshewa mishahara yao ili waweze kukaa hapa na mfano mzuri kabisa ni Mheshimiwa Waziri wangu ambaye alikuwa huko Afrika Kusini, mtaalamu aliyebolea, mtafiti aliyebolea kwa miaka 10 lakini leo hii tunaye hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mifano mingine. Pale kwenye taasisi yetu ya Nelson Mandela, kutokana na juhudhi hizi tayari kuna wataalamu wa *ICT*; Profesa mmoja alikuwa Marekani amerudi, kuna Profesa alikuwa *South Africa* amerudi, kwa hivyo mipango na mikakati tuliyonayo nina uhakika itawenza kuwawutia wataalamu wetu waweze kurudi. Lakini vile vile si vibaya wataalamu wetu wakienda kujifunza au kutoa au kushiriki katika tafiti nchi nyingine katika *SADC*, sio moja kwa moja, ili waweze kupata elimu na kupata uzoefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwalipa mafao mazuri nadhani, nimelieleza. Kuendelea kutumia mipango mizuri ya *COSTECH*, nadhani nimelieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Azimio hili, tumejipanga vizuri katika kutekeleza Azimio hili. Kwa mfano hivi karibuni tu Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia amesaini *Bilateral Agreement* na Nchi ya Afrika ya Kusini ambapo *COSTECH* itashirikiana kwa karibu sana na *National Research Foundation* ya *South Africa* yaani ile *COSTECH* ya *South Africa* ili washirikiane kwa *ku-share* wataalamu na kuweka mipango. Halafu vile vile tuna ile *Centre of Excellence* ya kwetu ile yenye *Super Computer* pale *DIT*, wamekubaliana kushirikiana na *High Performance Computer* iliyoko kule *Cape Town*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni machahe tu, lakini vilevile kuna mikakati ambayo kwa kupitia *COSTECH* ambayo ina-*coordinate* tafiti katika nchi yetu ambayo itawezesha Vyuo Vikuu vyetu viweze kupata vifaa, *institutions* zetu za *research* ziweze kupata *funding* ili ziweze kufanya *research* ambazo zitaweza kuleta manufaa kwa Taifa letu. Lakini si hivyo tu, sasa tunatoka kwenye *research* na *development*, tunakwenda mpaka kwenye *innovation*. Ukifika hapo *COSTECH* sasa hivi kuna *centre* ambayo tunaiita *incubation* ambapo wataalamu wanapikwa kuhakikisha kwamba anapotoka hapo, aweze kuchukua ile *knowledge* au *research* aliyonayo kui-*transform* kwenye maeneo ambayo yatakuwa ni ya uzalishaji. Kwa hivyo, nina uhakika baada ya muda mfupi tutakuwa tunafaidika zaidi na *research* zetu ambazo zitakuwa zimefanywa na wataalamu wetu kwa kushirikiana na wataalamu wengine kutoka katika nchi hizi za *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie gharama za mwaka ambazo zimezungumziwa katika hoja hii na hii imezungumzwa na Mheshimiwa John Mnyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu hawa tunaosema wataenda kwenye mikutano, leo hii mkutano wa Mawaziri unaendelea, hivi ni vitu vilivyokuwepo. Sasa tunachofanya hapa ni kuvirasimisha, ili tuirasimishe, ilikuwa *informal* haikuwemo

kwenye Sekretarieti ya SADC; *Science and Technology and Innovation* haikuwemo, kwa hivyo tunachojaribu ni kuunda Idara mpya kule na ndio sababu tukasema hakutakuwa na gharama za ziada katika kuridhia itifaki hii kwa sababu mchango wa Tanzania SADC utaendelea kubaki ule ule na katika bajeti zetu za nchini kwetu, pesa zile zile tulizokuwa tunatumia huko nyuma kwenda kushiriki katika mikutano hii, zitaendelea kubaki zile zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti itakayokuja ni namna ambavyo mipango itaongezeka, lakini hii italetwa kwenye Bunge lako katika Bajeti ya Wizara kwa kila mwaka na itakavyokuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lililosemwa la kwamba pale tunapokuwa tunawasilisha, basi *instruments* za nchi nyingine ziweze kuwasilishwa pamoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazo zuri na kama Bunge lako litaridhia na kufanya iwe ndio utaratibu nadhani hatuoni kama hilo ni tatizo. Ni ushauri mzuri na sisi tunauunga mkono. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

#### **WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kuwashukuru wale wote ambao wamechangia hoja iliyowasilishwa mbele yako. Naomba nianze kumtambua Mheshimiwa Charles Kitwanga, ambaye ni Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Napenda kuwatambua wachangiaji 36 katika kutoa hoja. Waliochangia kwa kusema ni 13 na waliochangia kwa maandishi ni 23. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwashukuru kwa dhati wale wote waliochangia kwa kuongea, nikianza na Mheshimiwa Peter Serukamba ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa mchango wake katika hoja hii. Pia nashukuru michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao kwa kuongea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa ambao wamechangia kwa kuongea amba ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Mbarouk Rajab Mohamed, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dokta William Mgimwa, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa *Engineer* Makame, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla na Mheshimiwa Dokta Binilith Mahenge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wafuatao ambao wamechangia kwa maandishi; Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Sabrina Sungura, Mheshimiwa

Diana Chilolo, Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Agness Hokororo, Mheshimiwa Aina Mwidau, Mheshimiwa Mariam Kisanji, Mheshimiwa Mwanamrisha Taratibu Abama, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhammed, Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Dokta Nyambari Nyangwine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitazungumza mengi kwa sababu karibu wote waliochangia kwa kuongea na wale waliochangia kwa maandishi kwa ujumla wameunga mkono hoja hii na nyingine zinalenga katika kuboresha namna ambavyo nchi yetu itashiriki vyema kwa manufaa zaidi, pale ambapo Bunge lako litaridhia Itifaki hii ya *SADC* ya Sayansi Teknolojia na ubunifu iliyo mbele yetu. Hata hivyo, naomba nitoe maelezo au ufafanuzi kwa mambo machache yaliyosemwa wakati wa kujadili hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na maoni yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Serikali imeyazingatia na itaifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa hoja zilizotolewa na upande wa Kamati ya Miundombinu, naomba nijibu kama ifuatavyo nikianzia na hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Peter Serukamba; hoja ya kwanza ilikuwa Makao Makuu ya Kitengo cha Sayansi, Teknolojia na Ubunifu yawe Tanzania ikiwezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo au jinsi ya kujibu hoja hiyo ni Makao Makuu ya *SADC* yako Gaborone, hivyo basi sio rahisi kuleta Kitengo cha Sayansi, Teknolojia na Ubunifu hapa Tanzania, ilhali makao yake makuu yapo huko na vitengo vyote mara nyingi vinabaki huko Gaborone, Botswana. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwa ni pamoja na sekta binafsi itaendelea na jitihada zake za kujenga uwezo wa asasi za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili kuvutia wanasyansi wengi kutumia uwezo tutakaoujenga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yake ya pili ilikuwa ni Serikali ihamasishé ubunifu na kuhakikisha kuwa wabunifu na wagunduzi wanawekewa mazingira mazuri ya kufanyia kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubaliana na mapendekezo hayo na imeshaanza kuyafanya kazi kwa kuyajumuisha katika Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo. Aidha, mkakati wa kutekeleza sera hii unaandalisha na utaangalia masuala mengi yanayohusu wabunifu na wagunduzi, ikiwa ni pamoja na kuwatambua kwa kutoa tunzo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Peter Serukamba ni mazingira ya wabunifu na wanasyansi wengine ya kufanyia kazi hapa nchini, yaboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inalitambua hili na tayari mchakato wa kuboresha mazingira ya kazi za watafiti umeanza ikiwa ni pamoja na kuangalia upya mfumo wa mishahara yao ambao utalingana na watafiti wa Vyuo Vikuu. Kwa hivi sasa upandishwaji wa vyeo, uimarishaji wa miundombinu ya watafiti na vifaa vingine vitaimarishwa katika vyuo vyetu vya utafiti. Kwa hili, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuendelea kulisimamia suala hili kwa karibu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Peter Serukamba, amekuja na hoja inayosema tuwatambue watafiti na wataalamu walioko nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwatumia wataalamu wa Kitanzania walioko nje ya nchi. Kwa kutambua hili Sera ya Taifa na Maendeleo, inaainisha namna mbalimbali za kuwatumia na kuwavutia watafiti waliopo nje ya nchi kurudi nyumbani. Kufuatia kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya kazi na vitendea kazi vingine. Kwenye suala hili nafikiri Serikali tumeanzisha Chuo chetu cha Sayansi na Teknolojia cha Mandela pale Arusha, chuo ambacho kitachukua tu wanafunzi wa *Masters* na *Ph.D* na vile vile tutakuwa tunawaalika watafiti mbalimbali kutoka nje ya nchi; na hapa tutaangalia hasa Watanzania, waje hapa ili kufanya kazi zao za kitafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo ambalo linafanyika ulimwengu mzima. Kwa mfano, ukienda *South Korea*, kila wakati wa sherehe za mwaka mpya mwezi Desemba, watafiti wengi wa *South Korea* wanaofanya kazi *US*, wanarudi nyumbani kufanya utafiti na sisi tunataka kushirikiana na watafiti wetu ambao wapo nje, wakati wa likizo zao wazitumie nyumbani kwa kuwasaidia watafiti wetu waliopo ndani ili waweze kujenga uzito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyofuata ilikuwa ni Serikali iwekeze zaidi katika utafiti na maendeleo ili nchi iweze kunufaika zaidi na kuridhiwa kwa Itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepokea ushauri wa Kamati. Serikali inaendelea kuwekeza katika utafiti na maendeleo kwa nguvu zote. Ukiacha fedha za utafiti zinazotolewa na Wizara au taasisi nyingine, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Serikali imetenga shilingi bilioni 30 kwa ajili ya utafiti ambapo pesa hiyo imepatiwa *COSTECH*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zinazofuata sasa ni hoja ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani, hoja yenye we inasema kama ifuatavyo; Serikali ijipange vyema katika kutekeleza sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia na sera hiyo ipitiwe, ushauri huu umepokelewa na Serikali na tayari umeshaanza kufanyiwa kazi. Tayari Serikali imeandaa Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo ili kuwekea muongozo masuala ya utafiti kwa ujumla. Vilevile Serikali imeanza mchakato wa kupitia sera ya sayansi na teknolojia ambayo inahusu pia mapito masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuweka misingi bora itakayotuwezesha kusimamia masuala ya utafiti ubunifu na uhaulishaji hii ni pamoja na

kuweka mfumo bora zaidi kwa kuwatambua wagunduzi na kuwasaidia kuendeleza juhudzi zao. Serikali tuna mipango ya kuwasaidia wagunduzi wetu, kwanza tutaanzia kwenye utafiti halafu tuwawezesha kwenda *prototype processing stage* halafu wakishamaliza kwenye *prototype* tutawapeleka waende kwenye *commercialization stage*, halafu tutawasaidia ili waweze kuzitangaza hizo tafiti zao. Kwa hivyo tumeweka mikakati mizuri kama Serikali jinsi gani tutaweza kuwaboresha wabunifu wetu watafiti wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa upande wa hoja zilizotolewa na wasemaji wa Kambi za Upinzani zimeisha, sasa naomba niende kwenye hoja zilizotolewa na wachangiaji, kwanza naomba nianze na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, hoja yake inasema kama ifuatavyo, kwanza kuwekeza katika tafiti, kuongeza Bajeti katika kuwekeza katika utafiti Serikali kama nilivyosema imetenga shilingi bilioni 30 mpaka sasa hivi tumeshapokea shilingi bilioni 4, katika bilioni 4 hizo tumedhamini wanafunzi 198, wanafunzi 142 wanasoma *Masters* (Uzamili)na vilevile tumedhamini wanafunzi 56 ambaa wanafanya *PhD*.

Vilevile katika hilo tulipokea maombi ya utafiti 380 kwenye maombi hayo tumeangalia kwa makini na tumehakikisha kwamba tunachukua yale maombi ambayo yana sifa za hali ya juu, mpaka sasa tumetenga maombi 106 ambayo tutachangia kwa ajili ya kuwawezesha kuweza kufanya utafiti. Kati ya hizo tayari maombi tisa sasa tumeshazipa mwega au tumeshazi-*support* na tumezi-*support* kwa kutumia shilingi milioni 900. (*Makofî*)

Hoja nyingine anasema Mheshimiwa Jenista kwamba kuwatambua watafiti na wabunifu wetu katika hili tuna mpango kama Serikali kuweka *database* ya watafiti wote wa hapa nchini na wengine wale ambaa wapo nchi za nje ambaa ni Watanzania ni muhimu kuweka *database* kama tutakuwa tunatakuwa kuwatumia ama kutakuwa na ushauri wowote ili tuweze kuwasiliana nao kwa rahisi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ameendelea kutoa hoja nyingine kuhimiza vijana wa shule za sekondari katika masomo ya sayansi, hili kama Serikali tumeona ni wazo muhimu sana na ni lazima tuhamasishe sayansi kwenye masomo yetu. Vinginevyo hii mipango yetu yote haitoweza kwenda kama huku chini hatukujenga *base*, *base* ni muhimu sana kwa vile sisi tumeweka mikakati mizuri ya kufundisha masomo ya sayansi na hesabu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jenista Mhagama aliendelea kutoa hoja kuwa wataalam wa Tanzania walio nchi za nje warudi nyumbani na kushirikiana na wataalam waliopo ndani, hii ni hoja nzuri na sisi Serikali kama nilivyosema tumeanzisha chuo chetu cha Mandela ambacho chuo hicho kitawaita au kitawakaribisha watafiti wetu walioko nje ili waweze kuja kufanya tafiti hapa nchini na kushirikiana na wataalam wetu wa ndani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Regia Mtema, ye ye amezungumzia kwanza hoja ya *gender*, *gender* ni

muhimu sana kwenye mambo ya utafiti na sisi kama Serikali tunataka kuweka kipaumbele kwa watafiti wanawake. Tunataka kuweka *funds* maalum au pesa kwa ajili ya *women researchers*, wanawake wanaofanya *research* vilevile na kwa *younger researchers* kwa sababu kama hatukufanya hivyo hatuteweza kuwajengea uwezo tuboreshe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima *research* kwa akinamama na vilevile kwa vijana ili tuweze kuwajengea uwezo na wao waweze kushiriki katika maendeleo au kujenga maendeleo ya nchi yetu. Vilevile Mheshimiwa Mbunge ametoa hoja kwamba tufikirie jinsi gani tutaweza kuboresha ofisi zetu kwa mfano yeye mwenyewe inakuwa ni vigumu kwenda kutoka *floor* moja au kwenda nyingine hili ni suala muhimu sana nafikiri na sisi kama Serikali tutaliangalia jinsi gani tutakavyoweka *specially elevators* kwa watu wenyewe ulemavu ili waweze kufikia kwenye ofisi wanazozihitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Mheshimiwa Herbert Mntangi ametoa hoja ya kuongeza ushirikiano katika nchi za *SADC*, wazo hili nzuri na nafikiri ni muhimu sana kujua kwamba *research* huwezi kufanya wewe peke yako, *research* ni muhimu kufanya na *team* ya watafiti na *team* hiyo inaweza kutoka nchi mbalimbali, kwa vile ushirikiano katika *research* ni jambo muhimu sana ni muhimu tushirikiane na *researchers* kutoka nchi zote za *SADC* kuanzia *South Africa*, Botswana, Malawi na kadhalika, kwa sababu gani? Kwa sababu wenzetu wengine wanajua au wana uwezo mkubwa na sisi vilevile tuna uwezo mkubwa kuliko wenzetu katika maeneo mengine kwa kushirikiana na kwa kubadilishana mawazo ninaamini tunaweza kutatua matatizo yanayotukabili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ameendelea kusema hapa Mheshimiwa wabunifu wetu wazingatiwe *COSTECH* tunaipa nguvu na tutaendelea kuipa nguvu kama nilivyosema mwaka huu wa fedha tulianzia shilingi bilioni 30. Hizi ni ndogo lakini hizi ni nyingi kwa sababu tatizo kubwa linalotukabili watafiti wengi wa Tanzania hawana ile *culture* ya kufanya *research*. Leo utashangaa Mheshimiwa tumepata *proposals* ambazo mtu anaomba shilingi milioni tano, shilingi milioni tano huwezi kufanya *research* pesa ndogo sana, sisi tuna *encourage researchers* wetu walete *proposal* za uhakika kuanzia milioni 100 na kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutaki mtu anatuletee *proposal* ya shilingi milioni mbili, shilingi milioni mbili ni kwa ajili ya tiketi ya *economy class* kwenda Nairobi. Huwezi kufanya *research* na pesa ndogo kama hii. (*Makofi*)

Vilevile hatutaki *proposal* ya mtu mmoja, kwenye *research* huwezi kufanya kazi wewe mtu mmoja, tunataka *as a team*, *we need a team* ya watu kama wanenye, watano kwa sababu mlikifanya *as a team* mtawezwa ku-solve problem vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo timu tunataka kuwe na wanafunzi, kwa sababu kazi kubwa ya *research* ni kuboresha taaluma, kwa wanafunzi wetu, hiyo ndiyo sababu leo Tanzania *Universities* zote zina matatizo ya walimu kwa sababu tulishindwa kufanya *research on time* ama tulifanya *research* chini ya uvungu, ya mtu mmoja, mmoja.

Tunatakiwa tufanye *research as a team* halafu tuwe na wanafunzi wa kutosha, kwa vile *COSTECH* ipo na inaendelea kufanya shughuli zake na tutazidi kuimarisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho Mheshimwia Mbunge alisema kwamba tuvisaidie vyuo vyetu nya utafiti, ni kweli sisi tuko tayari kuwasaidia lakini *research* zinavyofanywa ulimwengu mzima huwezi kumpa mtu tu *research funds*. Kitu cha mwanzo unaitisha *research call* na kila mtu ana *compete* (anashindana). Sasa mtu anakuletea *proposal page* moja, hajaonesha atafanya nini, hajaonyesha watu wangapi watashiriki kwenye tafiti hiyo, huwezi ukampa *funds*. Sisi tuna *encourage institution* zetu zote zi-*apply* na walete *research proposal* ambayo iko kwenye *good standards*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunajua wengine hawana uwezo kwa mfano kule Zanzibar Chuo cha Kilimo cha Kizimbani hawana uwezo wa kuandika *good research proposal* lakini sisi tunawasaidia ili na wao tuwawezesha. Hii ndiyo kazi ya Wizara ya Sayansi, ndiyo kazi ya *COSTECH*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kujibu hoja za Wabunge hapa tunaye Dokta Mgimwa ambaye ye ye amezungumza kutenga Bajeti ya kutosha. Hii nimeshaizungumza, Bajeti yetu bado iko ndogo, na hili si tatizo kwa Tanzania tu kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema hili ni tatizo kwa Afrika nzima. Ni nchi pekee ambayo sasa inakaribia 1% *GDP* ni *South Africa* ambayo wana 0.95% Tanzania mpaka sasa hivi tuna 0.025% *GDP* ambayo ni ndogo lakini angalau tumeanza. Mkumbuke kwamba Roma haikujengwa siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile twende hatua kwa hatua na sisi tutafika, alisema tuanzishe *academy of science*, *academy of science* nafikiri ni nzuri lakini kwa Tanzania hatujafikia kwenda kwenye *academy of science*, *as a research institution*, nakumbuka *academy of science* ziko *Russian Academy of Science*, *Hungarian Academy of Science* na *Poland Academy of Science*. Kwa sisi bado hatujafikia huko lakini sisi tunasema tunaanzisha *Mandela Institute of Science and Technology* pale tutakuwa tunawaleta wataalam wetu watafanya utafiti na tutaendelea. Kwa hiyo, suala la kuanzisha *academy of science* ni nzuri lakini kwa upande wa *research* nafikiri bado. Lakini Tanzania tunayo *academy of science* sasa hivi lakini yenyewe haifanyi kazi vizuri nafikiri sisi tutajaribu kuiboresha ili ifanye kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Godfrey Zambi, ye ye amezungumza sana kuhusu *COSTECH*, kwanza nafikiri tunataka tuelewe nini *mandate* ya *COSTECH*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *mandate* ya *COSTECH* sio kufanya *research* ni ku-*monitor* na ku-*manage* ile *research* kama inavyotakiwa ifanyike sio wao kuanza kufanya *research*, hapana *COSTECH* hawatakiwi wafanye *research*, *COSTECH* wanatakiwa wapewe pesa (shilingi bilioni 30) wazigawe kwenye zile *research institutions* na waanze kuangalia je, zile pesa zimetumika ipasavyo. Hii ndiyo kazi ya *COSTECH*. Sisi *COSTECH* tutaendelea kuwawezesha lakini sio kazi yao kufanya *research*, lakini wao kazi yao ni kuangalia tufanye nini kwenye *research*, jinsi gani tuweze kuboresha

*research*, jinsi gani tuweze kugawa hizo *funds* vizuri, jinsi gani tunaweza kupata matokeo mazuri ya ya utafiti na kuzipeleka kwa wananchi na kuzitumia. Hiyo ndiyo kazi ya COSTECH. (Makofi)

Lakini wao sio kufanya utafiti, hii nafikiri watu wengi wana-*confuse*, wanafikiri kwamba kazi ya COSTECH ni kufanya utafiti, sio kweli bwana wao ni ku-*monitor research* na ku-*manage* hiyo *research process funding*, lakini sio wao kufanya utafiti naomba hiyo tuelewe sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tutaendelea kuwaendeleza COSTECH. Ni kweli COSTECH sasa hivi wanajishughulisha sana na ubunifu, inabidi tubadilishe ile sera na sheria ya COSTECH ili waangalie mambo ya utafiti, ubunifu na sayansi pamoja, kwa sababu vinginevyo *mandate* yao ilikuwa haisemi hivyo. Wizara ipo katika *process* ya kufanya hivyo. (Makofi)

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi tunaipitia upya sera yetu ya STI ambayo ni Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili iweze kukidhi mahitaji ya wananchi au mahitaji ya wakati tulionao. Sasa tunaelekea kwenye kuitumia sayansi kwenye maendeleo ya nchi, ni lazima tuwe na sera ambayo inatuelekeza mambo ya ubunifu, kwa hiyo suala hili ni muhimu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Pindi Chana, alizungumzia kuhusu jinsi ya kuboresha kwanza sayansi kwa kuanzia kuwatunukia hawa watafiti wetu, ni kweli kama sisi Wizara tuna mipango kabambe ya kuwatunukia watafiti wetu kuanzia *senior research award*, *women research award* na kadhalika. Tunataka kuanzisha hizi *awards* ambazo tutapendekeza Mheshimiwa Rais awe anatoa hizi *award* kwa watafiti wetu. Tutaanza kwa *senior research award* kwa mtafiti bora tumpe zawadi halafu vilevile tutakwenda kwa *woman research award* kwa ajili ya mtafiti bora wa kike na *younger research award*, kwa ajili ya mtafiti kijana anayefanya vizuri. Hii ni muhimu sana kuwashamasisha watafiti wetu vinginevyo watakata tamaa. Sisi kama Serikali hiyo tumeiona na tunaifanyia kazi. (Makofi)

Vilevile Mheshimiwa Mbunge alizungumzia kwamba wakati umefika sasa shule zetu zianze kufundisha masomo ya teknolojia. Hili sisi tunakubaliana naye mia kwa mia na kama Serikali tuna mpango wa kuunganisha shule zetu na mkongo wa Taifa. Sasa kwa kupitia mkongo wa Taifa shule zote zitaunganishwa na zikiunganishwa tunategemea twende *e-learning*. Tutakwenda kwenye *e-book*. Tubadilishe vitabu vyetu vyya kawaida kwenda kwenye *electronically* ambao wafaidike wananchi wetu wote au wanafunzi wetu wote. Hayo Mheshimiwa ni masuala ambayo nimeyapata kwa wale ambao waliosema. Sasa naenda kwenye masuala ambayo walileta maandishi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa wengi sana walileta *comment* zao au walileta hoja zao kwa maandishi ni hoja nyingi sitoweza kuzitaja moja baada ya nyingine lakini nitachagua baadhi ambazo nitazzungumza hapa.

Hoja ya kwanza ilikuwa inatoka kwa Mheshimiwa Aina Mwidau, ambaye pia alisema hoja yake ya Serikali kuweka utaratibu wa kuwatambua wabunifu na kuwawezesha ili kuwapa moyo na kuendeleza vipaji vyao. Hili ni suala ambalo tumelizingumza kama Serikali sisi tumeweka mikakati mizuri ya kuhakikisha tunawatambua wabunifu wetu wote na pale inapowezekana tutawazawaidia zawadi ambazo tutawapa kwa wale wabunifu bora. Lakini Waheshimiwa Wabunge nataka muelewe sio kwamba kila mbunifu atapatiwa zawadi, kuna *procedures* ambazo tunazifuata kuchagua wabunifu bora, kila mbunifu tutamtambua. (*Makofi*)

Halafu kuna hoja nyingine ya Mheshimiwa Mbunge inarejea rejea kuwa Serikali ijipange vyema zaidi kugharamia utafiti. Kama nilivyosema Serikali ipo katika mipango mizuri ya kujipanga na kuweka fedha za kutosha kwenye utafiti, kwanza kuanzia na shilingi bilioni 30 na hiyo Bajeti yetu itaendelea kukua muda baada ya muda. Kwa vile Serikali tumejipanga vizuri na tunataka watafiti wetu nao wajipange vizuri hiyo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwengine ni Mheshimiwa Susan Kiwanga ambaye anasema Serikali ijipange vizuri ili kuhakikisha kuwa tutakapoanza utekelezaji wa itifaki hii tutaweza kupata manufaa mazuri.

Sisi kama Serikali tumeanza kujipanga vizuri na kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema, wiki iliyopita tulitiliana mkataba wa makubaliano na Serikali ya Afrika Kusini jinsi gani tunaweza kushirikiana na wao. Tuliamua kushirikiana kwanza kwa maeneo mawili baina ya kituo cha *Computer cha Dar es Salaam Institute of Technology* na *Cape Town High Performance Centre* ambapo ushirikiano utaanza hapo na vilevile tunesema tuenze ushirikiano baina ya *COSTECH* na *National Research Foundation*. Kwa hivyo, kama Serikali tumejipanga vizuri na tutahamasisha watafiti wetu au *researchers* wetu waweze kuitumia nafasi hii vizuri. (*Makofi*)

Mwingine ni Mheshimiwa Mariam Kisangi, ye ye ana hoja kwamba katika kutekeleza itifaki hii makao makuu yaye nchini Tanzania. Kama nilivyosema siyo rahisi makao makuu ya *unit* hii au kitengo hiki cha Sayansi na Teknolojia kuwepo Tanzania. Makao makuu na Idara zote za *SADC* zinakuwepo huko Gaborone, Botswana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingi hapa lakini zinazungumzia mambo yale yale, lakini kuna hii hoja ambayo ni muhimu sana nayo ni kuhusu Watanzania waliopo nje ya nchi kuwavutia kurudi nyumbani Tanzania. Nafikiri kuwepo nje ya nchi siyo tatizo, kwa mfano mimi nimekaa miaka 10 nje ya nchi, ukiniuliza katika miaka hiyo 10 nimefanya nini kwa Tanzania. Nikiwa *South Africa* mimi mwenyewe nilichukua wanafunzi wanenye wa *Masters* na mwengine mmoja wa *PhD* tumewasomesha bure. Sasa Watanzania kuwepo nje si tatizo nafikiri wakati tunawahitaji waje nchini waweze kufanya kazi zile tunazowatuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kumalizia naomba niwataje Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi nao ni Mheshimiwa Nyambari Nyangwine na ye ye vilevile amechangia kuhusu kuboresha *COSTECH*, sitaizungumzia

sana. Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Agness Hokororo, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour ambaye ye ye amechangia kwamba uchakachuaji wa mafuta bado ni tazito kubwa, hili suala tutalipeleka kwenye Wizara husika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi, Teknolojia *of course* tunahusika katika kujipanga kwenye teknolojia ambayo inaweza kuzuia ule uchakachuaji wenyewe lakini hili tutalipeleka kwenye Wizara husika. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya amechangia uendelezaji wa *ICT* katika eneo la *TIRDO* kwa ajili ya *incubations*, Serikali inalitambua hilo na uwezo wa *TIRDO* katika kuendeleza masuala ya *ICT*, mipango ya awali imeanza kutumika ili kuona jinsi gani tutaitumia *TIRDO* kwa ajili ya kuanzisha hizo *incubations*.

Vilevile Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya amechangia kuhusu kuainisha itifaki na sheria zetu, Serikali italifanyia kazi pendekezo hili ili kuhakikisha kuwa itifaki hii inakwenda na sheria za nchi. Pia amechangia kuhusu kuimarishe mawasiliano hadi vijijini kupitia *ICT*, sisi kama Serikali tumelipanga hilo na tayari tunalifanyia kazi, kuna maeneo tofauti ambayo tumeyaona na kwa kutumia mfuko wetu wa mawasiliano kwa wote kwa kushirikiana na sekta binafsi tutayapelekea maeneo hayo mawasiliano. (*Makofi*)

Vilevile Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, ye ye hoja yake ni kuanzisha vituo vya kuwaendeleza wabunifu. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea na juhudzi za kuanzisha vituo vya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ikiwa ni pamoja na viatamizi kwa ajili ya ngazi mbalimbali. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Ritta Kabati naye amechangia kuhusu kuipongeza Serikali kwa kuanzisha mfuko maalum wa kuwasomesha wasichana. Maeleo ya Serikali ni kwamba imepokea pongezi hizi na itaendelea kuboresha mipango yake ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wengi wasichana kwa wavulana wanasona masomo ya sayansi na teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali Wizara imepokea maoni yote na tunaahidi kuwa tutayafanyia kazi kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha kuwa nchi yetu inapata manufaa stahili kupitia itifaki ya *SADC* ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ambayo Bunge lako tukufu limeombwa kuridhia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**(Azimio la Kuridhia Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*The SADC Protocol on Science, Technology and Innovation*)**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa. Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa hotuba nzuri uliyoitoa na kupitia michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na suala lililo mbele yetu. (*Makofi*)

Sasa katika utaratibu wa kushughulikia maazimio wakati huu ni kwamba Azimio la Kuridhia Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika yaani *The SADC Protocol on Science, Technology and Innovation* limepitishwa rasmi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa Dodoma leo tarehe 14 Aprili, 2011 wakati wa Mkutano wa Tatu, kikao cha saba. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, katika utaratibu wetu wa maazimio hapo ndipo tumefikia mwisho wa azimio hili na kwa niaba yenu nimtakie kila la kheri Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote wanaohusika na Wizara hii katika kushughulikia mambo yanayohusiana na azimio hili ili Tanzania tuweze kufaidika zaidi na zaidi katika ushirikiano wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, kwa maana hiyo nawatakia kila la kheri. (*Makofi*)

Naomba nimalizie kwa matangazo ambapo nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho tarehe 15 Aprili, 2011 saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa kutakuwa na Mkutano Mkuu Maalum wa masuala ya CPA yaani *Commonwealth Parliamentary Association* tawi la Tanzania ambapo pamoja na mambo mengine kutakuwa na suala la uchaguzi. Kwa mujibu wa Kanuni za CPA kila Mbunge ni mjambe na hivyo ana haki ya kupiga au kupigiwa kura, muda wa kurejesha fomu za waliokuwa wanagombea umemalizika leo saa 10.00 jioni, hivyo tunaombwa kushiriki katika uchaguzi mkuu wa tawi hiyo kesho saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Msekwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pamekuwa na tatizo kidogo la kuhamahama kwa baadhi ya Wabunge katika viti mbalimbali. Kwa hiyo, ofisi inawaomba kwa yule ambaye jina lake limekaa sawa sawa na pale anapokaa haina tatizo lakini kwa yule ambaye jina linaonekana ni tofauti basi uandike jina ambalo ungependa lifahamike kwa sababu ofisi kwa baadaye inaweka *label* za chuma za kuonyesha jina lako vizuri. Lakini vilevile inatusaidia katika karatasi za mahudhurio na mambo mengine mbalimbali ilikuweza kujua *rows* zilivyokaa sawa sawa. (*Makofi*)

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyaa, Naibu Spika anaongea unaomba mwongozo?

Inasaidia pia kwa Mheshimiwa Spika na Naibu Spika au Mwenyekiti wa Bunge anapokaa hapa ni rahisi kujua Mheshimiwa ukisimama kuuliza swali kwa sababu ukiwa unakaa katika *position* ile ile ni rahisi zaidi kufahamu kuliko mtu akihama inakuwa taabu kidogo. Kwa hiyo, tunaomba ushirikiano katika jambo hilo. (*Makofî*)

Tangazo la mwisho naomba niwakumbushe najua nyote mnafahamu Wabunge wa CCM kwamba baada ya hapa tunaelekea kwenye kikao maalum cha uchaguzi katika ukumbi wa Msekwa naomba nitumie fursa hii kuwatakia kila la kheri wagombea wote washinde ili wawe Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM. (*Makofî*)

Sasa Mheshimiwa Mnyaa karibu.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba mwongozo wako kwa hekima za kitu chako, kesho ni siku ya Ijumaa yaani ni siku ya Ibada kwa Waislamu wote ambapo saa 7.00 mchana kufanya huu Mkutano wa CPA ina maana baadhi ya Wabunge utawakosa kuhudhuria na wangependa wawepo. Ninaomba kitu chako kitumie busara siku ya kesho Ijumaa saa 7.00 mchana Wabunge wapate fursa na kama uwezekano kuahirishwa itafutwe siku muafaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo na hekima zako. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, asante sana. Kwa vile suala ulilolitoa ni zito na ni suala la imani ya dini, basi niseme tu kwamba kesho utatolewa mwongozo asubuhi na Mheshimiwa Spika atakapokuwa hapa kwamba uchaguzi huu utafanyika wakati gani mwingine. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo haya mtaona kwamba katika *Order Paper* ya leo ilikuwa vilevile tushughulikie Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma wa mwaka 2010 yaani *The Public Procurement Bill, 2010* suala hilo pia litatolewa maelezo na Mheshimiwa Spika baada ya kipindi cha maswali kesho asubuhi. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho asubuhi.

(*Saa 12.55 jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 15 Aprili, 2011 saa tatu asubuhi*)